**30 JANUARI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

**Kikao cha Tatu – Tarehe 30 Januari, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tuketi.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Maelezo ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu Muswada wa Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania wa Mwaka 2024.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Maelezo ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Muswada wa Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania wa Mwaka 2024.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Mwantumu Mzamili Zodo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 41

### Upatikanaji wa Maji ya Uhakika Shuleni

**MHE. MWANTUMU M. ZODO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaweka mkakati madhubuti wa upatikanaji wa maji ya uhakika kwenye Shule za Msingi na Sekondari nchini?

**SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zainab Katimba, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali kuhakikisha upatikanaji wa maji ya uhakika kwenye shule za msingi na sekondari nchini. Mikakati hiyo ni pamoja na kutoa fedha kwa baadhi ya shule kwa ajili ya kuchimba visima virefu na vifupi, kutoa fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu ya kuvuna maji ya mvua na kununua matanki makubwa kwa ajili ya kuhifadhia maji na kutoa elimu ya namna ya kuhifadhi vyanzo vya maji vilivyopo katika maeneo yao ili maji hayo yasaidie kutumiwa na shule zilizopo jirani na vyanzo hivyo.

Mheshiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI itaendelea kushirikiana na Wizara ya Maji kuhakikisha kuwa shule za msingi na sekondari zinapata vyanzo vya maji vya uhakika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwantumu Zodo, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Serikali wameahidi watashirikiana na Wizara ya Maji kwa ajili ya kuhakikisha shule zetu zinapata maji, na kwa kuwa hali ni mbaya sana kwenye shule zetu, hasa za kutwa, naiomba Wizara ya TAMISEMI ifanye mazungumzo na Wizara ya Maji kwa kuwa, Mheshimiwa Rais pia, ametoa magari nchi nzima kila mkoa kuhakikisha shule zile zinapata maji.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, je, Wizara ya TAMISEMI ina mkakati gani wa kuhakikisha kwenye shule zote, hasa hii miradi mipya, zile barabara zinapitika muda wote? Kwa sababu, mbali na changamoto ya maji, pia changamoto kubwa huwa ni barabara hasa kwenye miradi mipya ambayo Mheshimiwa Rais amepeleka fedha nyingi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa kwa kweli, hata mimi umenichanganya kidogo. Swali lako linahusu upatikanaji wa maji, sasa hivi umesema barabara au nini, kwa ajili ya hili neno shule? Kwa hiyo, barabara zinazoenda shuleni?

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Spika, barabara zinazoenda shuleni, kwa sababu, Naibu Waziri ambaye yupo hapo, ndiye anayeshughulikia shule.

**SPIKA:** Naibu Waziri kusimama hapa haimaanishi anaulizwa swali lolote. Ni kwenye swali la msingi, ndiyo maana nimekuuliza ni barabara zinazoelekea shuleni?

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Spika, zinazoelekea shuleni kwa sababu, changamoto kubwa huwa ni maji na barabara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hoja ya nyongeza inayohusu swali hili ni lile alililoleta ombi la kutumia yale magari ambayo Serikali imepeleka kwenye mikoa ili ikachimbe visima. Ameleta ombi kwamba, ninyi mshirikiane, na kwa hiyo, pokea hilo ombi lake hilo. Swali la barabara, kama una majibu, mjibu; kama hauna majibu, ataleta kama swali la msingi ili aweze kujibiwa kikamilifu na Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya ya uwakilishi. Kuhusiana na swali lake la kwanza, naomba nimhakikishie kwamba, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha katika shule zetu za msingi na sekondari, huduma muhimu ya maji safi na salama inapatikana.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi uliowekwa, msingi wa ugatuzi wa madaraka kutoka Serikali Kuu kwenda kwenye Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa, halmashauri zina wajibu wa msingi wa kuhakikisha kwamba katika hizi shule zetu za sekondari na msingi maji safi na salama yanapatikana.

Mheshimiwa Spika, japokuwa Serikali Kuu huwa inaleta fedha katika baadhi ya miradi kwa ajili ya kusaidia katika eneo hili la upatikanaji wa maji safi na salama katika shule za msingi na sekondari, lakini wajibu wa msingi bado upo katika halmashauri zetu. Hivyo, nichukue nafasi hii kuendelea kuwakumbusha Wakurugenzi kuhusiana na suala hili na jukumu lao la msingi la kuhakikisha kwamba, katika shule zetu za msingi na sekondari, maji safi na salama yanapatikana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameleta mitambo 26 katika kila mkoa Tanzania Bara kwa ajili ya uchimbaji wa visima. Kwa hiyo, Wakurugenzi watumie nafasi hii, wawasiliane na mamlaka za maji za mikoa kupitia Ofisi ya *RAS,* ili waweze kupata mitambo hii kwa gharama nafuu na kwenda kuchimba visima katika shule zao Pia kuna namna nyingine nyingi za upatikanaji wa maji safi na salama na waweze kutumia nafasi hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa tumeelewa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, swali la pili la Mheshimiwa Mbunge, kuhusiana na upatikanaji au ujenzi wa barabara kuelekea katika maeneo ya shule zetu hizi, Serikali inafanya hivyo, inatambua kwamba, ili shule zetu ziweze kufikika kirahisi zinahitaji barabara nzuri.

Mheshimiwa Spika, kila mwaka wa fedha Serikali inatenga bajeti, kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya barabara zetu za wilaya na kipaumbele kinawekwa kujenga maeneo yale ambayo yanaelekea katika shule, vituo vya afya na maeneo mengine yanayotoa huduma za msingi kabisa katika jamii. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mwantumu Zodo, Serikali itazingatia ushauri wake.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge mliokuwa mmesimama nimewaona, maswali mafupi, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu mafupi. Mheshimiwa George Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Serikali, imejenga vyoo kwenye shule nyingi sana, lakini vyoo vingi ni vya kutumia maji *(flush toilets)*. Kwenye maeneo ambayo hawajapeleka miradi ya maji kwa ajili ya *flush toilets*, ni lini Serikali itapeleka huduma hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Joseph Kakunda kwamba, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha katika shule zetu za msingi na sekondari huduma ya maji safi na salama inapatikana. Kwa misingi ya ugatuzi wa madaraka kutoka Serikali Kuu kwenda kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa, halmashauri zina wajibu wa msingi wa kuhakikisha kwenye hizi shule zetu maji safi na salama yanapatikana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niendelee kutoa msisitizo, kuwakumbusha Wakurugenzi kuhakikisha wanatimiza wajibu wao wa

msingi wa kupeleka huduma za maji safi na salama katika shule zetu ili wanafunzi wapate mazingira mazuri.

**SPIKA:** Ahsate sana. Mheshimiwa Dkt. Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, kwa majibu ya awali ya msingi ya Mheshimiwa Naibu Waziri, swali langu limejibiwa.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, Mbunge wa Kalenga, sasa aulize swali lake.

Na. 42

**Kuwasikiliza Wananchi wa Kitongoji cha Bandabichi cha Kalenga**

**MHE. JACKSON G. KISWAGA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasikiliza Wananchi wa Kitongoji cha Bandabichi, Kijiji cha Ifunda, ambao walihamishiwa katika Kijiji cha Kivalali bila ridhaa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya mipaka ya maeneo ya utawala yamekuwa yakifanyika kwa kuzingatia Mwongozo wa Uanzishaji wa Maeneo ya Utawala katika Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2014. Serikali kupitia barua yenye Kumb. Na. *CFA*.89/141/01/"C"/19 ya tarehe 16 Januari, 2024 ilipokea ombi la kuhamishwa Vitongoji vya Kibaoni B, Bandabichi na Ifunda Sekondari vilivyopo Kijiji cha Bandabichi, Kata ya Ifunda, vihamie Kijiji cha Ifunda. Aidha, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeshafanyia kazi maombi hayo na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 796 la Agosti, 2024.

Mheshimiwa Spika, ikiwa kusudio la sasa ni kukirejesha Kitongoji cha Bandabichi katika Kijiji cha Bandabichi kilipokuwa awali, naishauri halmashauri kufuata utaratibu ulioainishwa kwenye Sheria ya Uanzishwaji wa Maeneo ya Kiutawala kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naishukuru Serikali kwa hizo hatua za awali na mchakato umeshaanza. Ombi langu, ni kwamba huo mchakato ukamilike kwa maana hata hilo eneo la Bandabichi tayari limeshaombewa. Ahsante sana kwa hatua hiyo, sina swali la nyongeza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, pokea ombi hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, nimepokea. Tutafuatilia kwa karibu ili waweze kukamilisha hizo hatua na sisi tutachukua hatua kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, kwenye Jimbo la Ndanda, Vijiji vya Pangani, Sululu ya leo na vijiji vingine vingi kwa muda mrefu vimeleta maombi kwenye Wizara hii ya TAMISEMI ili kuweza kupata namba za vijiji. Nataka kufahamu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, je, ni lini vitongoji hivyo vitapata namba za vijiji kwa sababu ni vikubwa sana na vinakidhi vigezo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Cecil Mwambe, tuweze kuwasiliana kufanya ufuatiliaji wa hatua ambayo maombi hayo yamefikia ili tuweze kuyafanyia kazi kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Lulindi, sasa aulize swali lake.

Na. 43

**Ajira za Muda Kutolewa kwa Watu Wasio na Ajira**

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA** aliuliza: -

Je, kwa nini ajira za muda kama za kuandikisha wapiga kura zisitolewe kwa watu wasio na ajira badala ya kuwapa watu walioajiriwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ajira za muda za uandikishaji wa wapiga kura zipo kwa mujibu wa Kanuni ya 9 (2) ya Kanuni za Uchaguzi za Mwaka 2024. Tangazo la Serikali Na. 572 na Kanuni ya 10 (2) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za Mwaka 2024, zinaelekeza Msimamizi wa Uchaguzi kufanya uteuzi wa watumishi wa umma watakaoandikisha na kuandaa orodha ya wapiga kura.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024, shughuli nyingine za ukarani (usaidizi katika vituo) zilitolewa pia, kwa watu wasio na ajira katika vituo vipatavyo 80,584.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchungahela, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, mara nyingi Serikali imekuwa haitoi fursa kwa wasomi ambao wamewasomesha wenyewe na hivyo, kujinyima haki ya kutumia fursa hizo, halikadhalika wamekuwa wakitoa ajira kwa watu ambao tayari wana ajira.

Hawaoni kwa kufanya hivyo wanazorotesha huduma zinazotakiwa kutolewa na waajiriwa hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, kwa kufanya hivyo, hawaoni kuwa, inawanyima fursa watu wasiokuwa na ajira angalau wapate kifuta machozi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Issa Mchungahela kwamba, Serikali inatambua na inathamini vijana ambao wamehitimu na wanataaluma tofauti tofauti na ina dhamira ya dhati kabisa ya kuweza kuwaajiri katika hizi ajira rasmi. Serikali imekuwa ikifanya hivyo, ikitangaza ajira na vijana wamekuwa wakiomba nafasi hizo. Kwa hiyo, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na wasomi na kuwatumia katika Serikali.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi, kwa muktadha wa kazi hii katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kuandaa orodha ya wapigakura, Sheria na Kanuni zimetoa mwongozo wa kutumia watumishi wa umma kwa ajili ya kufanya kazi hii, lakini kuna kada nyingine ambazo ajira zinatangazwa na Serikali na wasomi wetu wanaweza kuomba.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii kuendelea kuwapa moyo Watanzania ambao wamesoma, wana vyeti vyao na wanatafuta ajira, wafuate utaratibu. Serikali inapotangaza ajira waweze kuomba na watapata ajira kwa nafasi zinazokuwa zimetangazwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Mheshimiwa Abdul Yussuf Maalim, Mbunge wa Amani, sasa aulize swali lake.

Na. 44

**Tathmini ya Kaya Maskini – Zanzibar**

**MHE. ABDUL YUSSUF MAALIM** aliuliza: -

Je, tathmini ipoje juu ya maendeleo ya kaya maskini zilizodhaminiwa na *TASAF* kwa upande wa Zanzibar?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Deus Sangu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, tathmini kubwa ya Kipindi cha Kwanza cha Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini ilikamilika Mwaka 2019 na kipindi cha pili itakamilika mnamo Juni, 2025. Kwa upande wa Zanzibar, Tathmini kubwa ya kipindi cha kwanza cha Mpango ilionesha mafanikio makubwa katika maeneo mbalimbali kama vile, walengwa wanapata mahitaji ya msingi ya maisha kama vile chakula, vifaa vya skuli kwa watoto na makazi ya kuishi kuboreshwa; kuongezeka kwa mahudhurio ya watoto shuleni kufikia 95% na pia, viwango vya ufaulu; wazazi kupeleka watoto kliniki kwa zaidi ya 95%, kwa ajili ya ushauri wa kitaalam; na kuongezeka kwa mzunguko wa fedha katika shehia hivyo, kuchochea ukuaji wa shughuli za uchumi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdul Yussuf Maalim, swali la nyongeza.

**MHE. ABDUL YUSSUF MAALIM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Naomba kuuliza maswali madogo

mawili ya nyongeza. Kwa kuwa fedha hizi za Mfuko wa *TASAF* huwa zinachelewa, je, Serikali ina mkakati gani wa kuharakisha fedha hizi ili ziweze kunufaisha wananchi kwa wakati?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza wanufaika wa Mfuko huu wa Maendeleo wa *TASAF* ili kuweza kuwanufaisha wananchi wakiwemo wa Jimbo la Amani? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwanza nimpe pole Mheshimiwa Abdul kwa matatizo aliyoyapata, lakini namshukuru Mwenyezi Mungu, amerudi akiwa salama na anaendelea kupambana kuwatetea wananchi wake wa Jimbo la Amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikijibu maswali yake mawili ya nyongeza, kwanza ameuliza habari ya fedha za Miradi ya *TASAF* kuchelewa. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, siyo kwamba fedha hizi zinachelewa, isipokuwa utekelezaji wa miradi hiyo unahusisha wadau mbalimbali. Kwa mfano, tunapopeleka fedha zile zinakwenda kuhudumia sekta ya elimu, maji na afya. Sasa pale kuna wadau kama Wizara ya Elimu, Wizara ya Afya na Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na michakato mingi, lakini sisi pamoja na hawa wadau tumekaa, tumeweza ku-*stream line* na baada ya hapo tumeboresha zaidi kupunguza urasimu ili fedha hizo zifanye kazi kwa wakati na kuwanufaisha wananchi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nikuondoe shaka, tutahakikisha jambo hilo linafanyika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuongeza wanufaika ni kweli baada ya programu hii kukamilika mwitikio umekuwa mkubwa na kila mahali watu wanataka kunufaika na mpango huu wa *TASAF*. Nakuhakikishia kwamba, baada ya awamu hii ya pili kukamilika, mwezi Septemba

mwaka huu tunakuja na awamu ya tatu, na awamu hii Serikali imejipanga vizuri kuhakikisha wanufaika wanakuwa wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, tulipokuwa tunahamasisha sensa, tulikuwa tunawahakikishia wananchi kwamba kati ya matumizi ya takwimu zile, ni kutathmini upya zile orodha za watu wanaonufaika na *TASAF,* na kulikuwa na maswali mahsusi kuhusiana na hali ya umaskini kwenye kaya.

Mheshimiwa Spika, nataka nimwulize Mheshimiwa Waziri, je, ni lini sasa watatumia zile takwimu ili kuhakikisha kwamba kaya kadhaa za wananchi wa Vunjo ambazo wanaendelea kulalamika wanapata haki yao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Kimei, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika utekelezaji wa awamu ya pili ya *TASAF* kulikuwa na changamoto na malalamiko mengi. Baada ya kutambua hilo, ili kuboresha zaidi, Ofisi ya Rais, Utumishi tukishirikiana na taasisi nyingine kama Wizara ya Fedha kupitia Ofisi ya Takwimu, tumekaa pamoja na tayari tumefanya tathmini.

Mheshimiwa Spika, katika mpango mwingine, kwa maana ya awamu ya tatu ya *TASAF* itakayoanza baada ya Septemba, 2025, tutahakikisha tunatumia hizi taarifa ambazo tunashirikiana na Ofisi ya Takwimu kuhakikisha kwamba yale manung'uniko na lawama zote tunazimaliza kwa kuhakikisha wale walengwa sahihi wananufaika na mfuko huu, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 45

**Mamlaka ya Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma**

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaunda Mamlaka ya Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma ili kuimarisha usimamizi wa uwekezaji ndani ya Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, uundwaji wa Mamlaka ya Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma unasubiri kupitishwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Uwekezaji wa Umma, ambapo Muswada wa sheria hiyo, umesomwa kwa mara ya kwanza mwezi Novemba, 2023 na kuelekezwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma *(PIC)* kwa ajili ya uchambuzi. Mara baada ya Kamati kukamilisha kazi hiyo, Muswada huo utaletwa hapa Bungeni kwa ajili ya hatua nyingine zinazofuata za utungwaji wa sheria.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Tunatambua kwamba kuna Watanzania ambao wanaishi nchi za nje kama *diaspora*. Sasa ni nini

mkakati wa Serikali wa kuweka *incentive* kwa ajili ya kuwavutia Watanzania ili waje kuwekeza Tanzania?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, *EPZA* wamechukua eneo la zaidi ya ekari 3,000 kwa ajili ya uwekezaji. Sasa, ni nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba lile eneo ambalo wamelitenga Manyoni linatumika kwa ajili ya uwekezaji? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu, sasa tunakwenda kwenye marekebisho ya sheria kuweza kuwatambua *diaspora* kuwa na uraia maalum hapa nchini. Pia tunatambua kabisa kwamba uvutiaji wa wawekezaji kupitia Kituo cha Uwekezaji cha *TIC* tunawakaribisha hawa wawekezaji kutoka nje na tunawapa *incentive* pale wanapokuwa wanakuja na mtaji unaozidi zaidi ya Dola 200,000. Kwa Watanzania, tunawapa *incentive* pale wanapokuwa wamewekeza mtaji wa zaidi ya Dola 50,000.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa raia, hawa wa *diaspora* tutaangalia namna ya kuwavutia na wao wawe na punguzo kidogo ambalo litawafanya waweze kuvutiwa zaidi kuja kuwekeza hapa nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la pili, ni kweli *EPZA* imechukua maeneo ya Manyoni zaidi ya ekari 3,000 na imechukua maeneo haya maalum kwa ajili ya uwekezaji. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, mikakati bado inaendelea na wananchi wa maeneo hayo waliochukuliwa maeneo yao watalipwa na uwekezaji utaendelea katika eneo hilo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene, sasa aulize swali lake.

Na. 46

**Vijiji vya Bukene na Itobo Kuunganishiwa Umeme kwa shilingi 27,000**

**MHE. SELEMANI J. ZEDI** aliuliza: -

Je, lini vijiji vya Bukene na Itobo vitaunganishiwa umeme kwa gharama ya shilingi 27,000 kama vijiji vingine?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Judith Kapinga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali halisi ilivyo nchini, kuna maeneo ya vijiji na vijiji miji. Serikali inaendelea kuwahakikishia wananchi kwamba maeneo yote ya vijiji yataendelea kuunganishwa umeme kwa gharama ya shilingi 27,000. Maeneo ya Bukene na Itobo ni vijiji miji, hivyo, gharama ya kuunganisha umeme ni shilingi 320,960. Serikali inaendelea kuangalia kama kuna uwezekano wa kufanya maboresho kutokana na tathmini iliyofanyika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Selemani Zedi, swali la nyongeza.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Kama Kijiji cha Bukene ni kijiji mji, inakuwaje kwamba katika kijiji hicho hicho cha Bukene ambacho kina transfoma nne ukijiunganisha kwenye transfoma moja, unatozwa

shilingi 27,000, lakini ukijiunganisha kwenye transfoma nyingine ni shilingi 320,000 wakati ni kijiji kimoja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Itobo ambayo pia imesemwa ni kijiji mji ina vitongoji vinne au vitano, lakini kitongoji kingine kinatozwa shilingi 27,000 na kitongoji kingine kinatozwa shilingi 320,000/= wakati vitongoji vyote vinaunda kijiji kimoja. Kwa hiyo, hii inaleta mkanganyiko kwa wananchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge. Tayari nimemwelekeza Meneja wa Nzega na Meneja wa Mkoa wa Tabora wafike katika maeneo ya Bukene na Itobo, wafanye tathmini ili tuweze kupata majibu ya kina ili kuweza kuondoa mkanganyiko huo. Kwa hiyo, narudia tena kumwelekeza Meneja wa Wilaya ya Nzega na Tabora wafanye tathmini hiyo kwa Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kutatua suala hili ambalo limejitokeza, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Halmashauri ya Mji wa Ifakara bado ina maeneo ya vijiji kama vile Katindiuka, je, ni lini ombi letu kwa wananchi wa Katindiuka kuunganishiwa umeme kwa shilingi 27,000 litafanyiwa kazi? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo yanaunganishwa kwa shilingi 27,000 ni maeneo ya vijiji na shilingi 27,000 ni kutokana na *nature* ya miradi yenyewe ambayo Serikali inaweka fedha, na pia kuna fedha za wafadhili katika kutekeleza miradi hiyo. Kwa hiyo, siyo kila eneo linakidhi vigezo hivyo vya shilingi 27,000. Maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyasema hapa ya vijiji A na B yanapata tathmini ya mitaa. Kwa hiyo, tutaendelea kuangalia kwa kina kama yanakidhi vigezo vya shilingi 27,000 na kama

hayakidhi, basi gharama yake ya kuunganisha ni shilingi 320,960/=, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Theonest, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nataka kujua ni lini vijiji vilivyosalia Kyerwa vitapatiwa umeme ikiwepo Kijiji cha Bugaza ambacho kipo Kata ya Kimuli, na pia Kijiji cha Nyarugongo kilichopo Businde?

Mheshimiwa Spika, nasema haya kwa sababu *extension*…

**SPIKA:** Umeshauliza swali.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwa maeneo ya Kyerwa umeme umeshafika katika makao makuu ya vijiji. Tutaendelea kuangalia kama mkandarasi hajamaliza zile kilometa mbili za ziada. Kwa hiyo, nitafuatilia kwa vijiji hivi viwili, lakini kwa taarifa ambayo tunayo katika makao makuu ya Kijiji, umeme umeshafika. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Je, ni lini Serikali itakamilisha kwa haraka mradi wa ujazilizi katika Wilaya ya Karatu ambao unasuasua?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, Mkandarasi wa mradi wa ujazilizi yupo *site*, tutamfuatilia na tutaendelea kumsimamia kwa weledi ili kuhakikisha anakamilisha mradi huo kulingana na muda ambao umewekwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 47

**Adhabu Kubwa Zaidi kwa Wanaokutwa na Hatia ya Unyanyasaji**

**MHE. ROSE C. TWEVE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaweka adhabu kubwa zaidi kwa wanaokutwa na hatia ya unyanyasaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa niaba ya Wizara ya Katiba na Sheria.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, makosa mengi ya unyanyasaji yamebainishwa katika Sehemu ya 15 ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16, ambapo kuna makosa ya kubaka, kulawiti, kuzini na maalimu, shambulio la aibu, kunajisi punguani na kadhalika ambayo yana adhabu tofauti kulingana na aina na ukubwa wa kosa. Adhabu ya juu kwa makosa ya aina hii ni kifungo cha maisha jela na adhabu ya chini kabisa katika makosa haya ni kifungo cha miaka mitano kwa kosa la shambulio la aibu.

Mheshimiwa Spika, adhabu hizi zimewekwa kwa kuzingatia uzito wa kosa lililotendwa, hivyo Serikali bado inaamini adhabu hizo zinajitosheleza kuwa fundisho kwa wakosaji wa makosa haya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rose Tweve, swali la nyongeza.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami, pamoja na kuwa na hizo adhabu ambazo zimeainishwa na jitihada kubwa ambazo zimefanywa, bado changamoto ya unyanyasaji hasa kwa watoto ni kubwa. Hii siyo mara ya kwanza kuuliza swali hapa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge tukaonesha upungufu ambao upo katika sheria mbalimbali na Serikali ikafanya *commitment* kuwa itafanya utafiti na kutuletea baadhi ya sheria ambazo wanaona zina upungufu ili tuweze kuweka adhabu kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya upungufu ambao tulionyesha ni kuwa mtoto wa miaka 18 anaweza kubaka mpaka mara tatu ndiyo apate hiyo adhabu kubwa. Adhabu ya kwanza, anapata tu viboko, akibaka mara ya pili, ni miezi 12 na viboko. Sasa nilitaka kujua, ule utafiti Serikali mliosema mtaufanya umefikia wapi? Nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa swali moja la nyongeza linalohusu tumefikia wapi katika tafiti?

Mheshimiwa Spika, suala la tafiti ni jambo pana kidogo na linahitaji muda wa kutosha. Tunaendelea na utafiti kupitia taasisi yetu ya *Law Reforms* ambao wanaendelea kupitia mambo mbalimbali ikiwepo maoni na mapendekezo mbalimbali ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kwa sasa, muda wowote wanaweza wakakamilisha tafiti zao na watatupa majibu ambayo tutayafikisha kwako, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma.

Na. 48

**Mradi wa Maji Isale – Nkasi**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA K.n.y. MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itamaliza Mradi wa Maji Isale Wilayani Nkasi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Eng*. Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa maji Isale unaolenga kunufaisha vijiji sita vya Isale, Msilihofu, Ntuchi, Ifundwa, Kitosi na Nkata. Kazi zinazotekelezwa katika mradi huo ni pamoja na ujenzi wa chanzo cha maji *(intake),* ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 70.22, ujenzi wa matanki sita yenye jumla ya ujazo wa lita 420,000 na ujenzi wa vituo 75 vya kuchotea maji. Utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa 78% na umeanza kutoa huduma ya maji kwenye vijiji viwili vya Nkata na Kitosi. Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2025 na kunufaisha wananchi 20,113 wa vijiji hivyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Licha ya majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Miradi mingi ya maji inachukua muda mrefu kukamilika kwa sababu wakandarasi wanachukua muda mrefu kulipwa. Je, kuna mkakati gani wa kulipa hawa wakandarasi kwa wakati ili miradi ikamilike kwa wakati? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni lini mradi wa maji Bwawa la Mindu, Manispaa ya Morogoro utakamilika ili wananchi wa Manispaa ya Morogoro wapate maji ya kutosha na ya uhakika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Serikali ina mkakati wa kuhakikisha kwamba wakandarasi wote wanaotekeleza miradi ya maji wanalipwa kwa wakati ikiambatana na wao kuwasilisha hati za madai ambazo zinaendana na kazi ambayo wanakuwa wameifanya. Kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, tunaendelea kuangalia namna bora zaidi ya kuharakisha malipo kwa wakandarasi hao.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Bwawa la Mindu, tupo ndani ya mkataba na mkandarasi anaendelea na utekelezaji wa mradi huo. Lengo ni kwamba mradi ukamilike kwa wakati na wananchi wa Morogoro wapate huduma ya maji safi na salama, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Fiyao, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, nataka kujua, ni lini Serikali itapeleka fedha ili kukamilisha mradi wa maji Itumba – Isongole, kwa sababu mradi huu ni wa muda mrefu na wananchi wanakosa maji, kwani mabomba waliyoyaweka yanaendelea kupasuka kwa sababu ya kupigwa na jua?

Mheshimiwa Spika, ni lini mtapeleka fedha ili mradi huu uweze kukamilika na wananchi wanufaike na maji? Nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba miradi yote ya maji inapelekewa fedha. Vilevile tunapeleka fedha kulingana na hati ambazo wakandarasi wameleta. Tumekuwa tukikutana na baadhi ya changamoto, wakandarasi hawatekelezi kwa wakati, lakini tumekuwa tukichukua hatua kukatisha mikataba na wakandarasi wazembe.

Mheshimiwa Spika, lengo ni kwamba tuweze kuleta mkandarasi ambaye ataendana na *speed* ambayo sisi tunahitaji ya kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwa eneo la Songwe tutatoa kipaumbele kuhakikisha kwamba mkandarasi huyo anatekeleza mradi huo na ukamilike kwa wakati, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamisi Taletale, swali la nyongeza.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, je, ni lini Serikali itakamilisha mradi wa Kata ya Mkambarani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, mradi ambao Mheshimiwa Hamisi Taletale ameutaja ni kwamba tulikuwa na changamoto kidogo, mkandarasi akawa hayupo *site* na baadaye Serikali tumekaa mezani, tunaendelea na maongezi naye ili kuhakikisha kwamba anarejea *site* ili aweze kuendelea na mradi huo kwa sababu unalenga kuhudumia watu wengi ambao wana changamoto ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, jambo lake kwa sababu tayari ameshafika ofisini kwetu, tumeshaongea na liko katika hatua nzuri. Tunaamini kwamba litakamilika hivi karibuni. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, ni lini mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Wilaya ya Tarime na Rorya utakamilika ili kuweza kuondoa changamoto za maji kwa wananchi wale? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni ndoto ya Waheshimiwa Wabunge wanaotoka Mkoa wa Mara akiwemo Mheshimiwa Esther Matiko na hakika ameendelea kulisemea sana mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie kwamba miradi ambayo ipo katika mpango wa utekelezaji wa majukumu ya Serikali, tutahakikisha inakamilika kwa wakati kulingana na muda wa mkataba ambao tumesaini na wakandarasi, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Mjika, swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini mradi wa Ziwa Victoria utakamilika katika Mkoa wa Simiyu? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mradi wa kutoka Ziwa Victoria – Nyashimo – Bariadi – Itilima ambao una *phase* mbili, *phase* ya kwanza ikiwa inahusisha Wilaya tatu na *phase* ya pili ikiwa inahusisha Maswa pamoja na Meatu. Kwa *phase* ya kwanza umeshaanza na uko zaidi ya 25% lakini kwa awamu ya pili ambayo inahusisha Maswa pamoja na Meatu tayari tumeshatangaza tenda ya kumpata mkandarasi ambaye ataenda kutekeleza mradi huo.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi huu upo katika hatua nzuri na tunaenda vizuri kulingana na makubaliano yaliyoko kwenye mkataba. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, swali la msingi limezungumza kuhusu Kata ya Isale ipo Jimbo la Nkansi Kaskazini. Mradi huu una zaidi ya miaka 12. Naomba kufahamu, nini kimesababisha mpaka sasa ndiyo mradi umefikia 78%, na ni lini utakamilika? Nakushukuru.

**SPIKA:** Sasa hapo umeuliza maswali mawili, chagua moja. Chagua moja kati ya hayo mawili.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, ni lini mradi huu ambao umechukua zaidi ya miaka 12 utakamilika?

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, natambua na Serikali inatambua changamoto ya mradi huu ambapo Mkandarasi *Fally Enterprises* mwaka 2017 alipatiwa mkataba wa kutekeleza, lakini kwa sababu ambazo zilikuwa nje ya uwezo wake, alisuasua sana na Serikali tukachukua hatua ya kusitisha mkataba. Baada ya kusitisha mkataba huo tukapata kampuni nyingine inaitwa *Vibe International* ambayo tuliingia mkataba na Serikali mwaka 2022. Sasa hivi, kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi, mradi huu unatarajiwa kukamilika Juni, 2025. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, Mji wa Kinesi wenye *population* zaidi ya watu 10,000 hauna maji kwa zaidi ya miezi mitatu kwa sababu ya uharibifu wa pampu. Nini kauli ya Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan haiwezi kuvumilia pale ambapo tuna uwezo wa kuchukua hatua na Watendaji wasichukue hatua. Napenda kutumia fursa hii kumwelekeza *RM* Mkoa wa Mara kwenda katika eneo ambalo Mheshimiwa Jafari Chege amelizungumzia ili wakaangalie tatizo lilivyo na waweze kuchukua hatua ya kutatua changamoto hiyo na wananchi wa eneo hilo waanze kupata huduma ya maji safi na salama. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, Mbunge wa Arumeru Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 49

**Kukamilisha Miradi ya Maji Kata ya Jimbo la Arumeru Magharibi**

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha mradi wa maji wa Kata ya Kimnyaki, Tarakwa, Kiranyi na Siwandeti ambayo ni ahadi ya Waziri wa Maji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Kata ya Kimnyaki, Tarakwa, Kiranyi na Siwandeti Wilayani Arumeru. Kazi zinazofanyika katika mradi huo ni ujenzi wa tanki la kukusanyia maji *(sump well)* lenye ujazo wa lita 50,000, ununuzi na ufungaji wa pampu mbili zenye uwezo wa kuzalisha maji lita 1,560,000 kwa siku, ulazaji wa mabomba ya usambazaji umbali wa kilometa 67, pamoja na ujenzi wa vituo 70 vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi umefikia wastani wa 80% na umeanza kutoa huduma katika maeneo ya Olmringaringa na Kimnyaki kupitia vituo 13 vilivyojengwa. Mradi unatarajiwa kukamilika

mwezi Juni, 2025 na utanufaisha wananchi wapatao 57,541 waishio maeneo hayo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali na jitihada zilizofanyika kwa kiwango hicho. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa wananchi hawa wa Vitongoji hivyo vya Siwandeti, Kiranyi, Tarakwa na Kimnyaki wanateseka sana kwa ukosefu wa maji kutokana na wingi wao: -

(a) Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuharakisha mradi huu ili uweze kukamilika haraka na mapema zaidi?

(b) Je, pia ni lini Serikali itasambazia wananchi wa Kata ya Mlangarini, Kijiji cha Kiserian, Vitongoji vya Olmaroroi na Muungano ambapo bomba kubwa limepita katikati yao ili waweze kupata maji ili waweze kuondokana na adha ya ukosefu wa maji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi, mradi huu umefikia 80% na tunatarajia utakamilika mwezi Juni.

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida, mradi huu unaweza ukakamilika ndani ya miezi mitatu, lakini kuna kipengele cha *testing and commissioning* ambacho kitahitaji kama miezi mitatu tena. Kwa hiyo, tunaamini kwamba, mpaka ifikapo Juni, wananchi wa maeneo hayo ambapo Mheshimiwa Mbunge amekuwa akiwapambania sana, basi watapata huduma hiyo ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, kwa kipengele cha pili, katika Vitongoji vya Muungano na vingine hivyo ambavyo vimepitiwa na bomba kuu, kwa sera yetu ni kwamba, vijiji na vitongoji vinavyopitiwa na bomba kuu kilometa 12.5 kulia na kushoto ni lazima wapate huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anatambua kwamba juzi alikuwepo katika vitongoji vile na sisi kama Wizara tulipokea changamoto ya wananchi waliyoiwasilisha kwa Mheshimiwa Mbunge. Sisi tuliichukua na kutolea maelekezo na kuwaelekeza Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Arusha ili wahakikishe kwamba wanaharakisha usambazaji wa maji kwa wananchi wa vitongoji hivyo ili waweze kunufaika na huduma ya maji safi na salama. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itakamilisha mradi na usambazaji wa maji katika Mji wa Mererani unaotekelezwa na Mamlaka ya Mji Arusha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya maji ni maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan; na miongozo ya Mheshimiwa Waziri wetu ni kuhakikisha kwamba miradi hii inapokuwa inapata fedha bila kuwa na mkwamo wowote, basi ikamilike kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kuwaelekeza Mamlaka ya Maji Arusha kuhakikisha kwamba Mradi wa Maji Mererani ukasimamiwe kwa ukamilifu, ukamilike kwa wakati na uwe una ubora unaotakiwa na wananchi wapate maji safi na salama yenye gharama inayokubalika. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Mtenga, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mtwara Mjini ni jimbo ambalo tunakunywa maji ambayo ni ya visima na visima hivyo vimechimbwa miaka takribani 60 iliyopita. Kwa sasa tuna hali ngumu, baada ya muda, inawezekana maji yakapotea. Je, ni lini

Serikali itatuwezesha fedha za kuchimba visima vingine virefu ili maji yaendelee kupatikana kwenye Jimbo la Mtwara Mjini? Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, tunapata maji kwa njia mbili, *surface water* na *underground water*. Changamoto ya *underground water* ni kwamba hata kama tutaendelea kuchimba visima vingi, bado changamoto ya visima vingine kuendelea kukauka ni kubwa. Ndiyo maana tunachimba visima kwa ajili ya dharura na kutatua changamoto kwa muda mfupi na muda wa kati huku tukiwa tunaendelea kusanifu miradi mikubwa ambayo itakuwa suluhisho ambalo litasaidia wananchi kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, katika Mji wa Mtwara na Mtwara yenyewe, tunaendelea na miradi ile mikubwa ambayo ninaamini kwamba hiyo ndiyo itakuwa *solution* kubwa kwa ajili ya wananchi wa Mtwara kupata huduma ya maji safi na salama na ikiwa endelevu. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Pathan, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, ni lini Serikali itaanzisha mradi mkubwa wa maji kutoka Bwawa la Mwalimu Nyerere kuelekea Mkoa wa Lindi na Mtwara likawa suluhisho la kudumu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, katika vyanzo ambavyo ni vya uhakika vya maji ni Bwawa la Mwalimu Nyerere. Bwawa hilo litakuwa na uwezo wa uzalishaji wa maji wa lita nyingi zaidi kuliko bwawa lolote. Sisi Wizara ya Maji tayari tumeshaelekeza wataalamu wetu wafanye tathmini na kuangalia namna gani tutaweza kuingia kwenye kutafuta mtaalamu mshauri ili tuweze kutangaza tenda na kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi huo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, Mbunge wa Ngara, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Charles Mwijage.

Na. 50

**Forodha za Murusagamba na Kabanga Kufanya Kazi Saa 24**

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE K.n.y. MHE. NDAISABA G. RUHORO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwezesha Vituo vya Forodha vya Murusagamba na Kabanga kufanya kazi saa 24?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Forodha cha Kabanga ni kituo cha pamoja cha kutoa huduma za forodha baina ya Tanzania na Burundi. Kituo hicho kina miundombinu wezeshi kama vile taa za ulinzi, vyombo vya ulinzi na usalama, na maeneo ya kukagulia bidhaa, wasafiri na wafanyakazi, hivyo kuwa na uwezo wa kufanya kazi saa 24 kwa upande wa Tanzania. Hata hivyo, ili kituo hicho kiweze kutoa huduma saa 24, upande wa Kobero nchini Burundi unapaswa pia kuwa tayari kutoa huduma hiyo saa 24.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Kituo cha *OSBP* Kobero kwa upande wa Burundi kinatoa huduma kwa masaa 12 tu. Aidha, jitihada mbalimbali zinaendelea kufanyika ili kuwezesha mazingira ya kituo cha *OSBP* Kobero kufanya kazi kwa saa 24, hususan ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Murusagamba ni kituo kidogo cha uzuiaji cha forodha *(preventive office)*, vituo hivi hufanya kazi ya kuzuia magendo kwenye maeneo ambayo mwenendo wa bidhaa na watu ni mdogo. Kutokana na udogo wa mwenendo wa bidhaa na watu katika Kituo cha Murusagamba, uwezekano wa kutoa huduma kwa saa 24 haupo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Mwijage, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa maelezo ya Serikali kuhusu Kituo cha Murusagamba. Pamoja na jitihada hizo za Serikali, je, Serikali ina mpango gani wa kuweka *cargo scanner* upande wa Mutukula ili mizigo iweze kupita kwa kasi kwenda Afrika ya Kaskazini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Mwijage kwa ufuatiliaji wa karibu wa suala hili. Ninayo furaha kumwambia Mheshimiwa Mwijage kwamba tayari mkandarasi yuko kwa ajili ya *site* kufunga mdaki huo mkubwa ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza ushuru wa forodha kwa magari yanayoingizwa kwa ajili ya huduma za afya na elimu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka miongozo, taratibu, kanuni na sheria mbalimbali ambazo ninaamini Mheshimiwa Mbunge naye anazijua kwa kusamehe kodi kwa magari hayo ya afya na mengineyo

ambayo uthibitisho umepatikana kutokana na Wizara ambazo zinastahiki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Said Issa, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Forodha cha Malindi – Zanzibar kinahudumia zaidi ya kontena 2000 kwa mwezi lakini kinafanya kazi kwa saa 12 tu, je, ni lini kitafanya kazi kwa masaa 24 ili kuongeza ufanisi? Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyogeza la Mheshimiwa Mohamed, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwa sasa kituo chetu kile kinafanya kazi saa 12 tu, lakini tayari tumeshakaa na wenzetu upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yaani Zanzibar. Mazungumzo yanaendelea, basi tukifikia mwafaka wa jambo hilo, tutatoa huduma kwa saa 24.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Mtinga, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Horohoro kule Tanga hakina *scanner,* na hii inasababisha usumbufu mkubwa. Ni lini kitafungwa *scanner*, jambo ambalo ni muhimu kwa mapato ya nchi yetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge. Ni kweli anachokisema, na tayari Serikali kupitia *TRA* tumetenga bajeti kwa ajili ya ununuzi wa midaki mbalimbali. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba midaki itakayokuja ndani ya mwaka huu wa fedha, basi tutaingalia sehemu ya Horohoro na yenyewe, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha Maswali kutoka kwenu na Majibu kutoka upande wa Serikali. Nitaleta tangazo la wageni nililonalo hapa mbele.

Tutaanza na wageni waliokaa Jukwaa la Spika. Kwanza ni mgeni mmoja wa Mheshimiwa Naibu Spika ambaye ni Ndugu Mohamed Yakub – Naibu Meya Mstaafu wa Ilala na Mwenyekiti wa *Tanzania Salama Foundation*, karibu sana. *(Makofi)*

Pia wapo wageni saba wa Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, Waziri wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, hawa ni Ndugu Methusela Ntonda, Naibu Katibu Mkuu, karibu sana; Ndugu Stephen Kagaigai, Mwenyekiti wa Bodi, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Dkt. Ayoub Rioba Chacha, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Utangazaji *(TBC)*, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Abel Philip, Mkurugenzi wa Sera na Mipango, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Lugano Rwetaka, Mkurugenzi wa Kitengo cha Huduma za Sheria, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Gwakisa Mlawa, Mkurungenzi wa Sheria Shirika la Utangazaji *(TBC)*, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni 11 wa Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, hawa ni Wenyeviti na Makatibu wa Chama cha Mapinduzi kutoka wilaya zote za Mkoani Mbeya, karibuni sana viongozi wetu. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa Maryprisca Mahundi anao wageni wengine 20 ambao hawa ni Makatibu Wenezi na Sekretarieti ya Chama Cha Mapinduzi pamoja na familia yake kutoka Mkoani Mbeya ambao wamekaa nje ya Jukwaa la Spika, karibuni sana viongozi wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge mbalimbali. Kwanza ni wageni 11 wa Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Hawa ni Wadau, Watendaji na Maafisa wa Wizara hiyo. Wote wasimame kwa pamoja. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Hamisi Mwinjuma, Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Hawa ni wadau wa mpira wa miguu kutoka Jijini Dar es Salaam. Haya, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Stephen Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini ambao ni wapigakura wake kutoka Longido Mkoani Arusha. Haya, pengine hawajapata nafasi.

Wageni wawili wa Mheshimiwa Fatma Toufiq, hawa ni watoto wa dada yake wanatoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi 24 na walimu watano wa Shule Msingi ya *Al-Irishaad International* ya Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao viongozi 58 wa UVCCM Tawi la Chuo Kikuu cha Kiislamu cha Morogoro. Karibuni sana Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio wageni tulionao Bungeni. Wengine watakaokuja baada ya hawa, tutawatangaza. Tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania wa Mwaka 2024**

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada huu unakuja kwetu kwa mara ya pili. Sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, aje awasilishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahim kwa ruzuku ya uhai na kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Muswada huu wa Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)* wa mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nitumie nafasi hii kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambayo aliunda upya tarehe 08 Desemba, 2024. Wizara hii ina dhima ya kulinda mtima wa Taifa letu na kujenga taswira ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, aidha, nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake makini na mahiri wa kizalendo ambao katika miaka minne na nusu ya uongozi wake, nchi yetu imepata maendeleo makubwa sana yaliyotia fora duniani ikiwa ni pamoja na Sekta ya Habari na Utangazaji.

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitapongeza mambo makubwa yaliyojiri hivi karibuni ya Kitaifa. Kwa ruhusa yako nitumie nafasi hii kupongeza na kuunga mkono Azimio la Mkutano Mkuu Maalum wa Chama cha Mapinduzi la kumthibitisha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Mgombea wa nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa nafasi hiyo katika Uchaguzi Mkuu ujao. Pia, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, naye kwa kuthibitishwa kuwa Mgombea nafasi ya Urais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi la Zanzibar kupitia Chama cha Mapinduzi. Wote nawatakia kila lililo jema kwa maslahi mapana ya nchi yetu iliyojengwa katika misingi ya Chama cha *TANU* na baadaye Chama cha Mapinduzi ya Waasisi wa Taifa hili, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije katika suala la Muswada wa leo. Historia ya utangazaji nchini, ina uhusiano wa moja kwa moja na *TBC* kwa kuangalia historia ya Shirika kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, *TBC* ilianza kama Sauti ya Dar es Salaam mwaka 1951 kikiwa ni Kituo cha Utangazaji cha Serikali ya kikoloni. Ikawa Taasisi ya Utangazaji Tanganyika *(Tanganyika Broadcasting Services (TBS)*1955) ikiwa Idara ya Serikali. Ikaja kuwa Shirika la Utangazaji Tanganyika *(Tanganyika Broadcasting Corporation (TBC))* kupitia Sheria ya *Tanganyika Broadcasting Corporation Ordinance Cap*. 370. Ikaja kuwa *Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD)* mwaka1965 ikiwa Idara ya Serikali iliyoanzishwa baada ya *TBC* kufutwa kupitia Sheria ya Tanganyika *Broadcasting Corporation (Dissolution) Act No*. 11 ya 1965.

Mheshimiwa Spika, baadaye ikawa Taasisi ya Utangazaji Tanzania *(TUT)* 2002, Shirika baada ya kuunganisha *RTD* na *TvT* iliyoanzishwa mwaka 2000; na mwaka 2007 ikawa Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)* lililoanzishwa kwa amri ya Rais.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko mbalimbali...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri subiri kidogo.

Waheshimiwa tupunguze sauti kidogo. Tunaongea mambo ya muhimu sana, lakini tupunguze sauti. Kama ni lazima kuzungumza kwa sauti ya juu sana, basi milango iko mingi kabisa unaweza kutokea mlango ambao upo karibu na wewe ili Wabunge wengine waendelee kusikiliza hoja ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Waziri, endelea.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, *TBC* ni chombo cha utangazaji kinachotoa huduma kwa umma tofauti na vyombo vingine vya utangazaji, hususan vile binafsi, ambavyo kimsingi vinaendeshwa kibiashara zaidi. *TBC* ni chombo kinachotakiwa kulinda maslahi ya Taifa na umma, hivyo uwepo wa chombo hiki ni muhimu kwa maendeleo, amani, utulivu na utengamano wa nchi.

Mheshimiwa Spika, *TBC,* kama chombo cha Utangazaji cha Umma, ni nyenzo ya Serikali katika masuala ya ulinzi na usalama wa nchi inapotekeleza majukumu yake kwa Taifa. Hivyo, *TBC* haina budi pamoja na mambo mengine kujikita katika haya yafuatayo: -

(i) Kukuza umoja, utaifa, usalama, amani, utulivu na ustawi wa Nchi;

(ii) Kutangaza matukio yote ya kitaifa na kimataifa yenye umuhimu kwa maslahi ya Taifa;

(iii) Kuwa tayari muda wote kutangaza taarifa za Serikali kuhusu dharura yoyote inayojitokeza;

(iv) Kutangaza na kuhifadhi kumbukumbu za matukio yote yanayohusu Viongozi Wakuu wa kitaifa;

(v) Kuandaa vipindi mahususi kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu za matukio na masuala mbalimbali muhimu kwa Taifa;

(vi) Kuandaa, kutangaza na kuhifadhi vipindi vinavyoelezea masuala ya maendeleo, uzalendo, amani, utulivu, mila, desturi na utamaduni wa Mtanzania;

(vii) Kuwekeza kwenye miundombinu ya utangazaji ili kuhakikisha inafika maeneo yote na kumfikia kila mwananchi;

(viii) Kuandaa na kurusha maudhui yanayomgusa kila mwanajamii bila kujali mvuto wa kibiashara,

(ix) Kuwa daraja kati ya Serikali na wananchi wake. Kwa hali hiyo, inahakikisha kwamba mipango na programu za Serikali na utekelezaji wake zinawafikia wananchi na wakati huo huo kufichua changamoto zinazowakabili wananchi kwa ajili ya kutatuliwa na Serikali;

(x) Kuchochea ukuaji wa uchumi na uchumi bunifu kwa maendeleo ya Taifa; na

(xi) Kulinda taswira ya nchi na kusimamia maslahi ya Taifa.

Mhshimiwa Spika, tofauti na *TBC,* kampuni za utangazaji za kibiashara huandaa vipindi vyenye mvuto kibiashara kwa kuwa uhai na uendeshaji wa kampuni hizo, hautegemea faida itokanayo na matangazo.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji utakaoiwezesha *TBC* kutimiza majukumu yake kwa ufanisi, unahitaji fedha za uhakika kwa ajili ya uendeshaji, matengenezo ya mitambo na vifaa ili kudumisha ubora wake, pamoja na ununuzi wa vipuri na/au mitambo mipya pale inapochakaa.

Mhshimiwa Spika, Muswada huu umegawanywa katika sehemu saba ambapo sehemu ya kwanza inaainisha masharti ya awali yakijumuisha jina la sheria, kuanza kutumika kwa sheria, matumizi na tafsiri ya baadhi ya maneno yaliyotumika ndani ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili inafafanua kuhusu kuendelea kutambulika kwa shirika, majukumu na mamlaka ya shirika na wajibu wa shirika katika kuandaa vipindi.

Mhshimjwa Spika, sehemu hii ya pili ya Muswada inaweka masharti kuhusu kuendelea kulitambua shirika, majukumu na mamlaka ya shirika, pamoja na masharti kuhusu wajibu wa shirika hili katika kutekeleza majukumu yake. Shirika litaandaa vipindi kama vile:-

(i) Vinavyochangja kukuza demokrasia, maendeleo ya jamii, usawa wa kijinsia, ujenzi wa Taifa, utoaji wa elimu na kuimarisha maadili ya jamii;

(ii) Vipindi vinavyolinda, kuimarisha na kudumisha uhuru, umoja na taswira ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(iii) Vipindi vinavyolinda na kuimarisha mfumo wa kiutamaduni, kisiasa, kijamii na kiuchumi wa Tanzania;

(iv) Vipindi vinavyoakisi mitazamo, maoni, mawazo, maadili na ubunifu wa sanaa za Kitanzania;

(v) Vipindi vinavyokuza vipaji vya Watanzania kupitia vipindi vya elimu na burudani;

(vi) Vipindi vinavyoweka anuai inayojitosheleza na inayotoa mizania ya habari, elimu na burudani ili kukidhi mahitaji ya utangazajj ya Watanzania wote;

(vii) Vipindi vinavyotoa maoni, taarifa, habari na uchambuzi wa masuala mbalimbali kwa mtazamo wa Kiafrika; na

(viii) Vipindi vinavyoendeleza na kulinda maslahi ya Taifa na usalama ndani na nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu kwa ujumla inahusu Bodi ya Shirika, sifa za kuwa mjumbe, majukumu na mamlaka ya Bodi, mamlaka ya ukasimishaji Mamlaka ya Bodi, ada au posho za Wajumbe wa Bodi, kinga kwa Wajumbe wa Bodi, Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu, majukumu ya Mkurugenzi Mkuu na watumishi wa shirika.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne inapendekeza usalama, usimamizi wa ulinzi wa miundombinu ya utangazaji, makatazo kuhusiana na uharibifu wa mali za shirika, kuingia kwenye eneo la shirika na matumizi ya maudhui.

Mheshimiwa Spika, *TBC* inamiliki maeneo 65 mahususi kwa shughuli za utangazaji. Aidha, yapo maeneo yaliyoainishwa na Umoja wa Mawasiliano Duniani *(International Telecommunication Union - ITU)* kuwa ni mahususi kwa ajili ya masafa mafupi *(short wave)* na ya kati *(Medium wave)* ya redio katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Mbeya, Kigoma, Lindi, Dodoma, Ruvuma na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maeneo yaliyoainishwa na *ITU, TBC* inamiliki maeneo mengine mahususi kwa shughuli nyingine za utangazaji ili kufikisha huduma ya utangazaji katika maeneo yote ya nchi na kimataifa kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano, Sura ya 172 na Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Sura ya 306.

Mheshimiwa Spika, maeneo haya ya *TBC* ni maeneo nyeti yanayolindwa chini ya Sheria ya Usalama wa Taifa, Sura ya 47 na Sheria ya Sehemu na Maeneo Yanayolindwa Sura ya 74.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa yale yanayotambuliwa na *ITU*, mabadiliko ya matumizi yana athari za moja kwa moja za mwingiliano wa masafa *(frequency)* na nchi jirani. Hivyo, tunaziomba mamlaka

zote zinazohusu umiliki wa ardhi kuyaacha maeneo hayo kwa sababu tayari yanatambuliwa kimataifa na tukifanya hivyo tutakuwa tunazua migogoro na nchi zinazotuzunguka.

Mheshimiwa Spika, mipango ya baadaye ya *TBC* ni kuwekeza katika mitambo midogo ya *FM* ili kuhakikisha maeneo yasiyofikiwa kutokana na sababu za kijiografia kufikiwa. Aidha, *TBC* itawekeza katika mitambo ya *Medium Wave* (masafa ya kati) ili kuweza kufikia maeneo mengi zaidi ya ndani ya nchi na nchi jirani pamoja na kufanya utafiti na kuwekeza katika mitambo ya *Short Wave* (masafa mafupi) ili kufikisha matangazo dunia nzima na hivyo kutimiza azma ya kufikisha Kiswahili na utamaduni wa Kiswahili pande zote duniani.

Mheshimiwa Spika, tulifanya hivyo wakati wa ukombozi wa Kusini mwa Afrika. Tulijenga mitambo kama hiyo ambayo ilikuwa inatangaza nchi zote za Afrika ya Kusini. Sasa tutaanza kutangaza dunia nzima ili kukuza Kiswahili na kufikisha utamaduni wa Kiswahili kwa dunia nzima.

Mheshimiwa Spika, Shirika la *Voice of Nigeria* la Nigeria pamoja na mashirika kama *BBC* ya Uingereza yanatumia mitambo ya *Short Wave* ili kufikisha matangazo yake duniani. Fauka ya hayo, *TBC* inatarajia kuwekeza katika uanzishwaji wa Chaneli ya *TV* mtandao kwa ajili ya matangazo ya nje *(external service)* pamoja na kuimarisha kitengo cha *TBC Online*, lengo likiwa kufikisha maudhui ya kitanzania sehemu mbalimbali duniani.

Mheshimiwa Spika, pia itawekeza katika kuboresha *studio* zake kuwa za kisasa kuendana na teknolojia mpya pamoja na kufanya ununuzi wa mitambo na vifaa vya kisasa vya ukusanyaji, uchakataji na usambazaji maudhui vinavyozingatia teknolojia ya kisasa. Uwekezaji huu unahitaji mtaji mkubwa wa kifedha kutoka Serikalini.

Mhshimiwa Spika, sehemu ya tano inaweka masharti ya katazo kwamba mtu asiyehusika na shirika haruhusiwi kuingilia mali za shirika au vifaa vya shirika.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya sita inaweka masharti ya fedha ambayo yanajumuisha vyanzo vya fedha vya shirika, usimamizi wa fedha, makadirio ya mapato na matumizi, matumizi ya fedha, hesabu na ukaguzi na taarifa ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya saba na ya mwisho inaaainisha vifungu vya jumla ikiwemo udhamini wa vipindi, matengenezo au mabadiliko yanayoweza kuharibu mfumo wa matangazo, uanzishwaji wa chaneli maalum, adhabu ya jumla na mamlaka ya Waziri kutengeneza kanuni.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Miundombinu ambapo Idara ya Habari ilikuwepo mpaka tarehe 8 Desemba, 2024 ambapo Mheshimiwa Rais ilimpendeza kuiunganisha na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na kuunda Wizara mpya ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuwa na Wajumbe wa Kamati hiyo ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi wa Muswada na wadau waliotoa maoni yao ambayo yamezingatiwa katika jedwali la marekebisho litakalowasilishwa leo katika mjadala huu.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MHESHIMIWA PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI (MB), WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO AKIWASILISHA MUSWADA WA SHERIA YA SHIRIKA LA UTANGAZAJI TANZANIA (TBC) WA MWAKA 2024 KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, neomba nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahimu kwa ruzuku ya uhai na kwa kuniwezesha kusimame mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha

Muswada huu wa Sheria ya Shirjka ja Utangazaji Tanzaniä (TBC) wa Mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nitumie nafasi hii kumshukuru kwa dhati Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzanie kwa kuniämini na kuniteua kuwa Waziri wa Habari% Utamaduni, Sanaa na Michezo ambayo ina dhima ya kulinda mtima wa taifa letu na taswira ya nchi yetu. Aidha nitumie fursa hii kumshukuru Msheshimiwa Rais kwa uongozi wake mäkini na mahiri wa kizalendo ambao katika miaka minne na nusu ya uongozi wake nchi yetu imepata maendeleo makubwa sana yaliyotia fora ikiwa ni pamoja na sekta ya Habari na Utangazeji.

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitapongeza mambo makubwa yaliyojiri hivi karibuni ya Kitaifa.

Kwa ruhusa yako nitumie nafasi hii kupongeza na kuunga mkono azimio la Mkutano Mkuu Maalumu wa Chama cha Mapinduzi la kumdhibitisha Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Mgombea wa nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi kuwa Mgombea Mwenza. Sambamba nao, nampongeza Mhe. Dkt. Hussein Mwinyi naye kwa kuthibitishwa kuwa Mgombea nafasi ya Urais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi. Wote nawatakia kila lililo jerna kwa maslahi ya nchi yetu.

**1.0 HISTORIA YA TBC**

Mheshimiwa Spika, Historia ya utangazaji nchini, ina uhusiano wa moja kwa moja na TBC kwa kuangalia historia ya Shirika kama ifuatavyo:

a) Sauti ya Dar es salaam - 1951 — Kituo cha Utangazaji cha Serikali;

b) Taasisi ya Utangazaji Tanganyika [Tanganyika Broadcasting Services (TBS)] -1955 — Idara ya Serikali;

c) Shirika la Utangazaji Tanganyika (Tanganyika Broadcasting Corporation (TBC) kupitia Sheria ya Tanganyika Broadcastjng Corporation Ordinance Cap. 370;

d) Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD) — 1965 — Idara ya Serikali iliyoanzishwa baada ya TBC kufutwa kupitia Sheria ya Tanganyika Broadcasting Corporation (Dissolution) Actr no. 11 ya 1965;

e) Taasisi ya Utangazaji Tanzania (TUT) - 2002 - Shirika baada ya kuunganisha RTD na TvT (iliyoanzishwa mwaka 2000); na

f) Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) —2007.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko mbalimbali ya chombo hiki yalisababishwa ne mabadiliko yaliyokuwa yakiendelea kwa nyakati tofauti kisiasa, kiuchumi na kijamii.

## 2.0. UMUHIMU WA TBC KWA NCHI UNAOITOFAUTISHA NA VYOMBO BINAFSI

Mheshimiwa Spika, TBC ni chombo cha utangazaji kinachotoa huduma kwa umma tofauti na vyombo vingine vya utangazaji, hususani vile binafsi, ambavyo kimsingi vinaendeshwa kibiashara zaidi.

TBC ni chombo kinachotakiwa kulinda maslahi ya taifa na umma hivyo: uwepo wa chombo hiki ni muhimu kwa maendeleo, amani, utulivu na utengamano wa nchi.

Mheshimiwa Spika, TBC, kama chombo chã Utangazaji cha Umma, ni nyenzo ya Serikali katika masuala ya ulinzi na usalama wa nchi inapotekeleza mejukumu yake kwa Taifa. Hivyo, TBC haina budi pamoja na mambo mengine kujikita katika haya yafuatayo:

a) Kukuza umoje, utaifa, usalama, amani, utulivu na ustawi wa Nchi;

b) Kutangaza matukio yote ya kitaifa na kimataifa yenye umuhimu kwa maslahj ya Taifa;

c) Kuwa tayari muda wote kutangaza taarifa za Serikali kuhusu dharura yoyote inayojitokeza;

d) Kutangaza na kuhifadhi kumbukumbu za matukio yote yanayohusu viongozi wakuu wa kitaifa;

e) Kuandaa vipindi mahsusi kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu za matukio na masuala mbalimbali muhimu kwa Taifa;

f) Kuandaa, kutangaza na kuhifadhi vipindi vinavyoelezea masuala ya maendeleo, uzalendo, amani, utulivu, mila, desturi na utamaduni wa mtanzania;

g) Kuwekeza miundombinu ya utangazaji kufikia maeneo yote na kumfikia kila mwananchi;

h) Kuandaa na kurusha maudhui yanayomgusa kila mwanajamii bila kujali rnvuto we kibiashara,

i) Kuwa daraja kati ya Serikali na wananchi wake. Kwa hali hiyo inahakikisha kwamba mipango na programu za Serikali na utekelezaji Wake, zinawafikia wananchi na wakati huo huo kufichua changamoto zinazowakabili wananchi kwa ajili ya kutatuiiwa na Serikali;

j) Kuchochea ukuaji wa uchumi na uchumi bunifu kwa maendeleo ya taifa; na

k) Kulinda taswira ya nchi na kusimamia maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, tofauti na TBC, kampuni za utangazaji za kibiashara huandaa vipindi vyenye mvuto kibiashara kwa kuwa uhai na uendeshaji wa kampuni hizo, hutegemea faida itokanayo na matangazo.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji utakaoiwezesha TBC kutimiza majukumu yake kwa ufanisi, unahitaji fedha za uhakika kwa ajili ya uendeshajiy matengenezo ya mitambo na vifaa ili kudumisha ubora Wake, pamoja na ununuzi wa vipuri na/au mitambo mipya pale inapochakaa.

**3.0. MUUNDO WA MSWADA**

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanywa katika Sehemu VII, ambapo:

Sehemu ya I inaainisha masharti ya awali yakijumuisha jina la Sheria; kuanza kutumika kwa Sheria, matumiz na tafsiri ya baadhi ya maneno yaliyotumika ndani ya muswada huu.

Sehemu ya II inafafanua kuhusu kuendelea kutambulika kwa Shirika, majukumu na mamlaka ya Shirika na wajibu wa Shirika katika kuandaa vipindi.

**WAJIBU WA SHIRIKA KATIKA KUANDAA VIPINDI**

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inaweka masharti kuhusu kuendelea kutitambua Shirika, majukumu na mamlaka ya Shirika pamoja ne masharti kuhusu wajibu wa Shirika iki Katika kutekeleza majukumu yake, Shirika litaandaa vipindi kama vile:-

a) vinavyochangja kukuza demokrasia, maendefeo ya jarnii, usawa wa kijinsia, ujenzj wa taifa, utoaji wa e/imu na kuimarisha maadili ya jarnü;

b) vinavyolinda, kuirnarisha na kudumjsha uhuru, umoja na taswira ya Jamhuri ya Muungano;

(c) vinavyofinda na kujmarjsha mfumo wa kjutarnaduni, kisiasa, kijamfi na kiuchumi;

c) vinavyoakisi mitazamo, maoni, mawazo, maadifi na ubunifu wa sanaa za Kitanzania,'

d) vinavyokuza vipaji vya Watanzania kupitia vipindi vya elimu na burudani;

e) vinavyoweke enuai jnayojjtoshelezä ne inayotoa mizania ya habari, elimu na burudanj jlj kukjdhi mahitaji ya utangazajj ya Watanzania wote;

f) vinavyotoa maonj, tearifa, habari na uohambuzi wa masuala mbalimbali kwa mtazamo wa Kiafrjka; na

g) vinavyoendeleza na kulinda maslahi ya taifa na usalama ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya III kwa ujumla inahusu Bodi ya Shirika, sifa za kuwa mjumbe, majukumu na mamlaka ya Bodi, mamlaka ya ukasimishaji Mamlaka ya Bodil ada au posho za wajumbe wa Bodi, kinga kwa wajumbe wa Bodi, Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu, majukumu ya Mkurugenzi Mkuu na watumishi wa Shirika.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya IV inapendekeza usalama, usimamizi wa ulinzi wa Miundombinu ya utangazaji, makatazo kuhusiana na uharibifu wa mali za Shirika, kuingia kwenye eneo la Shirika, na matumizi ya maudhui.

**MAENEO YA TBC YALIYOIDHINISHWA NA ITU MAHSUSI KWA SHUGHULI ZA UTANGAZAJI:**

Mheshimiwa Spika, TBC inamiliki maeneo 65 mahsusi kwe shughuli za utengazaji.

Aidha yapo maeneo yaliyoainishwa na Umoja wa Mawasiliano Duniani (International Telecommunication Union — ITIJ) kuwa ni mahsusi kwa ajili ya masafa mafupi na ya kati ya redio katika mikoa ya

Dar es Salaam, Arusha, Mbeya), Kigoma, Lindi, Dodoma, Ruvuma na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maeneo yaliyoainishwa na ITU, TBC inamiliki maeneo mengine mahsusi kwa shughuli nyingine za utangazaji ili kufikishe huduma ya utangazaji katika maeneo yote ya Nchi na kimataifa kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano, Sura 172 na Sheria ya Mawasiiiano ya Kielektroniki na Posta, Sura ya 306.

Maeneo haya ya TBC ni maeneo nyeti yanayolindwa chini ya Sheria ya Usalama wa Taifa, Sura 47 na Sheria ya Sehemu na Maeneo Yanayolindwa: Sura 74.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa yale yanayotambuliwa na ITU: mabadiliko ya matumizi yana athari za moja kwa moja za kuingiliano wa masafa (frequency) na nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, mipango ya baadaye ya TBC ni kuwekeza katika mitambo midogo ya FM ili kuhakikisha maeneo yasiyofikiwa kutokana na sababu za kijiografia kufikiwa. Aidha, TBC itawekeza katika mitambo ya MW ili kuweza kufikia maeneo mengi zaidi ya ndani ya nchi na nchi jirani pamoja na kufanya utafiti na kuwekeza katika mitambo ya SW ili kufikisha matangazo dunia nzima na hivyo kutimiza adhma ya kufikisha Kiswahili pande zote duniani.

Mheshimiwa Spika, Shirika la VON la Nigeria pamoja na mashirika kama BBC ya Uingereza yanatumia mitambo ya SW ili kufikisha matangazo yake duniani. Fauka ye hayo, TBC inatarajia kuwekeza katika uanzishwa wa Chaneli ya TV rntandao kwa ajili ya matangazo ya nje (external service) pamoja na kuimarisha kitengo cha TBC Online, lengo likiwa kufikisha maudhui ya kitanzania sehemu mbalimbali duniani.

Mheshimiwa Spika, pia itawekeza katika kuboresha studio zake kuwa za kisasa kuendana na teknolojia mpya pamoja na kufanya

ununuzi wa mitambo na vifaa vya kisasa vya ukusanyaji, uchakataji na usambazaji maudhui vinavyozingatia teknolojia ya kisasa. (Uwekezaji huu unahitajj uwekezaji mkubwa wa Serikali kifedha).

Mheshimiwa Spika, sehemu ya V inaweka masharti ya katazo kwamba mtu asiyehusika na Shirika haruhusiwi kuingilia mali za Shirika au vifaa vya Shirika.

Sehemu ya VI inaweka masharti ya fedha ambayo yanajumuisha: Vyanzo vya fedha vya Shirika, usimamizi wa fedha, makadirio ya mapato na matumizt matumizi ya fedha, hesabu na ukaguzi na taarifa ya mwaka.

Sehemu ya VII inaainisha vifungu vya jumla ikiwemo Udhamini wa vipindi, matengenezo au mabadiliko yanayoweza kuharibu mfumo wa matangazo, uanzishwaji wa chaneli maaiurnu: adhabu ya jumla na mamlaka ya Waziri kutengeneza kanuni.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Prof. Palamagamba J. A. M. Kabudi, (Mb)
**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI. SANAA NA MICHEZO**
30 Januari, 2025.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa natafuta maana ya "fauka", nimeipata. Sijui wengine kama wanaijua maana ya "fauka", lakini ndiyo hivyo, tuendelee kujifunza Kiswahili fasaha. *(Kicheko)*

Haya, namwita sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, kwa niaba yake anakuja Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe. *(Makofi)*

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, kuhusu Muswada wa Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania wa Mwaka 2024. Awali ya yote naomba taarifa hii iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ilivyowasilishwa Mezani awali.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Machi, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Kuhusu Muswada wa Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania wa Mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ulisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza katika Mkutano wa Kumi na Sita, Kikao cha Sita, siku ya Ijumaa tarehe 6 Septemba, 2024. Baada ya hatua hiyo, na kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 97 (1) ikisomwa pamoja na Kanuni 136 (14) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ulitumia mamlaka yako kuuleta Muswada kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ili Kamati iujadili na kuufanyia uchambuzi.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Miswada ya Sheria ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika kutekeleza jukumu hilo, kama ilivyo desturi, Kamati ilianza uchambuzi wake kwa kupokea na kujadili Maelezo ya Serikali kuhusu maudhui ya Muswada, ambayo yaliwasilishwa na Mheshimiwa Jerry William Silaa siku ya Jumatano tarehe 16 Oktoba, 2024 akiwa Waziri wa iliyokuwa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kabla ya mabadiliko ya muundo wa Wizara yaliyofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 8 Desemba, 2024.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea Maelezo ya Serikali kuhusu Muswada, Kamati ilifanya Mkutano wa Kupokea Maoni ya Wadau *(Public Hearing)* siku ya Alhamisi tarehe 17 Oktoba, 2024 ili kutimiza masharti ya Kanuni ya 97 (2). Katika Mkutano huo, Kamati ilipokea na kujadili maoni ya wadau wafuatao: -

(i) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (*UDSM*);
(ii) Jukwaa la Wahariri Tanzania;
(iii) Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu *(LHRC)*; na
(iv) Wadau wengine binafsi.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati kabisa wadau wote waliofika mbele ya Kamati kutoa maoni yao na wale ambao waliwasilisha maoni yao kwa njia ya maandishi. Kwa kiasi kikubwa, maoni hayo yameongeza mawanda ya uchambuzi wa Kamati kuhusu maudhui ya masharti mbalimbali yaliyomo katika Muswada wa Sheria ya Utangazaji Tanzania wa Mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa Muswada, kwa maelezo ya awali, uchambuzi uliofanywa na Kamati, kwanza ulijielekeza katika masuala ya jumla kuhusiana na maudhui, masharti, mpangilio, na madhumuni ya sheria iliyopendekezwa kutungwa. Aidha, Kamati ilitathmini masuala mahususi ikiwemo ubora, utekelezaji *(practicability)* wa masharti mbalimbali, pamoja na masuala mengine katika kila ibara ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati ilifanya rejea katika nyaraka mbalimbali pamoja na uzoefu katika nchi nyingine katika suala zima la uendelezaji, uendeshaji na usimamizi wa mashirika ya umma ya utangazaji. Katika rejea hizo, Kamati ilifanya uchanganuzi linganifu *(comparative analysis)* kwa lengo la kubaini maeneo ambayo yangeweza kuboresha masharti ya sheria inayopendekezwa kutungwa.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania ili kuweka mfumo madhubuti na thabiti wa usimamizi na uendeshaji wa Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)* likiwa ni chombo cha utangazaji cha umma.

Mheshimiwa Spika, moja kati ya mambo ambayo Kamati imebaini ni kwamba, pamoja na kuanzishwa kwa Shirika la Utangazaji, Tanzania kupitia Amri ya Uanzishwaji wa Shirika la Utangazaji Tanzania, 2007 (Tangazo la Serikali Na. 186 la Mwaka 2007), Shirika hilo limepitia

changamoto mbalimbali za kiuendeshaji. Baadhi ya changamoto zilizobainika ni pamoja na kukosekana kwa msingi imara wa kisheria unaohakikisha uendelevu wa Shirika la Utangazaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, kutokana na kuanzishwa kwa Shirika chini ya Amri ya Uanzishwaji, Waziri mwenye dhamana ya utangazaji hakupewa mamlaka ya kutengeneza kanuni kwa ajili ya kusimamia na kuendesha masuala mbalimbali yanayohusiana na utendaji bora wa Shirika ikiwemo ukusanyaji wa mapato na ulinzi wa miundombinu ya utangazaji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto zilizobainika katika usimamizi, uendeshaji na uendelevu wa Shirika la Utangazaji Tanzania, sheria inayopendekezwa itajumuisha masharti ambayo yanayotoa ufafanuzi, ufumbuzi wa changamoto hizo ili kuwezesha Shirika la Utangazaji Tanzania kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa masharti yanayopatikana katika ibara mbalimbali za Muswada. Katika uchambuzi huo, Kamati ilibaini masuala kadhaa ambayo yalifanyiwa upembuzi kwa lengo la kuboresha maudhui yake. Aidha, Kamati iliainisha masuala hayo na kuyawasilisha kwa Serikali kwa lengo la kuboresha Muswada husika.

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako kwamba, kwa sehemu kubwa, maoni na ushauri wa Kamati kwa Serikali umezingatiwa katika kuboresha maudhui ya masharti yaliyomo katika Muswada. Hata hivyo, kwa ajili ya kuweka Kumbukumbu za Bunge sawa, nitazungumzia kwa msisitizo baadhi ya sehemu na ibara za Muswada ambazo Kamati ilizifanyia uchambuzi.

Mheshimiwa Spika, moja kati ya maeneo ambayo Kamati ilijadili na kupendekeza maboresho ni Jina Refu la Muswada ambapo Kamati ilishauri Serikali kuondoa dhana ya "kutambua mwendelezo wa uwepo wa Shirika" na badala yake kuweka masharti ya "kuendeleza, kusimamia na kuendesha Shirika".

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya yana lengo la kuboresha mawanda ya Jina Refu ili iendane na maudhui makuu ya kuendeleza shirika, bila kulazimika kubainisha utambuzi wake kwa kuwa tayari shirika linatambuliwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza ya Muswada, inaweka Masharti ya Utangulizi na inajumuisha Jina la Sheria, tarehe ya kuanza kutumika, mipaka ya matumizi, pamoja na kutoa tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya Nne inazungumzia majukumu na mamlaka ya Shirika la Utangazaji. Majukumu hayo yanajumuisha Shirika kutoa huduma za utangazaji wa umma, kushiriki katika matukio yote ya kitaifa yakiwemo yanayohusisha Viongozi Wakuu wa Serikali yenye maslahi ya umma na pia kutumia teknolojia mpya na zinazoibukia ambazo zinaendana na malengo ya Shirika.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake, Kamati ilitathmini nafasi ya Shirika kuongeza ushawishi kwa lengo la kuliwezesha Taifa kuenzi na kutunza maudhui, mila na desturi zetu. Kwa muktadha huo, Kamati imeishauri Serikali kuongeza jukumu la kuendeleza na kukuza uzalendo wa Taifa la Tanzania kwa kutumia sanaa, nyimbo, muziki na njia yoyote iwayo kwa kuendana na teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu, Ibara ya Sita ya Muswada inapendekeza kuanzisha Bodi ya Shirika ambayo itakuwa na Mwenyekiti atakayeteuliwa na Rais, Wajumbe nane watakaoteuliwa na Waziri na kwamba Mkurugenzi Mkuu wa Shirika atakuwa ndiye Katibu wa Bodi hiyo. Ibara hiyo pia inaainisha masuala yanayohusu muda wa kukaa madarakani, akidi, vikao na masuala mengine ambayo yataainishwa kwenye Jedwali la Sheria inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, moja kati ya masuala mahususi yaliyojadiliwa katika ibara hiyo ni sifa za Wajumbe wa Bodi ya kuwa na uzoefu wa miaka kumi na kwa mujibu wa masharti yanayopatikana katika Ibara ya 6(2)(b). Kama ilifanya tathmini ili kuona iwapo masharti hayo yataongeza ufanisi wa utendaji wa Bodi bila kuwepo kwa kigezo cha

kuwa na uzoefu wa miaka kumi ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa watu sahihi kutekeleza majukumu ya Bodi.

Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano ya kina, Kamati ilikubaliana na Serikali kwamba masharti yaliyomo katika Muswada yabaki kama yalivyo kwa kuzingatia umuhimu wa Wajumbe wa Bodi hiyo kuwa na uzoefu wa kutosha ili kutoa ushauri stahiki wa namna bora ya kuendesha Shirika.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya Saba inazitaja sifa mbalimbali za kuwa Mjumbe wa Bodi. Ili kuboresha uandishi wa ibara hiyo, Kamati imeishauri Serikali kuondoa neno "au" na badala yake kuweka neno "na" baada ya Ibara ya 7(1)(e) na kabla ya Ibara ya 7(1)(f). Lengo la mapendekezo hayo ni kupata Wajumbe wa Bodi wenye sifa zote zinazopendekezwa na Muswada.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada inahusu Makatazo. Ibara ya 18 inaweka katazo la kuingia kwenye eneo la Shirika bila ruhusa kwa mtu yeyote ambaye si mtumishi wa Shirika. Muswada unapendekeza kwamba mtu yeyote ambaye anatenda kosa na kutiwa hatiani kwa mujibu wa masharti ya ibara hii, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni 10 na isiyozidi shilingi milioni 20 au kifungo kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka mitano au vyote.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kwamba baadhi ya makosa ambayo yanatajwa katika ibara hii yanajumuisha matendo ambayo yanaweza yakafanywa katika mazingira ya bahati mbaya, mfano kukutwa katika eneo lolote linalomilikwa na shirika kwa mujibu wa Ibara ya 18(a), Kamati inaishauri Serikali kupunguza adhabu ya faini inayopatikana katika Ibara hii. Kamati inapendekeza Muswada kuweka adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni mbili na isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi miezi mitatu au vyote. Lengo la mapendekezo hayo ni kufanya sheria inayopendekezwa kuweka adhabu inayolingana na ukubwa wa kosa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Saba inaweka masharti mbalimbali ya jumla. Ibara ya 27 inahusu Matengenezo au Mabadiliko yanayoweza Kuharibu Mfumo, ambapo Kamati inashauri kuboresha maudhui yake ili kuweka wajibu wa kutoa notisi kwa shirika kabla ya kufanya matengenezo au maboresho ya miundombinu ya taasisi. Lengo la mapendekezo haya ni kulipa shirika uwezo wa kufanya uangalizi wa miundombinu yake wakati wa matengenezo au mabadiliko yanayofanywa na taasisi nyingine.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania wa Mwaka 2024. Sheria inayopendekezwa inatarajia kuweka mfumo madhubuti na thabiti wa usimamizi na uendeshaji wa Shirika la Utangazaji Tanzania. Kwa muktadha huo, Kamati ina maoni kwamba ili sheria inayopendekezwa iweze kuleta tija inayotarajiwa, Shirika la Utangazaji Tanzania lifanye yafuatayo:-

(a) Lihakikishe linafikisha matangazo kwa wananchi wote nchini bila kujali umbali, uchache wa watu kwenye eneo, au gharama za uwekezaji na uendeshaji;

(b) Kuandaa na kurusha maudhui yanayogusa maisha ya makundi yote ya jamii kwa kuzingatia utamaduni wa Taifa/Kiafrika; na

(c) Kuhamasisha, kuelimisha na kudumisha uzalendo miongoni mwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri Mahususi, Ibara ya Nne ya Muswada inaweka masharti kuhusu majukumu ya mamlaka ya Shirika moja kati ya majukumu hayo ni Shirika kuanzisha Maktaba na kutunza kumbukumbu zenye maudhui yanayohusiana na malengo ya Shirika.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, Kamati inaishauri Serikali kwamba, wakati wa utekelezaji wa Sheria inayopendekezwa, Shirika liweke mkakati madhubuti wa kuwa na Maktaba ya Kisasa ambayo itakidhi vigezo vinavyoakisi hali halisi ya mabadiliko ya teknolojia ya

habari na mawasiliano. Aidha, kwa lengo la kuhakikisha kwamba umma unanufaika na uwekezaji huo, Shirika lihakikishe kwamba, maudhui yanayohifadhiwa katika maktaba hiyo yanawafikia wananchi walio wengi zaidi kwa kadri inavyowezekana na kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, Wajibu wa Shirika katika kuandaa vipindi vyenye maudhui bora ya Kitanzania. Ibara ya Tano ya Muswada inalipa Shirika Wajibu wa Kuandaa Vipindi. Kwa kuzingatia hilo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba, Shirika la Utangazaji Tanzania, kupitia vyombo vyake vyote vya Habari, vinakuwa mfano na kielelezo cha kuandaa vipindi bora na vyenye ubunifu lakini pia vyenye malengo ya kulinda, kuimarisha na kudumusha utamaduni wa Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kwamba tasnia ya burudani nchini inakua kwa kasi, ni vema Serikali kupitia Shirika la Utangazaji ikawa na programu maalumu yenye lengo la kuhamasisha wazalishaji binafsi wa vipindi na maudhui kutengeneza vipindi na maudhui yenye ubora na kupata nafasi ya kuoneshwa au kutangazwa katika vyombo vya Habari vya Shirika. Juhudi hizo ziende sambamba na motisha ya kifedha inayoakisi ushindani wa soko kutokana na ubora wa maudhui hayo.

Mheshimiwa Spika, matumizi bora ya rasilimali za umma na utekelezaji wa miradi yenye tija. Ibara ya 3(2), pamoja na masharti mengine, inalipa Shirika uwezo wa kukopa fedha, kuingia mikataba mbalimbali pamoja na kupata, kumiliki na kutoa mali zinazohamishika na zisizohamishika.

Mheshimiwa Spika, aidha, Ibara ya 13 inampa Mkurugenzi Mkuu majukumu ya kusimamia rasilimali za Shirika ili kukidhi mipango ya uendeshaji wa Shirika. Kwa muktadha huo, na kwa kuzingatia masharti yanayopendekezwa katika Ibara ya 8(1), Kamati inaishari Serikali kuhakikisha kwamba Bodi ya Shirika inasimamia kikamilifu matumizi bora ya rasilimali za umma.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 20 ya Muswada inahusu vyanzo vya fedha vya Shirika. Moja ya masharti ambayo yalijadiliwa kwa kina na Kamati wakati wa uchambuzi ni yale yanayopatikana katika Ibara ya 20(1)(C). Masharti hayo yameainishwa kwamba moja ya vyanzo vya fedha vya Shirika ni ada na tozo kwenye bidhaa au huduma ambazo Serikali itaelekeza kwa ajili ya utangazaji wa umma.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba utekelezaji wa Shirika inayopendekezwa unakuwa bora, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba aina yoyote ya ada na tozo katika masharti ya Ibara hii haitaongeza gharama kwa mtumiaji wa mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, nawashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, ambao katika kutekeleza majukumu yao ya kikatiba, walichambua, kujadili, na kutoa maoni mbalimbali kwa lengo la kuboresha maudhui ya Muswada huu. Kwa kutambua mchango wao, naomba majina yao yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Jerry William Silaa, Mbunge, akisaidiwa na Naibu Waziri, Mheshimiwa *Eng.* Maryprica Winfred Mahundi, Mbunge, kwa ushirikiano ambao wameipatia Kamati wakati wa uchambuzi wa Muswada wa Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, nawashukuru Watendaji wa iliyokuwa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, pamoja na Uongozi wa Shirika la Utangazaji wa Tanzania *(TBC)* na ushirikiano wao katika kipindi chote cha Uchambuzi wa Muswada. Aidha, nawashukuru Watendaji wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Hamza Saidi Johari, Mbunge, kwa namna ambavyo walikuwa tayari kutoa ufafanuzi kuhusu masharti mbalimbali yanayopatikana katika Muswada.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Shirika la Utangazaji Tanzania sasa liko katika Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, nitumie fursa hii kumpongeza Waziri wa Wizara hiyo Mheshimiwa Prof. Palamagamba

John Aidan Mwaluko Kabudi, Mbunge, pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma, Mbunge, kwa kuaminiwa na Rais kuongoza sekta ya habari nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, niwatakie kila la heri katika utekelezaji wa Sheria inayopendekezwa kutungwa kwa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Ildephonce Leonard kwa kuratibu Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kuwa hii ni mara ya kwanza Kamati kuwasilisha taarifa Bungeni tangu kuteuliwa kwa Katibu wa Bunge, nichukue fursa hii adhimu kumpongeza kwa kuaminiwa na Rais kuteuliwa kushika wadhifa huo, na pia kumkaribisha katika Familia ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja. Baada ya kusema hayo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu inalishauri Bunge lako Tukufu kuujadili, kuukubali na kisha kuupitisha Muswada wa Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania wa Mwaka 2024 pamoja na Jedwali la Marekebisho kama ulivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, niaba ya Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

# Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Kuhusu Muswada wa Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania wa Mwaka 2024 – Kama Ilivyowasilishwa Mezani

*(Kanuni ya 99(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023)*

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 99 (5)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Machi, 2023, naomba kuwasilisha **Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Kuhusu Muswada wa Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania wa Mwaka 2024**.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu ulisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza katika Mkutano wa Kumi na Sita, Kikao cha Sita, siku ya Ijumaa tarehe 06 Septemba, 2024. Baada ya hatua hiyo na kwa kuzingatia masharti ya **Kanuni ya 97 (1)** ikisomwa pamoja na **Kanuni 136 (14)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ulitumia mamlaka yako kuuleta Muswada kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ili Kamati iujadili na kuufanyia uchambuzi.

### 1.2 Namna Kamati Ilivyotekeleza Majukumu Yake

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Miswada ya Sheria ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa mujibu wa **Kifungu cha 7(1) (b)** cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika kuteleza jukumu hilo, kama ilivyo desturi, Kamati ilianza uchambuzi wake kwa kupokea na kujadili Maelezo ya Serikali kuhusu maudhui ya Muswada, ambayo yaliwasilishwa na Mhe. Jerry William Silaa siku ya Jumatano tarehe 16 Oktoba, 2024 akiwa Waziri wa iliyokuwa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kabla

ya mabadiliko ya muundo wa Wizara yaliyofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 08 Disemba, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kupokea Maelezo ya Serikali kuhusu Muswada, Kamati ilifanya Mkutano wa Kupokea Maoni ya Wadau *(Public Hearing)* siku ya Alhamis tarehe 17 Oktoba, 2024 ili kutimiza masharti ya **Kanuni ya 97 (2)**. Katika Mkutano huo, Kamati ilipokea na kujadili maoni ya wadau wafuatao: -

1. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM)
2. Jukwaa la Wahariri Tanzania
3. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC); na
4. Wadau wengine binafsi.

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati kabisa, wadau wote waliofika mbele ya Kamati kutoa maoni yao na wale ambao waliwasilisha maoni yao kwa njia ya maandishi. Kwa kiasi kikubwa, maoni hayo yameongeza mawanda ya Uchambuzi wa Kamati kuhusu maudhui ya masharti mbalimbali yaliyomo katika Muswada wa Sheria ya Utangazaji Tanzania wa Mwaka 2024.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

### 2.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi uliofanywa na Kamati, kwanza ulijielekeza katika masuala ya jumla kuhusiana na maudhui, masharti, mpangilio, na madhumuni ya Sheria inayopendekezwa kutungwa. Aidha, Kamati ilitathmini masuala mahsusi ikiwemo ubora, utekelezaji *(practicability)* wa masharti mbalimbali, pamoja na masuala mengine katika kila ibara ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile Kamati ilifanya rejea katika nyaraka mbalimbali pamoja na uzoefu katika nchi nyingine katika suala zima la uendelezaji, uendeshaji na usimamizi wa mashirika ya umma ya

utangazaji. Katika rejea hizo, Kamati ilifanya uchanganuzi linganifu *(comparative analysis)* kwa lengo la kubaini maeneo ambayo yangeweza kuboresha masharti ya Sheria inayopendekezwa kutungwa.

**2.2 Upembuzi wa Maudhui**

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania ili kuweka mfumo madhubuti na thabiti wa usimamizi na uendeshaji wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) likiwa ni chombo cha utangazaji cha umma.

**Mheshimiwa Spika**, moja kati ya mambo ambayo kamati imebaini ni kwamba, pamoja na kuanzishwa kwa Shirika la Utangazaji Tanzania kupitia Amri ya Uanzishwaji wa Shirika la Utangazaji Tanzania, 2007 (Tangazo la Serikali Na. 186 la Mwaka 2007), Shirika hilo limepitia changamoto mbalimbali za kiuendeshaji. Baadhi ya changamoto zilizobainika ni pamoja na kukosekana kwa msingi imara wa kisheria unaohakikisha uendelevu wa Shirika la Utangazaji. Aidha, kutokana na kuanzishwa kwa Shirika chini ya Amri ya Uanzishwaji, Waziri mwenye dhamana ya utangazaji hakupewa mamlaka ya kutengeneza kanuni kwa ajili ya kusimamia na kuendesha masuala mbalimbali yanayohusiana na utendaji bora wa Shirika ikiwemo ukusanyaji wa mapato na ulinzi wa miundombinu ya utangazaji.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na changamoto zilizobainika katika usimamizi, uendeshaji na uendelevu wa Shirika la Utangazaji Tanzania, Sheria inayopendekezwa itajumuisha masharti ambayo yanayotoa ufumbuzi wa changamoto hizo ili kuliwezesha Shirika la Utangazaji Tanzania kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

**2.3 Uchambuzi Kuhusu Masharti ya Ibara za Muswada**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi wa masharti yanayopatikana katika Ibara mbalimbali za Muswada. Katika uchambuzi huo, Kamati ilibaini masuala kadhaa ambayo yalifanyiwa

upembuzi kwa lengo la kuboresha maudhui yake. Aidha, Kamati iliainisha masuala hayo na kuyawasilisha kwa Serikali kwa lengo la kuboresha Muswada husika.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulijulisha Bunge lako kwamba, kwa sehemu kubwa, maoni na ushauri wa Kamati kwa Serikali umezingatiwa katika kuboresha maudhui ya masharti yaliyomo katika Muswada. Hata hivyo, kwa ajili ya kuweka Kumbukumbu za Bunge sawa, nitazungumia kwa msisitizo baadhi ya sehemu na ibara za muswada ambazo Kamati ilizifanyia uchambuzi.

**Mheshimiwa Spika**, moja kati ya maeneo ambayo kamati ilijadili na kupendekeza maboresho ni **Jina Refu la Muswada** ambapo Kamati ilishauri Serikali kuondoa dhana ya "…**kutambua mwendelezo wa uwepo wa Shirika…**" na badala yake kuweka masharti ya "…**kuendeleza, kusimamia na kuendesha Shirika**…".

**Mheshimiwa Spika**, mapendekezo haya yana lengo la kuboresha mawanda ya Jina Refu ili liendane na madhumuni makuu ya kuendeleza Shirika bila kulazimika kubainisha utambuzi wake kwa kuwa tayari Shirika lilikuwa linatambuliwa.

### 2.3.1 Sehemu ya Kwanza ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inaweka Masharti ya Utangulizi na inajumuisha Jina la Sheria, Tarehe ya Kuanza Kutumika, Mipaka ya Matumizi, pamoja na kutoa Tafsiri ya Maneno mbalimbali yaliyotumika.

**Mheshimiwa Spika**, katika Ibara ya 2 ambayo inatoa tafsiri ya maneno mbalimbali, Kamati ilifanya tathimini ya maneno **"Viongozi Wakuu wa Serikali"**. Maneno hayo yanatafsiriwa kujumuisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Waziri Mkuu na Naibu Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na nia ya Serikali, Kamati inashauri kwamba tafsiri ya maneno hayo isijumuishe nafasi ya Naibu Waziri

Mkuu. Mapendekezo ya Kamati yamezingatia ukweli kwamba, masharti ya Sehemu ya Pili ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yamekitaja cheo cha Waziri Mkuu ambaye ni Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, pamoja na Baraza la Mawaziri. Kwa muktadha huo, nafasi ya Naibu Waziri Mkuu ni sehemu ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo tayari imeshatajwa katika Katiba.

**2.3.2 Sehemu ya Pili ya Muswada**

**Mheshimiwa Spika**, **Ibara ya 4** inazungumzia Majukumu na Mamlaka ya Shirika la Utangazaji. Majukumu hayo yanajumuisha Shirika kutoa huduma za utangazaji wa umma, kushiriki katika matukio yote ya kitaifa yakiwemo yanayohusisha Viongozi Wakuu wa Serikali yenye maslahi ya umma na pia kutumia teknolojia mpya na zinazoibukia ambazo zinaendana na malengo ya Shirika.

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake, Kamati ilitathmini nafasi ya Shirika kuongeza ushawishi kwa lengo la kuliwezesha Taifa kuenzi na kutunza maudhui, mila na desturi zetu. Kwa muktadha huo, Kamati imeishauri Serikali kuongeza jukumu la "**kuendeleza na kukuza uzalendo wa Taifa la Tanzania kwa kutumia sanaa, nyimbo, muziki na njia yoyote iwayo kwa kuendana na teknolojia ya kisasa**".

**2.3.3 Sehemu ya Tatu ya Muswada**

**Mheshimiwa Spika**, **Ibara ya 6** ya Muswada inapendekeza kuanzisha Bodi ya Shirika ambayo itakuwa na Mwenyekiti atakayeteuliwa na Rais, Wajumbe nane watakaoteuliwa na Waziri na kwamba Mkurugenzi Mkuu wa Shirika atakuwa ndiye Katibu wa Bodi hiyo. Ibara hiyo pia inaainisha masuala yanayohusu muda wa kukaa madarakani, akidi, vikao na masuala mengine ambayo yataainishwa kwenye Jedwali la Sheria inayopendekezwa.

**Mheshimiwa Spika**, moja kati ya masuala mahsusi yaliyojadiliwa katika Ibara hiyo ni sifa za Wajumbe wa Bodi ya kuwa na uzoefu wa miaka

kumi kwa mujibu wa masharti yanayopatikana katika **Ibara ya 6 (2) (b)**.

Kamati ilifanya tathmini ili kuona iwapo masharti hayo yataongeza ufanisi wa utendaji wa Bodi bila kuwepo kwa kigezo cha kuwa na uzoefu wa miaka kumi ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa watu sahihi kutekeleza majukumu ya Bodi.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya majadiliano ya kina, Kamati ilikubaliana na Serikali kwamba masharti yaliyomo katika Muswada yabaki kama yalivyo kwa kuzingatia umuhimu wa Wajumbe wa Bodi hiyo kuwa na uzoefu wa kutosha ili kutoa ushauri stahiki wa namna bora ya kuendesha Shirika.

**Mheshimiwa Spika**, **Ibara ya 7** inazitaja sifa mbalimbali za kuwa Mjumbe wa Bodi. Ili kuboresha uandishi wa Ibara hiyo, Kamati imeishauri Serikali kuondoa neno “**au**” na badala yake kuweka neno “**na**” baada ya Ibara ya 7 (1) (e) na kabla ya Ibara ya 7 (1) (f). Lengo la mapendekezo haya ni kupata Wajumbe wa Bodi wenye sifa zote zinazopendekezwa na Muswada.

### 2.3.4 Sehemu ya Tano ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu hii inahusu Makatazo. **Ibara ya 18** inaweka katazo la kuingia kwenye Eneo la Shirika bila ruhusa kwa mtu yeyote ambaye si mtumishi wa Shirika. Muswada unapendekeza kwamba mtu yeyote ambaye anatenda kosa na kutiwa hatiani kwa mujibu wa masharti ya Ibara hii, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni kumi na isiyozidi shilingi milioni ishirini au kifungo kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka mitano au vyote.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia kwamba baadhi ya makosa ambayo yanatajwa katika Ibara hii yanajumuisha matendo ambayo yanaweza yakafanywa katika mazingira ya bahati mbaya, mfano kukutwa katika eneo lolote linalomilikwa na shirika kwa mujibu wa **Ibara ya 18 (a)**, Kamati inaishauri Serikali kupunguza adhabu ya faini inayopatikana katika Ibara hii. Kamati inapendekeza Muswada

kuweka adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni mbili na isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka mitatu au vyote. Lengo la mapendekezo haya ni kuifanya Sheria inayopendekezwa kuweka adhabu inayolingana na ukubwa wa kosa.

### 2.3.5 Sehemu ya Saba ya Muswada

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu hii inaweka masharti mbalimbali ya jumla. **Ibara ya 27** inahusu Matengenezo au Mabadiliko Yanayoweza Kuharibu Mfumo, ambapo Kamati inashauri kuboresha maudhui yake ili kuweka wajibu wa kutoa notisi kwa Shirika kabla ya kufanya matengenezo au maboresho ya miundombinu ya taasisi. Lengo la mapendekezo haya ni kulipa Shirika uwezo wa kufanya uangalizi wa miundombinu yake wakati wa matengenezo au mabadiliko yanayofanywa na taasisi nyingine.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maoni na Ushauri wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Shirika la Utangazaji wa Tanzania wa Mwaka wa 2024. Sheria inayopendekezwa inatarajiwa kuweka mfumo Madhubuti na thabiti wa usimamizi na uendeshaji wa Shirika la Utangazaji Tanzania. Kwa muktadha huo Kamati ina maoni kwamba, ili Sheria inayopendekezwa iweze kuleta tija inayotarajiwa, Shirika la Utangazaji Tanzania lifanye yafuatayo: -

a) Lihakikishe linafikisha matangazo kwa wananchi wote nchini bila kujali umbali, uchache wa watu kwenye eneo, au gharama za uwekezaji na uendeshaji;

b) Kuandaa na kurusha maudhui yanayogusa maisha ya makundi yote ya jamii kwa kuzingatia utamaduni wa Taifa/Kiafrika; na

c) Kuhamasisha, kuelimisha na kudumisha uzalendo miongoni mwa Watanzania.

### 3.2 Maoni na Ushauri Mahsusi

#### 3.2.1 Umuhimu wa Shirika Kuwa na Maktaba ya Kisasa

**Mheshimiwa Spika**, **Ibara ya 4** ya Muswada inaweka masharti kuhusu majukumu na mamlaka ya Shirika. Moja kati ya majukumu hayo, ni Shirika kuanzisha maktaba na kutunza kumbukumbu zenye maudhui yanayohusiana na malengo ya Shirika. Kwa muktadha huo, Kamati inaishauri Serikali kwamba, wakati wa utekelezaji wa Sheria inayopendekezwa, Shirika liweke mkakati madhubuti wa kuwa na Maktaba ya Kisasa ambayo itakidhi vigezo vinavyoakisi hali halisi ya mabadiliko ya teknolojia ya habari na mawasiliano. Aidha, kwa lengo la kuhakikisha kwamba umma unanufaika na uwekezaji huo, Shirika lihakikishe kwamba, maudhui yanayohifadhiwa katika maktaba hiyo yanawafikia wananchi walio wengi zaidi kwa kadri inavyowezekana na kwa urahisi.

#### 3.2.2 Wajibu wa Shirika Katika Kuandaa Vipindi Vyenye Maudhui Bora ya Kitanzania

**Mheshimiwa Spika**, **Ibara ya 5** Muswada inalipa Shirika Wajibu wa Kuandaa Vipindi. Kwa kuzingatia hilo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba, Shirika la Utangazaji Tanzania, kupitia vyombo vyake vyote vya Habari, vinakuwa mfano na kielelezo cha kuandaa vipindi bora na vyenye ubunifu lakini pia vyenye malengo ya kulinda, kuimarisha na kudumusha utamaduni wa Kitanzania.

#### 3.2.3 Motisha kwa Watengezaji Binafsi wa Maudhui na Vipindi

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia kwamba tasnia ya burudani nchini inakua kwa kasi, ni vema Serikali kupitia Shirika la Utangazaji ikawa na

programu maalum yenye lengo la kuhamasisha wazalishaji binafsi wa vipindi na maudhui kutengeneza vipindi na maudhui yenye ubora na kupata nafasi ya kuoneshwa au kutangazwa katika vyombo vya Habari vya Shirika. Juhudi hizo ziende sambamba na motisha ya kifedha inayoakishi ushindani wa soko kutokana na ubora wa maudhui hayo.

### 3.2.4 Matumizi Bora ya Rasilimali za Umma na Utekelezaji wa Miradi yenye tija

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 3 (2)**, pamoja na masharti mengine, inalipa Shirika uwezo wa kukopa fedha, kuingia mikataba mbalimbali pamoja na kupata, kumiliki na kutoa mali zinazohamishika na zisizohamishika. Aidha, **Ibara ya 13** inampa Mkurugenzi Mkuu majukumu ya kusimamia rasilimali za Shirika ili kukidhi mipango ya uendeshaji wa Shirika. Kwa muktadha huo, na kwa kuzingatia masharti yanayopendekezwa katika **Ibara ya 8 (1)**, Kamati inaishari Serikali kuhakikisha kwamba Bodi ya Shirika inasimamia kikamilifu matumizi bora ya rasilimali za umma.

### 3.2.5 Vyanzo vya Fedha vya Shirika

**Mheshimiwa Spika**, **Ibara ya 20** ya Muswada inahusu Vyanzo vya Fedha vya Shirika. Moja kati ya masharti ambayo yalijadiliwa kwa kina na Kamati wakati wa uchambuzi, ni yale yanayopatikana katika Ibara ya 20 (1) (C). Masharti hayo yameainisha kwamba moja ya Vyanzo vya Fedha vya Shirika ni ada na tozo kwenye bidhaa au huduma ambazo Serikali itaelekeza kwa ajili ya utangazaji wa umma. Ili kuhakikisha kwamba utekelezaji wa Sheria inayopendekezwa unakuwa bora, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba aina yoyote ya ada na tozo katika masharti ya Ibara hii haitaongeza gharama kwa mtumiaji wa mwisho.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, ambao katika kutekeleza majukumu yao kikatiba, walichambua, kujadili, na kutoa maoni mbalimbali kwa lengo la kuboresha maudhui ya Muswada huu. Kwa kutambua mchango wao, naomba majina yao yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Moshi Selemani Kakoso, Mb. **Mwenyekiti**
2. Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb. **Makamu**
3. Mhe. Kapt. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb. Mjumbe
4. Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo, Mb. Mjumbe
5. Mhe. Abubakar Damian Asenga, Mb. Mjumbe
6. Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb. Mjumbe
7. Mhe. Ally Anyigulile Mlaghila Jumbe, Mb. Mjumbe
8. Mhe. Amina Ali Mzee, Mb. Mjumbe
9. Mhe. Angelina Adam Malembeka, Mb. Mjumbe
10. Mhe. Fredrick Edward Lowassa, Mb. Mjumbe
11. Mhe. Geoffrey Idelphonce Mwambe, Mb. Mjumbe
12. Mhe. Ghati Zephania Chomete, Mb. Mjumbe
13. Mhe. Innocent Edward Kalogeris, Mb. Mjumbe
14. Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako Mb. Mjumbe
15. Mhe. Livingstone Joseph Lusinde, Mb. Mjumbe
16. Mhe. Mbarouk Juma Khatib, Mb. Mjumbe
17. Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu, Mb. Mjumbe
18. Mhe. Mohamed Maulid Ali, Mb. Mjumbe
19. Mhe. Eng. Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mb. Mjumbe
20. Mhe. Mwatumu Dau Haji, Mb. Mjumbe
21. Mhe. Stella Simon Fiyao, Mb. Mjumbe
22. Mhe. Sylvia Francis Sigula, Mb. Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Jerry William Silaa (Mb.) akisaidiwa na Naibu Waziri, Mhe. Eng. Maryprica Winfred Mahundi (Mb.) kwa ushirikiano ambao wameipatia Kamati wakati wa uchambuzi wa Muswada wa Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania. Vilevile, niwashukuru watendaji wa iliyokuwa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, pamoja na Uongozi wa Shirika la Utangazaji wa Tanzania (TBC) kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha Uchambuzi wa Muswada. Aidha, niwashukuru watendaji wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, chini ya uongozi wa Mhe. Hamza Saidi Johari, (Mb.) kwa namna ambavyo walikuwa tayari kutoa ufafanuzi kuhusu masharti mbalimbali yanayopatikana katika Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Shirika la Utangazaji Tanzania sasa liko chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, nitumie fursa kumpongeza Waziri wa wizara hiyo Mhe. Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb.) pamoja na Naibu Waziri, Mhe. Hamis Mohamed Mwinjuma (Mb.) kwa kuaminiwa na Rais kuongoza sekta ya habari nchini. Kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, niwatakie kila la heri katika utekelezaji wa Sheria inayopendekezwa kutungwa kwa Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge, Ndg. Baraka Ildephonce Leonard kwa kuratibu Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa Taarifa hii. Aidha, kwa kuwa hii ni mara ya kwanza Kamati kuwasilisha taarifa Bungeni tangu kuteuliwa kwa Katibu wa Bunge, nichukue fursa hii adhimu kumpongeza kwa kuaminiwa na Rais kuteuliwa kushika wadhifa huo, na pia kumkaribisha katika Familia ya Bunge.

### 4.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kisha kuupitisha **Muswada wa Sheria ya Shirika la**

**Utangazaji Tanzania wa Mwaka 2024** pamoja na **Jedwali la Marekebisho** kama ulivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Moshi Selemani Kakoso, Mb.
**MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU**
30 Januari, 2025

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, nakushukuru sana kwa wasilisho hilo kwa niaba ya Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyo ada, nimeletewa majina hapa ya Wabunge ambao wanataka kuchangia kwenye hoja hii. Tutaanza na Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Anyigulile Mlaghila Jumbe, Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris ajiandae.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Muswada huu wa Shirika la Utangazaji Tanzania wa Mwaka 2024 ambao ni Muswada muhimu sana katika kulihuwisha na kulisimamia Shirika letu. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo ameendelea kusimamia Serikali yetu na namna ambavyo ameendelea kuunganisha nchi yetu na dunia na ambavyo amekuwa akitoa uongozi uliotukuka katika kuleta maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuteuliwa na Chama cha Mapinduzi kuwa Mgombea wa Urais wa Mwaka 2025, ni kuonesha tuna imani kubwa naye na aweze kuongoza Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimesema awali kwamba naomba nianze kuchangia Muswada huu muhimu, lakini nitakuwa na vipengele vinne katika kuchangia Muswada huu. La kwanza, nilitaka nieleze kuhusu umuhimu wa *TBC, TBC* ni Shirika la Utangazi Tanzania, ambacho ni chombo muhimu sana katika kukusanya na kuhifadhi maudhui mbalimbali ambayo yanasaidia kulifanya Taifa kuwa katika historia mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, *TBC* kama chombo cha umma tumeshuhudia katika kipindi toka uhuru mpaka leo katika kuhakikisha kwamba kimekuwa ni chombo muhimu siyo katika tu kutunza tu historia. Pia kimekuwa ni chombo muhimu katika kuhamasisha maendeleo.

Mheshimiwa Spika, najua wote tunafahamu baada ya kupata uhuru tuliona namna ambavyo *TBC* ilifanya harakati mbalimbali katika kuhakikisha kwamba inawahabarisha Watanzania katika kuifanya Tanzania ibadilike kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwenye hili naomba nichukue nafasi hii kwa kweli kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu kwa namna ambavyo wameleta sheria hii ambayo kwa hakika itaenda kuleta mapinduzi makubwa katika chombo chetu ambacho ni chombo cha Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pili nilitaka niseme tu kwamba tumeshuhudia hata tulipoenda pale kwenye *Studio* ya Dar es Salaam tumeona kuna *tape* mbalimbali zilizowekwa pale za historia mbalimbali ya viongozi katika kudai uhuru katika eneo hili la Kusini mwa Afrika. Kwa hiyo, nadhani nilitaka niseme tu kwamba *TBC* hii *TBC* ambayo leo tunaizungumza ni *TBC* ambayo nilitaka ibadilishwe kimfumo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kupitia sheria hii ambayo inapendekezwa naamini kabisa tutakua na chombo imara zaidi na chombo ambacho kitaenda kuisaidia nchi yetu. Kwenye eneo hili nampongeza sana Mkurugenzi wa *TBC,* Dkt. Ayub Rioba pamoja na wenzake kwa kweli wanafanya kazi ya kizalendo, wanafanya kazi

nzuri sana kuhakikisha kwamba chombo chetu hiki kinakuwa imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto zake, lakini ukiwasikiliza wanaongea mambo ambayo tukiwapa nguvu hii wataenda kuibadilisha sana *TBC* na itakua ni chombo cha kuigwa katika nchi yetu, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kwamba ni chombo ambacho hakiangalii maeneo ya mvuto wa kibiashara, inachoangalia ni maslahi mapana ya Taifa. Inaenda kuhuisha hata Kiswahili ambacho kuna baadhi ya maeneo Kiswahili kinakua hakijafika, lakini kupitia *TBC* tunaona watu hata wanaweza kuongea Kiswahili. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba ni chombo muhimu sana katika kuleta maendeleo ya Taifa letu na kukuza utamaduni wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni suala la amri ya kuanzisha *TBC*. Kama alivyosema amri ilikuwa Tamko la Mheshimiwa Rais ambayo aliitangaza 2007 kuanzisha Tangazo la Serikali Na. 186 ambalo lilieleza kwamba tumeanzisha *TBC*. Amri hii haikuwa imempa nguvu Waziri kuweza kutunga Kanuni mbalimbali za kuweza kuisaidia *TBC* kuondokana na changamoto zake. Kwa hiyo, kupitia hili ninaamini sheria hii itakuwa ni msaada mkubwa kuhakikisha kwamba, shirika letu linaenda kulingana na muda.

Mheshimiwa Spika, pia, changamoto ambazo tumezisikia wote ni kwamba, *TBC* imekuwa ikipambana na ukata mkubwa wa fedha (mapato). Kwa hiyo, kupitia sheria hii tunayoenda kuitunga, itaenda kuisaidia *TBC* uwezo wa mapato kwa maana kuwa na tozo mbalimbali na mapato ambayo yataisaidia kuhuisha baadhi ya huduma zake, kusimamia miundombinu na kuendana na wakati.

Mheshimiwa Spika, mfano leo *tape* zile tuzibadilishe kutoka kwenye analojia na kwenda kidijiti. Kwa hiyo, maana yake tutakuwa na uwezo wa kusambaza kirahisi zaidi kuliko ilivyo sasa mpaka ufike kwenye *studio* zao ambazo zipo pale Dar es Salaam. Kwa hiyo, ninaamini kabisa kupitia sheria hii itakuwa ni tiba kwa ajili ya kuisaidia *TBC* kuondokana na changamoto ambazo wamekuwa nazo.

Mheshimiwa Spika, pia, sheria hii inaenda kutoa ufumbuzi wa changamoto ambazo tumezieleza. Leo hii kuna baadhi ya mambo ambayo *TBC* haiwezi kufanya. Kwa mfano, leo kuna baadhi ya maeneo kwenye suala la ajira, wamebanwa na Sheria za Utumishi wa Umma ambazo haziwaruhusu wao kuangalia kulingana na maudhui ya watazamaji ambayo wanahitaji kuyaona. Kwa mfano, ukiangalia baadhi ya vyombo vingine, wanaweka watu ambao wana elimu ya kawaida, lakini lengo ni kuwavuta watazamaji waweze kuangalia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwenye eneo hili ambalo Kamati tumekuwa tukihoji, wanasema sheria imetubana. Wanakosa namna ya kuweza kufanya ubunifu mbalimbali, lakini kupitia sheria hii, ninaamini kabisa itaenda kuondoa changamoto ambazo tumekuwa tukiziona na tutaisaidia *TBC* kuondokana na tatizo ambalo tunalo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilitaka niombe tu kwamba, Waheshimiwa Wabunge wote tupitishe sheria hii kwa sababu inaenda kuwa ni suluhisho la changamoto ambazo tumekuwa nazo katika chombo chetu na kwamba itaenda kusaidia katika maslahi ya Taifa. Vilevile, itasaidia kuhakikisha kwamba inarekodi na kuvirusha baadhi ya vipindi ambavyo vitaweza kusaidia katika kuwafanya Watanzania wawe wazalendo na waendelee kuipenda nchi yao.

Mheshimiwa Spika, zaidi wataendelea kutangaza ziara mbalimbali za viongozi na mambo ambayo yanahusiana na maendeleo ya Taifa letu ikiwemo kujenga umoja wetu kama alivyosema Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, naomba nirudie tena kupongeza, na niwatakie kila la heri Wizara katika kazi hii. Sisi kama Wabunge tunaunga mkono hoja kwamba sheria hii ipitishwe, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, atafuatiwa na Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula ajiandae.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja ambayo ipo mbele yetu. Nitumie nafasi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuteuliwa kwake na Mkutano Mkuu wa CCM kuwa mgombea wa nafasi ya Urais kwa Uchaguzi Mkuu ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, nitumie nafasi hii kumpongeza Dkt. Nchimbi naye kwa kuteuliwa kuwa mgombea Mwenza wa Mheshimiwa Rais katika Uchaguzi Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mwinyi kuteuliwa kuwa Mgombea wa nafasi ya Urais kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, nitumie nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kuja na hoja ambayo ipo mbele yetu ya uanzishwaji wa Shirika la Utangazaji la Taifa *(TBC)*. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, naomba kwanza niunge mkono mapendekezo yote ambayo tumependekeza kama Kamati kwa Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uanzishwaji wa *TBC* kisheria unatokana na umuhimu wa kuwa na sheria ambayo inatambuliwa na Bunge. Uanzishwaji wake kama tulivyoelezwa na Mheshimiwa Waziri wa Habari na Utangazaji ni kwamba, kwanza ilikuwa ni kwa tamko la Kiongozi Mkuu wa Nchi kipindi hicho akiwa ni Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, mwaka 2007. Kwake yeye aliona umuhimu wa kuanzishwa kwa shirika hili.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa tunakwenda kulihalalisha kwa sheria kwa kutungwa na chombo kikubwa hiki cha Bunge ambacho ndiyo kinatambulika kisheria kwamba ndiyo kinachotunga sheria ya mambo yote katika uendeshaji wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaamini kabisa kwa kutungwa sheria hii tutakwenda kuipa *TBC* uwezo mkubwa wa kufanya mambo yake kuwa ya kisasa zaidi. Tuna mashirika mengi ya utangazaji katika nchi

hii, tuna *Azam TV*, *ITV*, Wasafi na tuna mambo mengi na redio nyingi. Sisi huku tungetamani kama Bunge, *TBC* ikawa ndiyo chombo kinachoongoza katika kutoa taarifa sahihi katika mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwangu mimi kutungwa kwa sheria hii kunakwenda kuipatia *TBC* uwezo mkubwa wa kufanya mambo makubwa ya Kitaifa ambayo Watanzania tunatarajia kuyaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kushauri na kuliomba Bunge lako Tukufu kwamba, kwa namna moja au nyingine turidhiane na tukubaliane na sheria hii, ili tuweze kuipatia *TBC* kisheria kuwa na vyanzo vya uhakika vya mapato ambavyo vitawawezesha *TBC* kuwa na uhakika wa kuwa na vyombo vya kisasa na kuendana na teknolojia ya habari ya kisasa na kuweza kufikisha maudhui ambayo tunatarajia yaweze kuwafikia Watanzania wote ikiwemo pembezoni mwa nchi, ukitilia maanani kwa sasa hivi *TBC* haisikiki wakati mwingine kwenye mipaka ya nchi, na huko Watanzania wanapata taarifa za redio za nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaamini kwa kuanzishwa sheria hii tutakwenda kuipa *TBC* uwezo wa mapato ili kuweza kununua mitambo na kuweza kupeleka taarifa kwa wananchi wetu. Naomba na nilishauri Bunge tukubaliane na sheria iliyoletwa, tuipitishe ili tuipe uwezo mkubwa *TBC* ikafanye mambo yake. Ninakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, atafuatiwa na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga na Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo ajiandae.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia Muswada ulioko mbele yetu. Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kunijalia afya njema ya kusimama katika hili Bunge lako Tukufu kuchangia Muswada uliopo mbele yako.

Mheshimiwa Spika, nisiwe mchoyo wa shukrani, niungane na Watanzania wenzangu kumpongeza Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ni ukweli usiofichika, mama ametuheshimisha kama Taifa na Watanzania. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. Tumeona Mkutano Mkubwa wa Afrika wa Nishati umefanyika nchini kwetu, ni jambo la kujivunia sisi kama Watanzania. Tunampongeza na tunasema Mama mitano tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza pia Serikali kwa kuleta Muswada huu. Huu Muswada umekuja wakati mwafaka kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. Kwa muda mrefu sana *TBC* imekuwa ikifanya kazi kwenye mazingira magumu. Tunajua ni Shirika la Umma, lakini limekuwa likifanya kazi kwenye mazingira magumu. Tunaamini kwa sheria hii tunayoenda kuitunga, *TBC* itaenda kuleta mabadiliko na mageuzi makubwa katika tasnia ya habari.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati, na tulifanikiwa kujadili Muswada huu kwa kina sana. Niungane na maoni na mapendekezo ya Kamati ambayo yamewasilishwa hapo mbele kwa niaba ya Mwenyekiti na Mjumbe mwenzetu wa Kamati, lakini nilikuwa nina vitu viwili ambavyo ningependa kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada umeeleza vizuri, nami ningependa kuchangia kipengele cha makosa na adhabu. Tunajua kabisa kwenye adhabu lazima tuangalie uwiano kati ya kosa na adhabu. Sasa, tunajua tuna dhamira ya dhati ya kulinda maeneo yetu na mali zetu za *TBC*, lakini ukisoma Ibara ya 18 utaona kabisa hatupati uwiano kati ya kosa na adhabu.

Mheshimiwa Spika, hapa niungane na Kamati, ukisoma Ibara ya 18 inasema: "Mtu yeyote atakayekutwa kwenye eneo lolote la *TBC* bila ruhusa, atatambulika kuwa amefanya kosa na adhabu yake ni faini isiyopungua milioni 10, isiyozidi milioni 20 au kifungo kisichopungua miaka miwili, kisichozidi miaka mitano." Sasa, tunatambua kabisa *TBC* ina maeneo mengi na ni ukweli usiofichika hatujafanikiwa kuweka uzio kwenye maeneo yote. Hatujafanikiwa kuweka vibao au alama kwenye maeneo yote. Sasa hapa tunaenda kuleta sintofahamu kati

ya wananchi wasio na hatia na maeneo ya *TBC*. Naona kabisa kifungu hiki hakitekelezeki na muda siyo mrefu sisi kama wawakilishi wa wananchi tutakuja hapa tuanze kufanya mabadiliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naona *it is either* tupunguze adhabu hii ili kuweka uwiano, kwa sababu bado tunataka tulinde maeneo na mali za umma. Napendekeza kama ambavyo Kamati imesema, muda huu, adhabu hii ni kubwa, faini ya shilingi milioni 10 ni kubwa kwa uwiano wa kosa. Kwa hiyo, ningeishauri Serikali ifanye tathmini kuona hii adhabu inaendana na uzito wa kosa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, jambo lingine ambalo ningependa kulisema, tunatambua mchango mkubwa unaofanywa na bodi mbalimbali hasa kuleta maendeleo na kutoa ushauri katika Taifa letu. Hapa kwenye bodi, Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi, sisi kama Taifa kanuni na sheria nyingi zinatambua umuhimu wa uzoefu wa wanachama au Wajumbe wa Bodi. Sasa kulingana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia, lakini tasnia hii ya habari haina muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, hapa nampongeza sana *DG*, Dkt. Chacha, huyu ni mwanahabari nguli wa muda mrefu, lakini wapo wachache sana. Sasa, kuweka uzoefu wa miaka 10 kwa Wajumbe wa Bodi, ninaelewa kuna vigezo vingine, lakini hili suala la uzoefu wa miaka 10 tutaenda kukosa vijana wenye weledi, ujuzi, uzoefu na wabunifu ambao wangeweza kutoa mchango wao kwenye hizi bodi.

Mheshimiwa Spika, tutaenda kuwakosa hapa, kwa sababu kigezo hiki cha uzoefu wa miaka 10 kitawaondoa vijana wengi wenye weledi, sifa na uzoefu katika kutusaidia kutoa mawazo yao na ushauri wao katika bodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna vijana wengi mtaani ni wanahabari wazuri, wana ubunifu mkubwa kusaidia tasnia ya habari. Pia, wana elimu nzuri ambao tungeweza kuwatumia kwenye hizi bodi wakatusaidia, lakini kuweka kwa kigezo cha uzoefu wa miaka 10,

kitatukosesha vijana wengi wazuri ambao wangeweza kulisaidia Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, ni vyema sana ili kuzingatia maslahi na uwezo wa vijana wetu ambao wamehitimu vyuo vikuu, lakini wapo mtaani wanafanya vizuri kwenye tasnia ya Habari, ni bora tukasema uzoefu angalau miaka mitatu, umfanye mtu kama ana ubunifu, weledi na sifa aweze kuwa Mjumbe wa Bodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natambua sana ukisoma hii Ibara ya Sita inaeleza Wajumbe wa Bodi ni nane. Kwa hiyo, kama Wajumbe wa Bodi wako nane, siyo vibaya kukawa na mchanganyiko kwa sababu ili tupate mawazo tofauti. Tunaweza tukawa na wenye uzoefu wa miaka 10 na miaka mitatu tukapata mawazo na uzoefu wao kwa pamoja ukatusaidia kupiga hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unaposema uzoefu wa miaka mitatu au 10 haimwondolei nguvu Waziri anayemteua mtu mwenye uzoefu wa miaka 10 au 20, lakini tukiiweka kwenye sheria kwamba ni lazima uzoefu wa miaka 10, tutanyima fursa vipaji, elimu na uwezo wa watu ambao hawajakidhi hiki kigezo cha miaka 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuweka mambo sawa, tunafahamu kabisa hii tasnia ya habari siyo tasnia ambayo imeanza muda mrefu, kwamba ina watu wengi wenye uzoefu hivyo. Sasa, kwa sababu tunatambua mahitaji ya soko na ulimwengu wa sasa, tunaona kabisa kigezo cha miaka 10 kitawatoa vijana na wanahabari wengi wasiokuwa na uzoefu huo wa miaka 10.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, naipongeza sana *TBC* pamoja na kuwa na mazingira magumu, imefanya kazi kubwa. Sasa hivi *TBC* usikivu ni mkubwa, mipakani tunaipata na vijijini tunaipata. Tumeona hata ziara za viongozi, matukio mengi ya Kitaifa *TBC* inajitahidi sana kutuhabarisha wananchi. Hata kwetu huko vijiji ukienda Rukwa kule ndani, Kigoma na Katavi, *TBC* inasikika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitumie nafasi hii kumpongeza *DG* na timu yake, wanafanya kazi nzuri na ninaamini kupitia sheria hii kama watapatiwa nguvu ya kifedha, tutaenda kuona mabadiliko na mageuzi makubwa sana kupitia *TBC*.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo. Mtoa Hoja, ajiandae.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi ya kuchangia Muswada huu wa Shirika letu la Habari. Kama ambavyo Mwenyekiti wetu wa Kamati na Mheshimiwa Waziri wamewasilisha hapa na kama Wabunge wenzangu walivyoanza kwa kuchangia kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais na Chama cha Mapinduzi, ni kwamba, sisi tumeshamaliza Wagombea wetu wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Zanzibar na Makamu wa Bara. Ni muhimu sana nami nikaungana nao katika kushukuru na kupongeza Chama cha Mapinduzi, tumemaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua wewe hufuatilii sana habari za wale wengine, lakini siyo mbaya nikakudodosea tu kwamba hata kukabidhiana ofisi hawajakabidhiana. Maana yake katika Bunge lako sisi tumekuwa watulivu sana hatuzodoi wengine, lakini wangekuwepo humu, ingelikuwa balaa.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naangalia Bunge lililopita, wengine mpaka wanachana makaratasi humu kwa mikwara. Sasa humu tuna Mzee Masato Stephen Wasira, *tata mura,* anasema: "Gari ni injini siyo bodi." *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo nilikuwa ninachomekea tu lakini hoja ya msingi hapa ni kuchangia Muswada wa Shirika letu la Utangazaji. Sisi hatufuatilii hayo, lakini wangekuwepo humu ungeona kazi ambayo wangekuwa wanachomekeachomekea. Dada yangu

Matiko anataka kuongea maneno hapa, lakini namwonea huruma. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee. Nawapongeza sana viongozi wote wanaosimamia shirika hili kuanzia Mheshimiwa Waziri mpaka Mzalendo Dkt. Ayub Rioba. Mimi kwa kweli naunga mkono hoja kwa sababu sheria hii itatusaidia kutambua mwendelezo wa uwepo wa Shirika la Utangazaji Tanzania, kubainisha wajibu na malengo yake, majukumu na mamlaka ya shirika, masharti ya ulinzi na usimamizi wa miundombinu ya utangazaji, na yanayofanana na hayo.

Mheshimiwa Spika, *TBC* ina umuhimu wake, ndiyo maana naiomba hapa Serikali iendelee kulisadia shirika hili. Mimi mwenyewe kupitia *TBC,* nimejifunza maneno mengi sana ya Kiswahili. Nilipokuwa nazungumza nilikuwa ninafikiri najua Kiswahili, kumbe kina utamu wake. Kiswahili ni tembo, wanaposema Kiswahili ni tembo. Maana yake, kimejaa nyama na kimenenepa. Kwa hiyo, kupitia kijana na Mwalimu Joram Mkumbi ambaye wamemwalika, nitakuibia utamu wa maneno ya Kiswahili machache ambayo kupitia shirika hili nimejifunza.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali itawekeza na sheria hii itamwezesha Waziri kutunga kanuni zinazobadilika mara kwa mara kutokana na ujana na kwa mazingira ya sasa ambapo Taifa letu lina vijana wengi, hata katika zile nchi nyingine ambazo shirika litaenda kuwekeza, basi tutakikuza Kiswahili kwa juhudi kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nimesikiliza neno 'sako kwa bako', nilishawahi kulitamka hapa, lakini lilitokea *TBC*. Likasemwa na huyu Mwalimu wanayemwalika Joram Mkumbi mpaka taasisi mbalimbali zikachukua kwenye matangazo yake ya biashara kutangaza sako kwa bako. Ukitaka kuzungumza Bungeni hapa unaambiwa useme, "Mheshimiwa Spika, ni tajamala na sudi kupata nafasi ya kuzungumza hapo." Yaani ni bahati iliyo njema kusimama mbele zako. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, wanatuambia *TBC*, wanasimulia hadithi za mzee mchekea mwezi. Yaani kijijini kwenu ukiona mzee mmoja makini, msikivu, basi unaweza kumwita mzee huyo, Mzee Mchekea Mwezi.

*TBC* wanatusihi tufanye ulumbi kila mahali, yaani tuzungumze lugha kwa ufasaha kila mahali. Tutondoe utondozi. Angalia Kiswahili kilivyo na raha, cha kutondoa utondozi, yaani kujadili kwa kina, hasa sisi Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati tunajadili, basi tuchachawize; *point of interaction*, ile kutoleana taarifa, ni kuchachawiza. Kiswahili hicho chote tunakipata kupitia *TBC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kucheka na kuterema, yaani mtu anacheka mpaka anapitiliza. Anatuhimiza tufanye mazoezi, basi anasema tukifanya mazoezi sana, tufanye mpaka tuhakikishe tunapata jasho jekejeke. Jasho ambalo linalowanisha tisheti yako ni jasho jekejeke. Haya yote tunayapata kupitia shirika letu hili, kama lisingelikuwa limewekeza na limewezeshwa, basi nisingeliweza kuyajua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukizungumza tuzungumze kwa jitimai na buka. Vijana wa *TBC* wanatusisitiza kwamba, tusizidishe matukulele katika mambo ya kazi, yaani tusizidishe mzaha mzaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili nilikuwa nachomekea tu kujua umuhimu wa shirika letu. Kama lisingekuwepo, basi maneno hayo mimi nisingeyajua. Hiyo maana yake katika Ibara ya Tano na zile kanuni ambazo Mheshimiwa Waziri ataziunda, wanasema basi zitaruhusu maudhui kuwa mazingira ya kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi pia nimesoma Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere. Sidhani kama kuna *audio* (sauti) ya Mwalimu Nyerere ambayo imehifadhiwa pale, tangu amekuwa kiongozi mpaka anang'atuka. Sijasikiliza, kwa sababu, pale chuoni kuna *library*, lakini zile sauti wamezihifadhi katika mashine za zamani, kwa hiyo, unaweka *headphone* unasikiliza.

Mheshimiwa Spika, tangu huko Mwalimu anaanza harakati za kutembea, sauti zake zote ziko pale. Kupitia sheria hii sasa, Wizara, wanaweza kuzibadilisha zile kuzipeleka kwenye *CD*, kuzipeleka

kwenye *flash*, wakagawa kwa *media* mbalimbali na vijana wetu wakaweza kuzipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo katika dunia hii ya utandawazi, wewe uko *busy* hapa, lakini *either* jioni au muda wowote ungetaka kusikia habari za msingi za nchi yetu. Ukipitia *TBC* ambayo imewekezwa vizuri, unaweza kuzisikiliza.

Mheshimiwa Spika, kwenye Kamati nilitoa mawazo, nikafikiria *TBC* iende mbali zaidi, ikibidi itengeneze habari za msingi za siku na hata kuziuza kwenye *media* nyingine. Kwa sababu, leo nikwambie, unaweza ukafungua *media* fulani ukakuta habari za siku ya leo, kuna habari zimetokea Bungeni au Mheshimiwa Spika kafanya nini Mbeya, ama Rais wetu, ama Rais wa Zanzibar, kwao siyo kipaumbele. Kwao kipaumbele ni mambo mengine katika ubinafsishaji huu wa *Private Sector*.

Mheshimiwa Spika, unafungua mitandao ya kijamii, yule mwenye *media* anakata kipande chenye *interest*. Mimi nikikosea hapa, kile kinachomhusu yeye ndiyo huwa anakikata.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukawa tumependekeza, japokuwa wataalamu na wadau walipokuja walisema jambo hilo ni gumu sana, bado ninaliweka kwenye meza ya viongozi wetu, Mawaziri na watu wa *TBC*. Ikibidi wahariri wetu wa vyombo *private* na Serikali wawe wanakubaliana kwa siku kama ni habari 10, habari tano, warushe habari zao. *Private Media* zirushe habari zao, hatuzuii, lakini kuwe na habari za Taifa, kama baadhi ya nchi nyingine zinavyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nitajua saa mbili asubuhi, ama saa saba mchana, ama saa mbili usiku nikitaka kujua nchi yangu leo imefanya nini, nitafungua habari hizo. Katika sheria ingewekwa, labda ingesaidia. Kwamba, anzisha *media* yako, rusha habari zako za Kilombero, rusha habari zako za Kichaga, za Kipare, za Kihindi, za Kimasai, lakini sharti katika *media* yako utarusha habari ya Taifa letu kwa dakika tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa wanasema ooh, ikikosewa itakuwa na adhabu, itakuwa na namna gani. Je, Mhariri wa *TBC* tutamwamini vipi?

Mheshimiwa Spika, basi wahariri nao wawe na bodi yao. Wakae wakubaliane, jioni saa mbili usiku kila *media* itarusha kwa dakika tano habari kama hizi. Kwamba, tutakuwa na habari 10 au 20 za nchi yetu. Nikijua leo kuna mafuriko sehemu, leo kuna matrekta yamegawiwa, leo kwenye kilimo tuna hiki, itatusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kwamba, hili ni jambo la msingi sana. Tukiendelea nalo katika dunia hii ya utandawazi, kila *media* inazalishwa na *interests* zake. Sisi vijana wa sasa hivi tunafungua tu *Instagram,* unakutana pale na kaka zangu akina Maulidi Kitenge wanafanya kazi nzuri, ukishashika pale, umemaliza, umeshapata habari zote, unafikiri kwamba, umemaliza jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, huku nikienda kumalizia, nasisitiza sana umuhimu wa kuliendeleza Shirika letu la Utangazaji la *TBC*. Kuliwezesha, kulipa nguvu ya kisheria, kumpa Waziri nguvu ya kubadilisha kanuni kulingana na wakati ili tuweze kuendeleza nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ni tajamala na sudi kusimama mbele zako, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, mtoa hoja ajiandae.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami kuweza kuchangia Muswada huu wa Sheria ulioletwa mbele yetu hii leo. Nami naungana na Wabunge wenzangu wote na Watanzania kwa ujumla, kwanza kabisa kuwapongeza Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wa CCM Taifa, ambao walitoa hoja mahususi ambayo imeturahisishia mambo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nampongeza sana Mbunge mwenzetu, kijana wetu, ambaye yeye alitoa hoja hiyo mahususi. Nampongeza sana, tukiwa kwenye *Party Caucus* nitaongea zaidi kuhusiana na hoja ile aliyoitoa kijana huyu na umahiri wake alioufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nampongeza Mheshimiwa Rais, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuteuliwa kuwa mgombea wa tiketi ya Chama cha Mapinduzi katika uchaguzi wa mwaka huu. Tumemteua, lakini mimi nasema tumemaliza, ndiyo Rais wetu. Hana shaka, hasa ukizingatia mambo mazuri ambayo ameendelea kuyafanya katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nampongeza sana Dkt. Emmanuel Nchimbi kwa kuchaguliwa na kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza. Tunaamini yeye ndio atakuwa Makamu wetu wa Rais wa Serikali yetu hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nampongeza Makamu Mwenyekiti, mzee wetu, mzee wa hoja, ambaye ninaamini atakwenda kutupunguzia mambo mengi ambayo atayaweka sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunajadili Muswada huu wa *TBC*, Wabunge wenzangu waliotangulia wamezungumza umuhimu wa Shirika hili la Utangazaji la Taifa *(TBC)*. Ama kwa hakika wote tunafahamu *TBC* ina umuhimu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mdogo wangu, Mheshimiwa Asenga amejifunza na anaendelea kujifunza Kiswahili kwa kupitia *TBC*. Yapo maneno mengi, lakini mimi pia nimepata neno moja ambalo kwangu ni muhimu sana. Nimejifunza kuna neno linaitwa ‘Memsapu’. Memsapu, kwa wataalamu wa Kiswahili, lina maana kubwa sana na ipo namna ya kumheshimu Memsapu. Kwa hiyo, hayo yote tumeyapata ndani ya Shirika la Utangazaji la *TBC*. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mambo mengi ya ukweli na ya uhakika yanapatikana *TBC*. Hata sehemu mbalimbali mikoani shirika letu

linasikika sana. Zipo changamoto kadhaa ambazo zimetokana na shirika hili kutokuwa na sheria. Pia, naipongeza Serikali kwa leo kuamua kuileta sheria hii Bungeni ili tuweze kuipitisha na hatimaye *TBC* iweze kupata nguvu.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu, *TBC* kwa utungaji wa sheria inaenda kupata mambo mengi. Kwanza, tutampa Mheshimiwa Waziri mamlaka ya kutunga kanuni mbalimbali ambazo zitaifanya *TBC* kujiendesha kibiashara. *TBC* itaweza kuongeza vyanzo vyake vya mapato. Ama kwa hakika, katika sheria ambazo hazihitaji kupigiwa debe sana katika Bunge lako hili, ni Sheria hii ya *TBC*. Ninaendelea kuwapongeza sana viongozi wanaoliongoza Shirika hili la *TBC* kwa sababu, waliona sasa ni wakati muafaka wa kuleta sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye Kamati tumepitia sheria hii kwa kina, na tumejadili kipengele kwa kipengele. Pamoja na umuhimu wa sheria hii, kama walivyosema wenzangu, vipo vipengele viwili ambavyo vinahitaji kuangaliwa kwa kina na kama ikiwezekana vifanyiwe marekebisho.

Mheshimiwa Spika, ukienda ile Ibara ya 18 ambayo imezungumzia makosa na adhabu zake, hasa katika kile kipengele cha mtu yeyote atakayekutwa katika katika eneo la *TBC* apewe adhabu ya shilingi milioni 10, napendekeza adhabu ishushwe, lakini na kile kipengele chenyewe kiseme, "mtu yeyote atakeyekutwa katika maeneo ya *TBC* ambayo yamezungushiwa ukuta," itakuwa imetoa maana nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, yapo maeneo ya *TBC*, kwa mfano kule Temeke, ni kama limekuwa pori. Vijana kwa wakati tofauti wamekuwa wakienda kufyeka na hatimaye kufanya mazoezi ya mpira. Kwanza wanapata afya, lakini eneo lile wanaliweka linakuwa katika hali ya usafi. Wakati mwingine wanafanya bila kupata ruhusa kutoka *TBC,* kwa hiyo, vijana hao wakikutwa pale watatakiwa wapewe adhabu kwa mujibu wa sheria iliyoletwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana kipengele hiki kifanyiwe marekebisho ili kiweze kukidhi mahitaji tuliyonayo, na namna ambavyo *TBC* kwa sasa haijaweza kuyazungushia *fence* maeneo yake yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipengele kingine ni uzoefu wa Wajumbe wa Bodi, ambapo sheria inataka wawe na uzoefu wa miaka isiyopungua 10. Tumeona hapa, ukiangalia umri wa baadhi ya Wabunge hapa na umri wa yule kijana wetu, Mbunge mwenzetu aliyetoa hoja pale, ambapo hoja yake imekuwa na msingi na mashiko sana, ni tofauti. Kwa hiyo, maana yake ni nini?

Mheshimiwa Spika, maana yake ni vijana wetu hawa wa miaka ya hivi karibuni wana uelewa na uwezo mkubwa wa kujenga hoja. Kwa hiyo, tukiweka kiwango cha uzoefu wa miaka 10, tunaenda kukosa mawazo na ubunifu wa kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, binafsi sikutegemea, tuliona watu mbalimbali wakitoa hoja, lakini hoja ambayo ilikuwa na mashiko na mvuto mkubwa katika mkutano ule ni hoja iliyotolewa na Mbunge kijana. Kwa hiyo, inaonesha ni kiasi gani hawa vijana tukiwapa nafasi, tukiondoa hii sifa ya uzoefu, basi tutakuwa tumepiga hatua kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mwanzo, sheria hii haihitaji kupigiwa debe sana. Mimi ninawaomba sana Wabunge wenzangu waungane na mawazo ya Kamati na hatimaye tuipitishe sheria hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naipongeza sana Serikali kwa kuleta Muswada ujulikanao

kama Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania ya Mwaka 2024. Shirika hili ni chombo muhimu sana cha utangazaji ambacho ni muungano wa iliyokuwa Redio Tanzania Dar es Salaam na Televisheni ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, shirika hili la umma lina jukumu kubwa la kutoa huduma ya utangazaji kwa umma kwa njia ya redio na televisheni kwa kutoa habari, taarifa, elimu na burudani. Sheria hii inatoa uhuru kwa shirika hili kuendesha shughuli zake kwa kuzingatia sheria. Sheria hii imekuja kutatua changamoto mbalimbali ambazo ziliwanyima nguvu ya kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, *TBC* ni nyenzo muhimu ya Serikali inayotumika kulinda usalama, taswira na umoja wa nchi yetu. Hivyo basi, sheria hii inakwenda kulipa shirika nguvu za kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. Hii ni pamoja na uwezo wa uendeshaji kimfumo na ukusanyaji wa mapato ambavyo kwa pamoja vitasaidia kujiendesha kwa tija.

Mheshimiwa Spika, sheria hii imekuja kwa wakati muafaka, kwani inalenga kutambua mwendelezo wa uwepo wa Shirika la Utangazaji Tanzania kwa kubainisha wajibu, malengo, majukumu na mamlaka ya shirika; kuweka masharti kuhusu ulinzi na usimamizi thabiti wa miundombinu ya utangazaji pamoja na kuainisha masuala mengine yayohusiana na hayo.

Mheshimiwa Spika, ujio wa sheria hii umetoa uhuru wa kisheria wa jinsi ya kujiendesha, kujitawala na kukabiliana na changamoto ambazo wamekumbananazo miaka mingi iliyopita. Sheria hii inaipa nguvu *TBC* kupanua wigo na kufika sehemu nyingi hapa nchini kwa kuongeza stesheni nyingi za *FM* kule ambako matangazo hayafiki. Pia, sheria inatoa fursa ya kupeleka taarifa nje ya nchi kwa kupitia masafa ya kati *(MW)* na mafupi *(SW)*. Kwa kufanya hivyo, *TBC* itatoa mchango mkubwa kueneza lugha ya Kiswahili na tamaduni za Kitanzania nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sheria hii imetoa wigo wa shirika kuwa na maktaba ya kutunza kumbukumbu ambazo zinaweza kufikiwa na

wadau mbalimbali, shirika kuandaa vipindi vyenye maudhui ya Kitanzania na kutoa fursa ya kusimamia vizuri rasilimali za shirika zikiwemo fedha. Yote haya ni mambo muhimu kwenye maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuusoma Muswada wa Shirika la Utangazaji Tanzania wa Mwaka 2024 na kwa kuzingatia maelezo ya Serikali na uchambuzi wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, naona Muswada umekuja wakati muafaka. Utaongeza tija kwenye utekelezaji wa majukumu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja ya kupitisha Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania ya Mwaka 2024.

**SPIKA:** Sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa, na Michezo, Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, aje ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA, NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kukushukuru tena kwa dhati, kwa kunipa nafasi ya kufanya majumuisho ya mjadala kuhusu Muswada wa Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania, wa Mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, jumla ya Waheshimiwa Wabunge watano wamechangia katika Muswada huu. Nami nawashukuru sana kwa mchango wao ambao una lengo la kuiboresha sheria hii itakapotungwa iwe ni sheria yenye tija na manufaa zaidi. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Singida Mashariki, Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mbunge wa Morogoro Kusini, Mheshimiwa Sylvia Sigula, Mbunge wa Viti Maalumu, Mheshimiwa Abubakari Asenga, Mbunge wa Kilombero na ndugu yangu Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, Mbunge wa Mbagala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapokea kwa dhati pongezi zote ambazo zimeelekezwa kwa Shirika la Utangazaji Tanzania. Nami naungana

nanyi kwamba wanafanya kazi kubwa, kazi ya kizalendo, kazi ya kujitolea ambayo hatuna budi sote kuitambua. Napokea pongezi zenu kwa niaba yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kuona maendeleo makubwa ambayo yamefanyika katika Shirika la Utangazaji, hasa kuhakikisha redio na televisheni inasikika maeneo yote ya Tanzania. Mpaka sasa tuna vituo vya *FM* vingi, ambavyo pia vimehakikisha matangazo yetu yanasikika. Usikivu wa *TBC* mwaka 2016 ulikuwa 54%, mwaka huu 2025 tumefikia 92%. Hayo ni mafanikio makubwa sana, kwamba, sasa usikivu wetu ni 92%, tunapambana na hiyo asilimia nane ili baada ya hapo usikivu wetu uwe 100%.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Miraji Mtaturu kwa mchango wake wa kutambua mchango mkubwa uliofanywa na *TBC*. Ninamhakikishia kwamba, kwa kupata sheria hii sasa, *TBC* itakuwa na uwezo mkubwa wa kufanya mambo mengi ambayo kabla ya hapo ilikuwa haiyafanyi kwa sababu yalikuwa hayajafafanuliwa na kuwekwa vizuri ndani ya sheria.

Mheshimiwa Spika, ile tu kwamba, sasa chombo hiki kina sheria ya Bunge, chombo cha juu kabisa cha utungaji wa sheria katika nchi yetu, inaonesha ni jinsi gani Serikali inatambua umuhimu wa chombo hiki. Sasa kinasimamiwa na sheria iliyotungwa na Bunge, ingawa pia, amri ya Rais nayo ni sheria, lakini ni sheria ndogo inayotokana na sheria ya mamlaka ya Rais, lakini sasa Bunge lenyewe limechukua nafasi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, namshukuru Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris kwa mchango wake wa kuichambua *TBC,* uwezo wake na wajibu mkubwa walionao kwa kweli tutazidi kuongeza ubunifu ndani ya *TBC*. Mpaka sasa *TBC* imeshaanzisha chaneli nyingine. Tuna *Bongo FM* na chaneli nyingine muhimu.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala ambalo limeletwa na Mheshimiwa Sylvia Sigula na Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, nalo

ni kuhusu, moja, Ibara ya 18. Serikali inapendekeza Ibara ya 18 ibaki ilivyo, nami niwatoe hofu.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 18 hailipi Shirika la *TBC* mamlaka ya *compounding of offences.* Badala yake, mtu yeyote atakayekuwa ametuhumiwa amefanya kosa, mchakato wote wa kawaida, uchambuzi wa makosa hayo kwenda kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka, utapitiwa na Dhahiri. Ikiwa mtu huyo ameingia katika eneo ambalo halina wigo, halina ulinzi, hawezi kupelekwa Mahakamani. Kwa hiyo, siyo jambo ambalo limetokea, umekutwa ndani ya eneo la *TBC*, unaambiwa basi lipa faini hii au kifungo hiki.

Mheshimiwa Spika, patakuwa na mchakato wote wa uchambuzi wa makosa kwa kuhusisha chombo ambacho kimepewa jukumu hilo, ambacho ni *National Prosecution Services* na hatimaye kwenda Mahakamani. Hata akienda Mahakamani, mtu aliyefanya jambo kwa bahati mbaya, bado ana nafasi katika utetezi wake kuomba jambo hilo lisichukuliwe kama kosa. Hata akitiwa hatiani, huwa kuna kitu tunakiita *mitigation,* unapoambiwa jieleze kwa nini Mahakama isikupe adhabu.

Mheshimiwa Spika, katika Mfumo wa Makosa ya Jinai tuna mambo mawili, kuna kutiwa hatiani na kupewa adhabu. Unaweza ukatiwa hatiani ukaachiwa bila kupewa adhabu, ukaambiwa basi tumekupa kifungo cha nje. Kwa hiyo, mara nyingi watu tutofautishe mambo mawili, kutiwa hatiani na adhabu. Ndiyo maana kabla ya kupewa adhabu, unaambiwa jitetee, kwa nini Mahakama isikupe adhabu?

Mheshimiwa Spika, ingawa mara nyingi watu wakishafika hapo, sababu kubwa wanasema, nina wazazi, wazee, wanaonitegemea mimi. Kwa hiyo, Mahakama inionee huruma, lakini kuna sababu nyingi ambazo zinaweza kutolewa. Kwa hiyo, sisi tungependekeza kwamba, kifungu hiki kibaki. Kwa nini? Maeneo hayo, kama nilivyosema, yanalindwa na Sheria ya Usalama wa Taifa, Sura ya 47 na yanalindwa na Sheria ya Sehemu na Maeneo Yanayolindwa, Sura ya 74.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo maeneo haya kuwekwa chini ya Sheria ya Usalama wa Taifa, maana yake yameonekana ni maeneo muhimu kwa usalama na ulinzi wa nchi yetu. Ingawa sasa nchi zote za Afrika zimejikomboa, kwa sababu wakati ule maeneo yale yalilindwa kwa sababu pia yalikuwa ni maeneo ambayo yalipeleka habari Afrika ya Kusini, Zimbabwe, Namibia, Angola, Msumbiji, lakini leo maeneo hayo pia yana wajibu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba suala la adhabu libaki lile lile, lakini niwahakikishie, adhabu hii itakuwa baada ya mtu kufikishwa Mahakamani na kutiwa hatiani na siyo *compounding of offences* kama ilivyo katika sheria za Maliasili kwa mfano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la uzoefu, hapa ningependa tutofautishe mambo mawili. Tutofautishe ajira na ujumbe wa bodi. Bodi kazi yake ni usimamizi na ushauri, siyo utendaji. Kwa hiyo, vijana hawa waliobobea katika akili mnemba, vijana hawa waliobobea katika teknolojia ya habari, vijana hawa waliobobea katika ubunifu, eneo lao ni katika ajira; eneo lao ni katika kuandaa vipindi; eneo lao ni katika kuboresha mifumo, lakini unapokuja kwenye bodi, unahitaji watu wa kusimamia, watu wa kushauri, na hapa unahitaji watu wenye uzoefu wa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo kweli kwamba tasnia hii ni ya muda mfupi, la hasha! Miongoni mwa watu ambao katika maisha yao ya ujana walikuwa ni Waandishi wa Habari ni pamoja na Mheshimiwa Joseph Sinde Warioba, Makamu wa Rais wa Kwanza Mstaafu na Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe mfano huo, kwa hiyo, siyo tasnia ambayo imeanza hivi karibuni. Tunao watu wengi ambao watasaidia katika suala hilo, linahitaji watu wanaoielewa nchi hii vizuri, linahitaji watu wanaoielewa dunia vizuri, linahitaji watu wenye busara na hekima. Busara na hekima kwa kiasi fulani inatokana na uzoefu, watu wamejifunza katika maisha yao kwa makosa mbalimbali yaliyofanyika ili waweze kuishauri *TBC* vizuri na waweze kusaidia watendaji wafanye kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, nami niwatie shime vijana wote kwamba sasa wana nafasi kubwa katika *TBC* kuandaa vipindi vyao, kuandaa tamthilia zao, kuleta mifumo ili iende. Nikuhakikishie, katika ajira tutahakikisha tunaajiri vijana wengi zaidi wenye taaluma hizo na siyo taaluma hizo tu, lakini vijana wengi pia wenye vipaji vingine ambavyo haviendani na elimu ya karatasi, lakini wanao ujuzi ambao shirika linauhitaji. Kwa hiyo, niungane na Kamati kwamba uzoefu ubaki miaka 10 na zaidi kwa bodi, kwa sababu bodi siyo ajira, bodi ni usimamizi na ushauri.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, namshukuru sana Mheshimiwa Abubakari Asenga, sikujua kwamba naye amekuwa ni mahiri katika Kiswahili. Naipongeza sana *TBC* kumsaidia Mheshimiwa Abubakari Asenga sasa kuwa mzungumzaji mzuri wa Kiswahili, na hiyo ndiyo moja ya kazi kubwa ambayo sasa *TBC* inakwenda kufanya kama nilivyosema na kama tutakavyosema *Inshallah* katika hotuba ya bajeti kwa kuwekeza sasa katika mitambo ya *short wave* ili kuweza kupeleka Kiswahili na utamaduni wa Kiswahili duniani kote.

Mheshimiwa Spika, hatuna uwezo wa kuomba redio za nchi nyingine au televisheni za nchi nyingine zitupe masafa, kwa hiyo, kazi yetu kubwa sasa ni kwenda huko ili kuhakikisha tunapeleka Kiswahili na utajiri wa lugha ya Kiswahili ambao leo ndugu yetu Abubakari Asenga ameuonesha na ameudhihirisha hapa. Nami nimefurahi kujua kwamba naye ni mtazamaji mkubwa wa *TBC* kwa sababu nilidhani ni mtazamaji wa *television* na redio zinazoendana na haiba na umri wake, kumbe yeye ameungana na umri wa wale wengine ambao ni wa kale wanasikiliza pia mambo ya lugha. Hili nalo ni muhimu sana na ndiyo kazi kubwa.

Mheshimiwa Spika, pia nawashukuru wale wote ambao hawakuchangia, lakini ndani ya mioyo yao, Muswada huu wanauunga mkono ikiwa ni pamoja na hawa wanaonitazama kwa macho ya bashasha mbele yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri. Tumepokea maoni

mazuri ambayo yanalenga kuboresha na kuimarisha utendaji wa shirika na tunaahidi kuendelea kuyafanyia kazi maoni hayo ili kuhakikisha kuwa Shirika la Utangazaji Tanzania linakuwa na tija kama ilivyokusudiwa. Kama wasemavyo Waswahili “kuzima kwa koleo siyo mwisho wa uhunzi”. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuruni sana, na naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania wa Mwaka 2024**

Jina Refu

*(Jina Refu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 1

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 2

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 3

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ukipiga meza tukiwa kwenye Kamati ni kwamba una jambo, kwa hiyo usipige meza.

Tuendelee, Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

Ibara ya 3

**MWENYEKITI:** Kifungu cha tatu hakina marekebisho ya Serikali, lakini nilitaka tu kuelewa Mheshimiwa Waziri, kwa sababu Shirika la Utangazaji limekuwepo, kwa hiyo kifungu kinasema, "kutaendelea kuwepo Shirika linalojulikana kama…" Shirika lilianzishwa kwa kitu kinaitwa waraka au *order* ama nini? Ndiyo tuko kwenye Kiswahili, maana sheria yetu inatungwa kwa Kiswahili leo. Inaitwaje ile iliyoanzisha?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ile amri, kwa sababu ilikuwa ni...

**MWENYEKITI:** Amri ya Rais.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, amri ya Rais, kupitia tangazo la Serikali la mwaka 2007.

**MWENYEKITI:** Sawa. Sasa kwa sababu sheria zetu zinaruhusu kwa mamlaka aliyonayo Mheshimiwa Rais kutoa ile amri, sasa hapa tunasema, kuendelea kuwepo. Mtu akiwa anajiuliza, hili shirika lilianzishwa na kitu gani? Kwa sababu hatuna mahali ambapo tunasema kwamba pengine kuna mahali lilianzishwa, sasa ndiyo mtu akatafute huko halafu ndiyo aje hapa.

Sasa kuna mawili, kwa sababu ukisoma sheria nzima, vifungu vingine vinazungumza kuhusu kuanzishwa ofisi ambazo kimsingi zipo. Kwa mfano, unazungumzia Mkurugenzi, kifungu cha sita kinasema, "kutakuwa na Bodi ya Wakurugenzi", ambayo ipo. Kifungu cha 12 kinasema, "Kutakuwa na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika ambaye atateuliwa na Mheshimiwa Rais", ambaye yupo.

Kwa hiyo, kwa sheria hii ukiitazama yote kwa ujumla, tutakuwa tunakosea mahali tukisema shirika limeanzishwa, au tuandike mahali kama sasa, sijajua Kiswahili fasaha cha *marginal note* ni nini, ili mtu awe anajua ni wapi lilianzishwa, halafu anaweza kwenda huko. Vinginevyo, inakuwa kama inaelea. Yaani hiki kifungu peke yake ndiyo kinaelea, vingine vyote vinaeleza kwa sura ambayo inaleta mambo mawili kwa wakati mmoja. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafikiana nawe kwamba ama tungeweza kusema shirika linaanzishwa na kule mwisho kabisa tungeweka zile *service provisions,* lakini hapa hapa tunaweza tukaunganisha katika Ibara hii ya tatu, fasili ya kwanza kuunganisha na kwamba shirika hili linalojulikana kama Shirika Utangazaji Tanzania *(TBC),* tutatafuta Kiswahili kizuri, lililoanzishwa kwa mujibu wa amri ya Rais namba hiyo ili pale tuweke hiyo *marginal note* ya *GN* Na.186/2007, lakini tungeweza kwenda na hiyo nyingine ya kusema linaanzishwa, halafu kule mwisho tungeweza kuwa na *service provisions.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kwa muktadha wa leo basi hapa tuweke *cross reference* na ile amri iliyokuwa imelianzisha na maana hiyo, basi linaendelea kuwepo.

**MWENYEKITI:** Sawa, sasa tunaweza kufanya jambo moja. Hiki kifungu cha tatu labda kwa sababu hapa wataalamu wapo na *AG* wakati tunaendelea na wewe kutazama hivi vingine, hebu watazame lipi litakuwa limeiweka sheria yetu iwe safi zaidi? Ile ya kuweka kule mwishoni ili vifungu vinavyosomwa vyote, visomwe vikiwa na maneno yanayofananafanana, kwa sababu vingine vyote vinaanzisha vyombo huku ambavyo tayari vipo. Ni kifungu hiki tu kidogo ndiyo kinaelea.

Kwa hiyo, wao watazame wakati tukifika mwisho tutakirejea hiki kifungu ili tuone lipi litaifanya sheria yetu iwe maridadi zaidi? Maana nilitaka kusema *neat,* tena nikakumbuka duh, tunatunga kwa Kiswahili hapa. *(Kicheko)*

Sawa, kwa hiyo, kifungu cha tatu Waheshimiwa Wabunge tutarejea kuwahoji wakiwa wameshatazama hawa ndugu zetu, lipi litaiweka sheria yetu ikae vizuri zaidi?

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kimei unajua ukisema mwongozo maana yake nikavae joho nirejee pale juu, eeeh! *(Kicheko)*

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina taarifa ndogo.

**MWENYEKITI:** Sawa karibu.

**TAARIFA**

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natatanika kidogo kwamba leo tunapitisha sheria hii kwa lugha ya Kiswahili, jana tulikuwa tunatumia Kiingereza. Sasa *version* ya Kiingereza hii haipo. Sasa sijui tunaendaendaje? Tutakuwa nyingine tunapitisha kwa Kiswahili na nyingine kwa Kiingereza au tutakuwa tunafanyaje?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kimei, tulishatunga sheria hapa, Bunge kutoa fursa kwa Bunge lenyewe kutunga sheria kwa lugha aidha ya Kiswahili au ya Kiingereza. Sheria ikitungwa kwa Kiingereza inatakiwa kutafsiriwa ndani ya miezi sita, eti Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali! Ni ndani ya miezi sita inatakiwa kutafsiriwa, vivyo hivyo na hii iliyotungwa kwa Kiswahili inapaswa kutafsiriwa ndani ya miezi sita kwenda kwenye Kiingereza.

Hivyo, hiyo ndiyo tulitunga wenyewe sheria, lakini ni hoja. Hoja yako ya msingi nimeielewa, na hii ilienda pia kwenye matumizi ya lugha kwenye vyombo vingine ambavyo vinatumia sheria tunazotunga ikiwa ni pamoja na Mahakama kutoa hukumu zake kwa lugha aidha ya Kiingereza ama ya Kiswahili. Kwa hiyo, kama tunaona kuna changamoto mahali tunaweza sisi wenyewe kuitazama sheria tuliyoitunga lakini kwa sasa Serikali iko sahihi kwa kuleta Muswada huu katika lugha ya Kiswahili.

Waheshimiwa Wabunge, Kifungu cha Tatu tutakirejea, lakini tunaendelea na vingine ili tuweze kuukomboa wakati.

Haya, tuendelee, Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

Ibara ya 4
Ibara ya 5

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 6

**MWENYEKITI:** Kifungu cha Sita kina marekebisho ya Serikali, lakini hiki kifungu ndiyo naona Wajumbe wa Kamati wamekichangia sana kuhusu uzoefu.

Mheshimiwa Waziri ametoa ufafanuzi hapa kwamba uzoefu unahitajika. Nadhani hoja ya msingi ilikuwa kwenye huu uzoefu wa zaidi ya miaka 10, ni lazima iwe miaka 10? Kwa sababu tumejaribu hapa baada ya kusikia michango mingi ya Wajumbe kuangalia sheria mbalimbali, baadhi ya sheria zinataja uzoefu wa muda gani na baadhi ya sheria hazitaji uzoefu wa muda gani?

Sasa kwa upande wa hii tasnia ya habari bado mnaona miaka 10 ni lazima iwepo au inaweza kutajwa tu uzoefu kwenye eneo, kwa hiyo haijalishi kama mtu ana uzoefu wa muda gani, lakini pengine anaweza kufanya kazi kwenye hiyo bodi?

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge kuna baadhi ya sheria zinataja muda, nyingine hazitaji muda. Kwa hiyo, labda Mheshimiwa Waziri anaweza kutupa hapo maelezo ya ziada ili tunapokitunga hiki kifungu, wote tuwe na amani kwamba Watanzania wale ambao tungetamani waingie kwenye bodi wataweza kutoa mchango wao. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa uzoefu unatofautiana kati ya sheria na sheria. Tulipendekeza miaka 10 katika eneo hili kwa sababu kama tunavyofahamu, habari ni kitu nyeti sana na hasa maudhui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kuzingatia aina ya shirika tunalolijenga na aina ya mambo yanayoisimamia; kuwa na chombo ambacho hakileti taharuki; kuwa na chombo ambacho kinaijua nchi hii imetoka wapi na inakwenda wapi; Kuwa na chombo ambacho hakiwezi kuyumbishwa na mawimbi ya dunia yasiyotabirika; kuwa na chombo ambacho kitajikita kulinda mtima wa nchi yetu *(National Ethic)*; kuwa na chombo ambacho kitaonyesha taswira nzuri ya Tanzania; tuliona ni vyema kuwa na watu wenye uzoefu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hao wapo wengi, leo hii bado tunao akina Edda Sanga ambao wana uzoefu wa zaidi ya miaka 30 katika utangazaji. Leo hii tunao watu, akina Dk. Harrison Mwakyembe ambao wanao uzoefu wa zaidi ya miaka 40 katika utangazaji na

habari, leo hii tunao mafundi mitambo wa miaka mingi ambao wamevisimamia vyombo hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tulidhani ili Menejimenti ya *TBC* iweze kuwa na bodi ambayo ina umahiri, bodi ambayo inasimamia mambo kwa kina, basi tutumie watu wenye uzoefu wa miaka 10 katika eneo hili, tukijua kwamba hawa wanakwenda kusimamia jambo muhimu sana katika Taifa letu ambalo ni tofauti na mambo mengine ambayo hayabebi jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, pamoja na kwamba leo tunapitisha sheria hii, lakini maeneo yale yanalindwa na Sheria ya Usalama wa Taifa, na maeneo yale yanalindwa na sheria nyingine. Kwa hiyo, kwa kuangalia kundi kubwa tulilonalo la watu ambao wamekuwa humu na chombo hiki ni muhimu na tupo watu ambao tunaufahamu umuhimu hata wa Redio Tanzania Dar es Salaam katika elimu, mimi na wenzangu wengi humu tulifundishwa na Mwalimu mmoja wa Kiingereza Tanzania nzima, mara moja kwa wiki, Mwalimu Mwakisombe, kwa hiyo, ni eneo ambalo lina watu wengi wenye utajiri, lakini kwa sababu ya umuhimu wake, kwa usalama na ulinzi wa nchi yetu, tulipenda basi wawe na watu ambao wanao uzoefu wa muda mrefu na wanaweza wakatoa mambo ya uzoefu wao katika kusimamia jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nje ya hayo, ni jambo ambalo mwafaka wa Bunge nao ni muhimu, lakini sisi tungependa iwe zaidi ya miaka 10 na *Inshallah* miaka ijayo naweza pia nikawa Mjumbe wa Bodi hii, miaka hiyo nikiwa nimeacha kuwa katika nafasi za kwenda mbio mbio.

**MWENYEKITI:** Hapa nilikuwa natafakari, yaani Mheshimiwa Sylvia Sigula, hawezi kuwa Mjumbe wa Bodi kweli? Nilikuwa tu natafakari. Yaani hiyo bodi lazima inataka watu wenye mambo ya ziada!

Waheshimiwa Wabunge, nadhani tumemwelewa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Haya, aah, sawa. Uzuri sheria ikishatungwa, kuna nafasi ya kufanya mabadiliko tukiona kuna changamoto mahali. Kwa hiyo, hili halituzuii kuirejea hii sheria kwa hapo baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, kifungu cha Sita pamoja na marekebisho ya Serikali kinaafikiwa?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 7

**MWENYEKITI:** Kifungu cha Saba kina marekebisho ya Serikali. Hili nalo ni la uelewa. Mheshimiwa Waziri hapa kuna kifungu kidogo kipya kimeongezwa. Kwanza hiki Kifungu cha Saba nadhani huyu mtumishi au mwajiriwa wa chama, kigezo kwamba haiwezekani sababu yake ni nini, anakuwa ana shida gani kwenye ile Bodi?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Utangazaji la Tanzania *(TBC)* ni chombo cha utangazaji za umma hii ni *public service*. Kwa hiyo, kwa kiasi kikubwa hakina budi kuonekana kwamba kinawakilisha watu wote bila kuwa na mlengo fulani wa kiitikadi ambao unaweza ukadhaniwa kuwepo. Ndiyo maana suala la mwajiriwa wa chama chochote tumeliondoa kwa sababu hiki ni chombo cha umma *(public)*. Kwa hiyo, tukaona pasiwe na mtu anayeonekana ametoka chama fulani ndani yake mwajiriwa wa chama ndilo lengo lake tu. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Kama hivyo ndivyo, najaribu kuwaza, kwa mfano mtu ameshapata kuwa Mwenyekiti wa chama fulani kwenye hii bodi yeye anaruhusiwa? Maana sio watu wote wanajua huyu ni mwanachama wa chama fulani, yeye anaruhusiwa? Yaani ameshakuwa kiongozi wa chama fulani cha siasa.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa ameacha kuwa mwanachama au kiongozi wa chama hicho, atakuwa amepata sifa ya kufikiriwa.

**MWENYEKITI:** Haya, sawa.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

**NDG. HUSSEIN ATHUMANI - KATIBU MEZANI:**

Ibara ya 8
Ibara ya 9

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 10

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 11

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 11, hakina marekebisho ya Serikali lakini kuna neno limekosewa hapo. Mheshimiwa Waziri unao ule Muswada? Kuna neno hapa limeandikwa "au jambo lolote alililotenda", inapaswa kuwa "jambo lolote alilolitenda." Kwa hiyo, 'i' inahamia mbele, na 'o' inarudi nyuma. Ni sawa?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, haya mtafanya marekebisho yanayotakiwa hapo.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 12

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15
Ibara ya 16
Ibara ya 17

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 18

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnzava, ni kwenye kifungu kipi? Kifungu cha 18? Haya, karibu Mheshimiwa Timotheo Mnzava.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza vizuri maelezo ya Mheshimiwa Waziri, lakini pia nimeisoma vizuri taarifa ya Kamati. Ukisoma Taarifa ya Kamati imeeleza vizuri sana. Changamoto ambayo ninaiona ni kwamba Kamati haijaleta *schedule,* lakini hoja ya Kamati hapa ni hoja ya msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hiki Kifungu cha 18 (a) ile (i) na (ii) inazungumza vizuri kwamba "mtu ambaye bila ruhusa au kama sio mtumishi wa shirika anakutwa katika eneo lolote linalomilikiwa na shirika bila kibali cha maandishi cha shirika."

Mheshimiwa Mwenyekiti, shirika letu lina maeneo mengi takribani nchi nzima, na yapo maeneo mengine sasa hivi bado hayajaingia hata kwenye matumizi. Kusema atakayekutwa kwenye eneo lolote linalomilikiwa na shirika atakuwa ametenda kosa, ni sawasawa, lakini

kama Kamati ilivyosema, huoni hapa uwiano wa adhabu na hili kosa ambalo limewekwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia vile vifungu vingine vidogo, kwa maana ya (b) na (c) kuna mambo mengine ambayo ni mazito kidogo ambayo kweli unaona kuna umuhimu wa kuwa na adhabu kubwa, lakini ukiangalia vizuri ni kama yapo *covered* kwenye kile Kifungu cha 17 pale juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri tu Serikali ione namna ya kupunguza hii adhabu ya faini isiyopungua milioni 10 na isiyozidi milioni 20 au hiki kifungo, kwa sababu ni kubwa sana ukilinganisha na uwiano wa kosa na uhalisia wa maeneo yenyewe ya shirika yaliyotawanyika nchi nzima ambapo mengine mpaka sasa hivi hayapo kwenye matumizi, na wananchi wetu wanaweza kuwa wanapita kufanya shughuli nyingine mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnzava, hoja yako imeeleweka. Hiyo ni pamoja na haya marekebisho ambayo Serikali imependekeza? Marekebisho ya Serikali kwa sasa, kifungu kitakuwa kinasomeka hivi, "anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni mbili na isiyozidi shilingi milioni tano, au kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka mitatu au vyote".

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho yamejitahidi, lakini hayajajibu ile hoja ya msingi ya Kamati, hasa kwa hii aya ya 18(a). Hoja ya Mheshimiwa Waziri hapa ni kwamba, kwa marekebisho haya haitakuwa kama ile *compounding offences* kwa maana kwamba atakwenda Mahakamani, atachajiwa ataendeshwa kesi, atakuhukumiwa, halafu atapewa adhabu, lakini bado kwa kosa la kukutwa kwenye eneo lolote, bado adhabu hii ni kubwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, nafikiri changamoto kubwa iliyopo ni hapa kwenye bila ruhusa. Samahani, 18 (a) "bila ruhusa au kama si mtumishi wa shirika anakutwa katika eneo lolote linalomilikiwa na shirika bila kibali cha maandishi cha shirika." Huku kukutwa ni kwa maeneo gani? Kwa sababu kuna maeneo nadhani ni yale mtu anapita njia, au mtu kasimama tu. Huku kukutwa, ni kwa aina gani?

Hiki cha pili kinasema, "au anakataa kuondoka katika eneo la shirika baada ya kutakiwa kufanya hivyo na shirika." Hiki kilivyo kwa sababu mtu tayari ameambiwa kwamba aondoke halafu akakataa hilo ni suala lingine; lakini hii sehemu ya kwanza ya (a) inaleta changamoto, kwa sababu kukutwa tu, ni kama vile hata *TBC* umekwenda unamsubiria Mheshimiwa Naibu Waziri, huna kibali cha maandishi, umekutwa kwenye eneo la *TBC*. Kwa hiyo, ile "kukutwa" sasa ndiyo hatujaelewa ni kukutwa kwa mazingira gani ili mwananchi asipate hiyo athari ambayo Wabunge wanaiona? *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme kwamba ni kweli kabisa *TBC* ina maeneo mengi na yote kwa kadri kubwa yamewekwa mabango kutangazwa mtu asiingie. Pia, yapo maeneo ya *TBC* ambayo yenyewe yamewaruhusu baadhi ya watu kufanya shughuli. Kwa mfano, hii Barabara ya Nelson Mandela, lile eneo pale, ukifika pale kuna wale machinga wameruhusiwa kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kukutwa, narudia tena, "kukutwa" tukiiondoa kwa sababu hii, siyo kama ni *offences* kukutwa katika eneo hilo, maana yake ni eneo ambalo limewekwa matangazo, usiingie katika eneo hili. Eneo hili limelindwa, na yeye bado amekutwa. Kama amekutwa huko, sitaki kwenda kwenye mambo yatakayokwenda Mahakamani iwe ni usiku au kwenye giza hakuweza kuona, pana utetesi mwingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tutayaona haya mambo ni madogo, na kwa sababu nyingine nisiweze kusema. Vyombo hivi vimehujumiwa sana katika historia ya nchi na maeneo haya. Kwa hiyo…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, tukichukua hii (a) (ii) tukaifanya ndiyo (a) imekamilika bila hiyo ya (a) (i) kwa sababu inayoleta changamoto ni huko "kukutwa" ni kweli maeneo yanahujumiwa yanafanywaje? Si ndiyo mmetaja huku chini! Kwamba mali za kitu gani, amekutwa kwenye maeneo anapohitajika na mtumishi kutaja jina, kwa sababu yote yapo huku chini.

Pale juu panaposema kwa kukutwa tu ndipo panapoleta changamoto, kwa sababu hata akikutwa amesimama tu, halafu hapa haisemi na kutakiwa kuondoka; inasema au. Kwa hiyo, hata sijaambiwa niondoke, sijaambiwa chochote, nimekutwa tu. Kifungu hicho sijui kama upo nacho hapo. Ukikisoma kinawapa changamoto.

Hiki kifungu cha (a) (ii) haina shida. Vinginevyo kama tunataka (i) ibaki hapa labda badala ya neno 'au' tuweke 'na' ili akutwe, halafu aambiwe aondoke, akatae ndiyo ije huku chini, lakini ukiweka 'au' inaleta hiyo changamoto. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni heri pawe na neno 'na' kuliko kuiondoa namba moja ya Kirumi. Kama 'na' inatibu na kuondoa wasiwasi huo, basi hilo ni jambo la tajamala na lifanyike hivyo, tuweke 'na' kuliko kuondoa kabisa namba moja.

**MWENYEKITI:** Haya. Kwanza, Mwenyekiti wa Kamati, lakini pia Mheshimiwa Mnzava, ikiwekwa neno 'na' maana yake vyote viwili lazima viwe vimekwenda pamoja. Yaani akutwe na aambiwe kwamba aondoke, halafu akakatae ndipo inakuja sasa. Kuliko au maana yake hata akikutwa tu na akikataa ni makosa mawili tofauti. Mheshimiwa Mnzava. *(Makofi)*

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru umeiweka vizuri. Ikikaa hivyo itakuwa haina shida. Labda tu utusaidie sasa kwenye uandishi, hatutakuwa na sababu ya kuwa na moja na mbili, tunaweza tukaiweka ikawa pamoja kwamba zisomeke kwa pamoja, hizi zote mbili, moja na na mbili.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tujaribu kuliboresha kwa kusema, "mtu ambaye (a) bila ruhusa au kama si mtumishi wa shirika; namba (i) anakutwa katika eneo lolote lililozuiliwa na ambalo linamilikiwa na shirika bila kibali cha maandishi cha shirika." "Lililozuiliwa na ambalo linamilikiwa." Tukiweka neno "lililozuiliwa" maana yake lipo *fenced* ili kuondoa hiyo taharuki ambayo naiona inakuja. Lililozuiliwa maana yake limekuwa *fenced.*

**MWENYEKITI:** Sawa. Kwa mfano, eneo kuna mitambo na halijawekewa fensi, akikutwa huyo mtu na akaambiwa aondoke?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mitambo yote ambayo imewekewa yote ipo *fenced.* Tukishaweka mitambo inakuwa *fenced,* na mara moja kama nilivyosema maeneo yote ya mitambo yetu kwa sababu yanalindwa pia na Sheria ya Usalama wa Taifa, yote yapo *fenced* na yanalindwa kwa watu kuonekana na yanalindwa kwa njia ambayo haionekani.

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO – MWENYEKITI WA KAMATI YA YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kamati ilijadili kwa kina sana kwenye eneo hili kwa sababu kwanza tunakubaliana na hoja ya Serikali kwamba maeneo ambayo ni ya *TBC* yanahitaji kuwa na ulinzi na hayahitaji kuwa na mwingiliano kwa sababu ni eneo ambalo lipo *sensitive* kwa ajili ya usalama wa nchi yetu. Kwa sababu anaweza akatokea mhuni tu mmoja akaenda kwenye kituo cha redio akafanya uharibifu, au akaingia kwenye eneo la utangazaji akatangaza vitu ambavyo vitatoa taharuki kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Kamati iliangalia kwa kina, tukiangalia maeneo ambayo yamemilikiwa na *TBC,* kiuhalisia mengi hayapo kwenye *fence*. Kwa hiyo, mwananchi anaweza akaenda pale sheria ikamhukumu. Ndiyo maana kwenye kipengele hiki tuliishauri sana Serikali kwamba kwenye eneo hili lazima tuangalie ili

tusije tukatunga sheria ambayo itakuja kumhukumu mwananchi kwa makosa ambayo yamewekwa na shirika lenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo mifano, pale Mbeya eneo lililopo la *TBC,* lipo wazi kiasi kwamba watu wanakwenda tu pale wanafanya shughuli zao. Sasa mtu ukimhukumu kwenye maeneo kama yale tutakuwa hatujamtendea haki kwa sababu pana uhitaji wa maeneo ambayo yamemilikiwa yaliyowekwa kwenye *fence,* na sheria itambue kwenye yale maeneo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, pale Dar es Salaam wamevamia, watu wamekuja kwenye maeneo ambayo ni ya *TBC* ambapo wanaweza wakaingia moja kwa moja mpaka kwenye eneo la redio. Lile eneo kwa kuwa kuna fensi wamefanya kosa lile, sheria inaweza ikamhukumu na mkaona kwamba mtu aliyevunja sheria amefanya makusudi. Lakini yapo maeneo ambayo mtu anaweza akapita tu, anakwenda, anashtuka sheria ile imemdhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tulipendekeza kwamba kipengele cha kwanza kifanyiwe marekebisho ya Serikali ili tulete sheria ambayo itakuwa na umuhimu wa kusaidia pande zote mbili katika Taifa letu. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa. Mheshimiwa Waziri nafikiri tufanye marekebisho kidogo kwenye kifungu hiki halafu tuone namna kinavyosoma kama kitaleta maana ile mliyokuwa mmekusudia. Kwanza, ni hapa mwanzo, mtu ambaye bila ruhusa au kibali. Hii "mtumishi", kwa sababu tayari yeye ana kibali, kwa hiyo tukishaweka neno "kibali", maana yake yeye ana kibali, kwa sababu ni mtumishi.

Kwa hiyo, tukiweka hapa "au si mtumishi wa shirika", maana yake tunakuwa *superfluous.* Mheshimiwa Asenga, inaitwaje kwa Kiswahili, maana Kamusi zimeshakuwa nyingi humu ndani. Tunakuwa kama tunajirejea wenyewe kwa sababu mtumishi ana kibali cha kuwepo hapo. Kwa hiyo, tunaweza kusema hivi, "mtu ambaye bila ruhusa au kibali cha shirika, anakutwa katika eneo lolote linalomilikiwa na shirika na anakataa kuondoka katika eneo hilo baada ya kutakiwa

kufanya hivyo," unarudi sasa huku chini, "atakuwa anatenda". Kwa sababu maneno "shirika" hapo yapo kama matatu hivi. Karibu, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata tena faida ya kupitia hili. Tunashauriwa kwamba ibaki "au" kwa sababu tukiweka "na" ina maana sasa kile cha kwanza kitakuwa siyo kosa hadi akatae kuondoka. Sisi tungependekeza pale tu-*qualify* ile, tuseme eneo lililozuiliwa kama halipo *fenced,* basi halina shida, lakini likiwa *fenced* ndiyo hiyo (i) ibaki halafu hiyo (i) badala ya "na" tuweke "au".

**MWENYEKITI:** Changamoto ya Wabunge, kuna mawili hapa nilisema tangu mwanzo, labda nirejee tena. Aidha, kile cha kwanza (i) kiondoke kabisa kisiwepo ili kibaki hiki cha pili (ii), ndicho kiwe (a) pekee yake. Kwa nini? Kwa sababu si umesema na wewe kwamba kuna maeneo ambayo hayapo *fenced,* na nyinyi mnataka yote yalindwe! Labda kama hapa sasa tunasema kwenye kifungu tunataka tulinde yaliyo *fenced* ambayo hayapo *fenced,* hana shida akikutwa. Kama hiyo ndio nia yenu, sasa ndiyo tuanze kusoma hapa kwamba, tunalinda eneo pekee lililokuwa *fenced,* ambalo haliko *fenced* wananchi waruhusiwe.

Kama hata ambalo haliko *fenced* wananchi hawaruhusiwi, maana yake hapa lazima tufanye marekebisho. Ndiyo hoja ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Swalle na Mheshimiwa Olelekaita, nimewaona, ngoja Mheshimiwa Waziri aseme kwanza. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda na kurudi kwa sababu lengo la kwanza lilikuwa ni kuwaruhusu wale ambao wana kibali cha maandishi. Wapo watu ambao shirika limewapa kibali cha maandishi kufanya shughuli zao pale kwa kujua kwamba haya maeneo katika muda mfupi hayatahitajika mpaka hapo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo ambayo hayajawa *fenced,* tumeweka matangazo kabisa mabango hata hilo la Mbeya kama unakwenda *Airport* lile eneo lote sasa inabidi tulilinde kwa sababu tumekuja kujua lile eneo limechukuliwa na *International Telecommunication Union.* Tukiliingia lile eneo au tusiweke mitambo tunayotakiwa kuweka pale tutakuwa tumeharibu na tumeingiliana na maslahi ya Zambia na Malawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, maeneo yale sasa yatawekwa mabango kwamba, eneo hili mtu asiingie kwa maana ya kulimiliki, lakini kama patakuwa na mahitaji ya Halmashauri ya Jiji la Mbeya kwa shughuli ambazo siyo za kudumu na ambazo wakiambiwa ondokeni wataondoka, na yale maeneo ambayo yapo *fenced*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tungetamani tusaidiane Bunge kwamba, maadam shaka ipo katika yale maeneo ambayo hayajawa *fenced* na ambayo bado mengine tunaruhusu watu wafanye shughuli zao kwa kibali cha maandishi kama tulivyosema hapa. Tulidhani hiyo *roman* (i) ibaki kwa sababu wapo ambao wapo kwenye maeneo yale sio *trespassers*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shirika lenyewe kwa makusudi kabisa limeruhusu, wekeni vibanda vyenu lakini siku tukilihitaji eneo hili mwondoke. Kwa hiyo, tulitaka huo uwezekano uwepo wa shirika kuweza kuwaruhusu watu kuweza kufanya shughuli zao katika maeneo hayo. Hili ambalo halipo *fenced,* basi tuliongeze lililozuiliwa na ambaye hana kibali cha maandashi halafu hiyo "au" ikabaki. Kwa sababu pia kuliondolea shirika uwezo wa kuwaruhusu watu kutumia kwa maandishi, nadhani tutakuwa tumezuia watu wengine kufanya shughuli zao katika maeneo haya ambayo kwa sasa shirika linalo kama akiba, lakini haliyahitaji katika muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bado tunapendekeza ukiona inafaa, wewe na Kamati ya Bunge tukiongeza haya maneno "lililozuiliwa" je, itakuwa bado tashwishwi ipo au itakuwa tashwishwi tumeiondoa na kuweka uelewa unaolingana?

**MWENYEKITI:** Sawa. Waheshimiwa Wabunge wawili niliwaona. Mheshimiwa Waziri, tusome sasa kwa namna ambavyo sheria huwa inasomwa. "Mtu ambaye bila ruhusa au kama si mtumishi wa shirika anakataa kuondoka katika eneo la shirika"; ili awe anakataa kuondoka si lazima awepo kwenye hilo eneo? Sasa hiki tutakisomaje peke yake tukiweka neno "au" hapo? Umeshika ule Muswada wako Mheshimiwa?

"Mtu ambaye bila ruhusa, au kama si mtumishi wa shirika anakataa kuondoka katika eneo la shirika baada ya kutakiwa kufanya hivyo na shirika," si lazima awe amekutwa ndiyo awe anakataa? Haya Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa namna ambavyo unakuwa mvumilivu kwa mambo ambayo yanaleta utata katika kipindi cha Kamati. Pia, ni jukumu la Bunge hili kulinda mali za umma yakiwemo maeneo ya umma; na ni jukumu la Wabunge hawa kulinda mali hizi za umma yakiwemo maeneo ya umma, lakini pia kuwalinda wananchi dhidi ya kuonewa na Serikali. Maana yake Serikali ina wajibu huo wa kuwalindia wananchi mali yao hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia ndiyo inayosababisha kutungwa kwa sheria hii. Tunavyozungumza sasa, maeneo haya tayari yapo kwenye migongano mbalimbali. Yapo ambayo yamevamiwa, yapo ambayo yamewekewa uzio na yapo ambayo wapangaji au watu ambao wamevamia wanakataa kutoka, hali ambayo inasababisha kuona sasa maeneo haya muhimu sana kwa Taifa na maeneo ambayo ni *classified* kwa *nature* ya hadhi yake ya kiusalama, kama ambavyo imeelezwa na Mwenyekiti wa Kamati kwamba inaweza ikahatarisha na hata ikafikia mtu akaingia hata kwenda kutangaza kwamba imetokea hivi na hivi akaleta hamaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo dhamira ya vifungu hivi 18 (a) *roman* (i) na (ii) vyote vinavyosomeka na neno lile 'au' lilikuwa na utashi wake.

**MWENYEKITI:** Twende tusomee hivi Mheshimiwa Waziri. Tusomee hiyo *roman* (ii) peke yake kuanzia kule juu yaani namna itakavyosoma kwa sababu ukiweka "au", maana yake inaweza kusomwa peke yake ikiwa imesimama. Haya tusomee.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *roman* (ii) ukiisoma peke yake itaelea, lazima uisome kuanzia hapo juu.

**MWENYEKITI:** Hapana, mimi nimesema itaelea kwa sura ipi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni mambo mawili tofauti.

**MWENYEKITI:** Ndiyo maana nasema ukishaweka neno "au" maana yake hiki cha kwanza kipo kamili na cha pili kipo kamili.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba vinatofautiana na utofauti wake ni huu. Anakutwa katika eneo lolote linalomilikiwa na shirika…

**MWENYEKITI:** Tusomee ya pili ndiyo tuna shida nayo kwa sababu tuna lengo fulani tunataka kufika.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, "anakataa kuondoka katika eneo la shirika baada ya kutakiwa kufanya hivyo na shirika." Anakataa kuondoka huyu…

**MWENYEKITI:** Anzia mwanzo kwa sababu neno "anakutwa" linahusika na cha kwanza pekee. Cha pili hakina neno "anakutwa" Mheshimiwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nilisema, maudhui ya *roman* (i) na (ii) ni tofauti.

**MWENYEKITI:** Tupo kutunga sheria, tusomee namna itakavyosomeka Mheshimiwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu ni kwamba ibaki kama ilivyoandikwa hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Olelekaita…

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu vina maudhui tofauti.

**MWENYEKITI:** Sasa kama kinaelea, ukasema kina maudhui tofauti…

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, havielei kwa tafsiri, kwa sababu haikufika hapa hivi hivi. Imepitia kwenye Kamati…

**MWENYEKITI:** Ndiyo tupo kwenye kutunga sasa hivi. Wewe umesema una pendekezo. Pendekezo lako si umesema Mheshimiwa!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu, maudhui ya "kukutwa katika eneo lolote" na maudhui ya "kukataa kuondoka" ni mawili tofauti. Kwa hiyo, au …

**MWENYEKITI:** Nimesema hivi Mheshimiwa, tusomee. Umekataa kusoma ndiyo maana hunielewi. Ngoja mimi nikusomee. Kitasomeka hivi, "mtu ambaye bila ruhusa au kama si mtumishi wa shirika anakataa kuondoka katika eneo la…" ndiyo kitakavyosomeka.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nasema mimi siji na kitu kipya, najaribu kusimamia kwenye kilichoandikwa. "Mtu ambaye bila ruhusa au kama si mtumishi wa shirika; (i) anakutwa katika eneo lolote linalomilikiwa na shirika bila kibali cha maandishi cha Shirika; au anakataa kuondoka…" ni vitu viwili tofauti, na maneno haya hayana shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu, hayaingiliani, hayaleti ugomvi, na yanatengeneza sheria nzuri tu.

**MWENYEKITI:** Mpigakura wa Mbeya Mjini, maana ndiyo mfano uliotumika hapa; akijikuta yupo kwenye hilo eneo ambalo ni la *ITU* ambalo haliko *fenced,* anatenda kosa? Maana yake hii hapa ina-*establish* kosa la *strict liability*.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *no*. Tunasema *it is a procedural,* yaani haifiki tu kwenda ku-*establish strict liability* kwa sababu si ni kosa? Si ni lazima liwe *established?* Ndiyo maana Waziri alijibu…

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa umeeleweka. Mheshimiwa Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi, na unajua shida ipo hapa, ukisoma *marginal note* inasema ni kuingia kwenye eneo. Hata ukiweka mguu tu, ndiyo *intention,* lakini sasa anavyotuelezea Mheshimiwa Waziri, kama nampata sawasawa. Ni mtu anayeingia na kufanya shughuli fulani bila kibali. Maana yake siyo kuingia tu, haiwahusu wale wanaopita tu, na kupita kama njia. Aingie na afanye shughuli, halafu hana kibali ndiyo *intention,* si ndiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama ndivyo, basi hii *number one* anayosema Mheshimiwa Spika haina haja ya kuwepo kwa sababu kwanza mme-*qualify* kwa kuwapa nafuu tena kwamba ukutwe na uambiwe uondoke ndiyo kosa lije. Kwa hiyo, ukikataa kuondoka ndiyo

kosa litakuja, ndiyo maana mkaweka hii ya pili. Sasa kama ndivyo, kwa nini tusiseme tu moja kwa moja kwamba ukikutwa kwenye eneo linalomilikiwa unafanya shughuli fulani na ukaambiwa uondoke na hujaondoka, halafu ndiyo kosa sasa liwe *clear*? *Otherwise* hii ni *confusion*, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya nafikiri Mheshimiwa Olelekaita hapo ulipozungumza, hoja ya Mheshimiwa Simbachawene ni kwamba, hizi hoja zinajitegemea kwa maana ya kwamba kuna anayekutwa, yule naye ni kosa lake, na kuna anayekataa. Sasa huyu anayekataa sijajua yeye atakuwa hajakutwa, ila anakataa. Kwa hiyo, kwa sababu ni mambo mawili tofauti, sasa yaani hapo kidogo ndiyo tunapata mchanganyiko wa mambo.

Mheshimiwa Swalle.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi niseme kwamba naungana sana na hoja ya Mheshimiwa Mnzava pamoja na Wajumbe wa Kamati ambapo pia umetuongoza vizuri sana. Nitakwenda kwa mfano, pengine kidogo Mheshimiwa Waziri na timu yake wanaweza wakatuelewa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hii ambayo Wabunge tunaisema hapa kwamba mtu akikutwa tu kwenye eneo aonekane kuwa na kosa la kwenda kushtakiwa, imeshatokea mara kadhaa kule Mkoani Njombe. Pale Njombe kuna uwanja wa ndege ambao upo katikati ya makazi ya watu, hauna *fence* na kuna mahali kuna nyasi ndefu ambazo watu na wanyama wanaweza wakaingia muda wowote. Kumeshakuwa na shida mara kadhaa watu bila kujua, usiku kwa mfano, mtu amepanda pikipiki anaamua kushuka kwa sababu upande wa pili kuna mitaa ya watu anaamua kupita pale, bila kujua kama kuna katazo la kupita tu pale, wamejikuta watu wakienda Mahakamani, na kulipa faini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu Bunge limepata hii nafasi muhimu ya kutunga sheria nyingine ambayo tayari imeshakuwa na shida maeneo mengine, mwongozo wako ni muhimu sana

kwamba, tuwasaidie watu ambao watafika kwenye eneo wakiwa hawajui, wakipewa nafasi ya kujulishwa wakakataa, ndipo liwe kosa la wao kushtakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono hoja ya Wabunge kwamba ni lazima watu wapewe nafasi ya kujulishwa kwa sababu sisi kama Serikali maeneo yetu bado hatujayapa ulinzi wa kutosha kufanya watu wafanye makosa kwa kujua, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, samahani, kulikuwa na Mbunge mwingine amesimama pale. Samahani Mheshimiwa Waziri, ngoja amalize yeye halafu nikurejee. Mheshimiwa Francis Mtinga.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi sio mwanasheria, lakini hapa kuna wanasheria na wananchi. Sasa mimi hapa nimesimama kama mwananchi ambaye anapambana na sheria ambayo imeshatungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo kwenye suala la kukutwa na kukataa kuondoka ninavyodhani mimi, Serikali ilikusudia kuna watu tayari ilishawapa maeneo na inawaambia watoke. Sasa wamegoma, hivyo wanataka waweke sheria. Kwa hiyo, wangeweka tu vizuri vifungu hivyo vitofautiane ili kusiwe na tatizo kwamba kuna mtu alipewa kwa nia njema, kwa barua kabisa pengine fanya shughuli, kama wale Machinga waliopewa pale Dar es Salaam, lakini Serikali inapotaka kutumia eneo lile na kuwaambia watoke, inakuwa shida, hawataki kutoka. Sasa wanataka kuweka sheria kudhibiti hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo kingewekwa tu kifungu tofauti ili likae wazi lijulikane kwamba ukipangishwa, kuna siku ukiambiwa toka ukikataa kutoka kuna sheria itakufuata nyuma. Hii nadhani vikiwekwa hivyo vifungu vikatofautishwa sisi ambao ni wananchi sio wanasheria, tuna taaluma nyingine, tutaelewa vizuri moja kwa moja kuliko hivyo ambavyo mnataka kuvibebanisha na vinaleta mtafaruku kati yenu ninyi wanasheria mliobobea, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusikiliza maelezo yote haya na ulivyotuelekeza, suala la kukutwa ni muhimu sana. Kuna jambo nilisita kulisema, nitalisema sasa na watu wa umri mkubwa zaidi ya mimi watalielewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kipindi fulani nchi yetu hii ilikuwa kila taarifa ya habari ya saa mbili inaingiliwa na matangazo yanavurugwa. Hata hivyo, tumshukuru Mwenyezi Mungu Rahimu, nchi yetu ni ya amani. Mtu anaweza kabisa akaenda *studio* akafanya mambo yasiyoakisi utamaduni wetu. Kwa hiyo, suala la kukutwa bado ni muhimu, kwamba umekutwa. Hapa siyo mahali tena pa kuendelea kudadavua mambo ambayo wengi wanayaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hofu yangu ni kwamba, tukiondoa kabisa "kukutwa", tutaruhusu watu, huyu ambaye atajikuta ameingia *studio* na akatuletea matatizo. Nimetoa mfano huo, wale watu wa umri wa Mheshimiwa Mzee Mkuchika wanajua, na ilichukua jitihada kubwa baadaye kuja kujua ni nani alikuwa anafanya mambo hayo, na baadaye ikaonekana ni hizi *antenna* za Mlima Image.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa ningependekeza ama tuseme, "bila ruhusa, na si mtumishi wa shirika anakutwa na anakataa kuondoka." ili tusonge mbele. "Anakutwa na anakataa kuondoka", kama hilo linatibu, ingawa mimi linanipa jakamoyo, nipo tayari kwenda nalo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tutakuwa na kifungu kimoja?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Sawa.

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimefuatilia kwa makini sana mjadala wa kipengele hiki. Jambo la msingi ambalo inabidi tuzingatie hapa, sheria nyingi za taasisi ambazo zina *vital installations* lina kosa kama hili la kukutwa kwa sababu tu *trespassing* usipoidhibiti na hizi *vital installation* zikaingiliwa, inaleta madhara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa tuna-*establish* makosa mawili tofauti. Kosa la kwanza ni kukutwa bila kibali katika maeneo yanayomilikiwa na *TBC,* na *TBC* ni miongoni mwa taasisi ambazo zina *vital installation*…

**MWENYEKITI:** Sawa, la pili ili twende vizuri…

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kosa la pili ni yule ambaye amekutwa kwenye eneo hilo na hataki kuondoka, hiyo ni kosa lingine tofauti. Kwa hiyo, *trespassing* na ku-*deny* kuondoka baada ya kutakiwa kufanya hivyo, yote hayo ni makosa mawili tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kama alivyosema vizuri mtoa hoja, hapa *issue* inayotutia wasiwasi sisi ni zile adhabu. Adhabu hizi haziwezi kutokea mpaka utiwe hatiani.

**MWENYEKITI:** Sawa, lile kosa la pili turejee pale pale kwanza. Lile kosa la pili. La kwanza ni *trespassing*; la pili, ni *refusal to leave*. Kwa hiyo, huyu sio *trespasser* ila unataka aondoke. Nielewe vizuri hoja yako. Yaani huyu kwa sababu hapa, si tunasema makosa ni mawili, yaani kuna mtu ambaye amefanya *trespassing,* tutumie kabisa Kiingereza, huyu wa pili hajafanya *trespassing* lakini wewe unataka aondoke.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Sasa hili kosa hapa tukiunganisha linafanana kwa sababu tumeyaweka yote kwa pamoja. Vinginevyo tuweke vifungu viwili tofauti ili tujue huyu *trespasser* tunamzungumzia kwa sura hii. Huyu

ambaye ameingia, ana kibali na kila kitu, halafu naye kafanya kosa, kwa nini? Kwa sababu tangu huku mwanzo unazungumzia bila ruhusa, na unazungumzia bila kibali. Yeye anaingiaje pale kama sio *trespasser?* Maana yake unayetaka kumwondoa ni *trespasser*.

Hoja ya Bunge ni kwamba huyu unayetaka wewe kumwondoa kwa kifungu hiki (a) ni *trespasser,* ndiyo kosa lake kubwa, unataka aondoke. Sasa sisi ndiyo tunasema, huyu *trespasser* tumekubali, lakini awe ni *trespasser* kwa mazingira aliyopo, ni *trespasser* na akatae kuondoka, ni *trespasser* aondoke.

Sasa wewe unasema tuyatenganishe *which is also okay*. Tuyatenganishe *trespasser* na huyu ambaye ana kibali, lakini yupo ila wewe kwa muda huu humtaki awepo, aondoke. Hiyo ni sawa?

Haya, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa upo sahihi kabisa, kabisa, kabisa. Kwa usahihi huo huhitaji kuongeza kitu hapa kwa sababu unachokizungumzia, ukisoma vizuri haya maandishi, maudhui yake ni kwamba, kuna mtu, maana yake hata hii *roman* (i) inasema anakutwa katika eneo lolote linalomilikiwa na shirika bila kibali.

**MWENYEKITI:** Sawa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kibali, huyu sio *trespasser*.

**MWENYEKITI:** Sawa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kibali cha maandishi cha Shirika.

**MWENYEKITI:** Endelea.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu *roman* (ii) anasema, anakataa kuondoka…

**MWENYEKITI:** Au!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, au anakataa kuondoka katika…

**MWENYEKITI:** Kule juu, *opening* imeanza, "na bila ruhusa". Aliingiaje hapa kama siyo *trespasser?* Ndiyo maana tunasema ukiki-*dump* hapa kinakosewa kifungu, kwa sababu *trespasser* huwezi kumwita *trespasser* kwa sababu tu, yaani wewe umeamua kumwita, hapana. Ni mtu ambaye hana kibali, hana ruhusa, ndiyo anaitwa *trespasser*.

Ukimchanganya hapa, angalia hapo kwenye nakala yako, inasema; "mtu ambaye: (a) bila ruhusa", ndiyo *opening*. Sasa "ambaye bila ruhusa", maana yake ni *trespasser*. Kwa hiyo, hakuna ambaye kaingia ana kibali, halafu bado unamwambia tena bila ruhusa. Ile *opening,* ya pale juu inayafanya haya makosa yaingie yote yakiwa pamoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi tu-*establish* kingine, lakini hii hapa ibaki hivi hivi lakini tu-*establish* kingine cha *trespasser.*

**MWENYEKITI:** Haiwezi kubaki hivi kwa sababu tunapotunga sheria ikibaki hivi, maana yake hapo unaanzisha kosa la mtu ambaye haja-*trespass,* lakini wakati huo humtaki. Yaani, kwa mfano, humu Bungeni, wote humu si tuko humu sawa sawa kabisa, lakini si kuna mtu anaweza akafanya fujo nikamwambia atoke? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *yes*.

**MWENYEKITI:** Si amefanya fujo, nikamwambia afanye nini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, atoke.

**MWENYEKITI:** Japo alikuwa na kibali cha kuwa humu ndani. Ni tofauti na kwa mfano akiingia mtu sasa hivi ambaye sio Mbunge, ambaye haruhusiwi na hatujatengua kanuni. Kwa hiyo, hayo ni makosa mawili tofauti. Mbunge ana kibali cha kuwa humu ndani, mimi nimemwambia toka nje, lakini yuko anayeingia humu ambaye sio Mbunge. Sasa kifungu hiki kinakusudia anayeingia humu ndani ambaye sio Mbunge. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakubaliana nawe kama nilivyosema kwenye msingi wetu...

**MWENYEKITI:** Wewe kama unakubaliana nami, nadhani tumeelewana. Ukieleza mengine ni kama unanichanganya hivi...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wetu ni kwamba makosa haya ni mawili tofauti, ila kuna lingine halionekani sawasawa...

**MWENYEKITI:** Sawa. Ndiyo hilo sasa, kama ndiyo nia yetu, hapa haliwezi kuwekwa pamoja na la bila ruhusa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi tu-*establish* ya *trespass* na tu-*establish* na ya huyu aliyekataa kuondoka.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nollo. *(Makofi)*

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami siyo mwanasheria, ila tu natumia sasa *logic* ya kuona sheria inataka kwenda kupambana na kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona maeneo matatu. Kwanza, inaongelea habari ya mpitanjia *(trespasser)*, inaongea habari ya shughuli ya kiuchumi, na tatu inaongea uvamizi wa ofisi, kama nimemsikiliza vizuri Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *trespasser, obvious* mimi nitaondoka. Nang'angania kufanya nini humu ndani, mimi mpitanjia? Ndiyo napita na nikiambiwa kuondoka, naondoka, si mpitanjia? Ukija kwenye shughuli za kiuchumi, natakiwa niondoke kwenye eneo hilo, nisifanye shughuli ya kiuchumi; lakini mvamizi wa ofisi, huyu naye ndio anatakiwa sasa aondolewe, atoke; anang'ang'ania kwenye maeneo hata kama kwenye mitambo ya kurushia au ndani ya ofisi ile!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *logic* ya kwamba amekutwa, ameng'ang'ania, inakuwa katika *context* tatu tofauti. Nadhani *clarity* yake ikae vizuri, kwamba, sasa huyu mpitanjia anang'ang'ania, lakini amekutwa. Ukienda kule kwenye ofisi au kwenye mitambo nako, amekutwa anang'angania. Kwa hiyo, hapa kuna *confusion* kubwa, nami naiona katika maeneo matatu. Mpitanjia, shughuli katika eneo la *TBC* na vilevile katika uvamizi wa Ofisi za *TBC* na mitambo yake, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya. Nadhani, Mheshimiwa Olelekaita ulisimama tena.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama na mimi...

**MWENYEKITI:** Jamani, ninyi wawili mtakuwa wa mwisho sasa kwenye hoja hii. Au nani mwingine, na Mheshimiwa Kamonga! Haya, Mheshimiwa Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kuna *scenario* nyingine ambayo naanza kuiona hapa. Unajua *trespass* siyo lazima iwe ya maandishi ndiyo umapate *defence! By the way*, tusichukulie hii *generally*, unaweza ukawa sio *trespass,* kwa sababu umepata *invitation* ambayo siyo *necessarily* ya maandishi. *That is one concept,* lakini hii hapa mme-*qualify* kwamba ili isiwe *trespass* lazima iwe maandishi ambayo kawaida siyo kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukapata *oral invitation,* umepata ruhusa ya yule mtu bila hata maandishi, hakuna *trespass; that is one scenario*. Hata hivyo, lingine ambalo ndiyo naona sasa hii *logic* ya mtu ameingia bila ruhusa hiyo ya maandishi na akafanya shughuli, ndiyo hiyo *roman one;* lakini kuna mtu anaambiwa aondoke na akakataa. Kwa hiyo, *assumption* ni kwamba, huyu mtu akifunguliwa *charge*, atakuwa na makosa mawili. Kwanza, kukutwa bila kibali na ameambiwa aondoke akakataa. Kwa hiyo, maana yake kutakuwa na *offence* mbili kwenye kumshtaki huyo mtu mmoja. *That is one scenario*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *scenario* nyingine, kuna mtu kaingia ana ruhusa, tena ya maandishi, lakini akaambiwa aondoke na akagoma. Maana yake huyu atashtakiwa kwa *refusal* ya kukataa kuondoka. Kama ndivyo, swali lingine tu, sasa wale wapitanjia si mtawashtaki pia hapo?

**MWENYEKITI:** Haya, umeeleweka Mheshimiwa. Halafu hili neno, "kufanya shughuli," nadhani watu mmejiongeza katika michango. Kwenye kifungu hiki, yaani kwamba umeingia halafu ukafanya shughuli haipo kwenye hiki kifungu. Yaani ni wewe umekutwa umesimama unakula *Big G,* hilo ni suala lako. Siyo lazima ufanye shughuli, yaani umekutwa. Mheshimiwa Kamonga, tutamalizia na Mheshimiwa Mnzava.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Hii *trespass* ni kosa la jinai, lakini vilevile linaingia kwenye *civil,* kwenye *tort*, kwa sababu mtu akishaingia pale

wakati hana kibali, tayari amesha-*trespass*. Anaweza akashtakiwa kwa jinai na anaweza akashtakiwa kwa madai, kule kwenye *tort*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *tort* ile aliyoeleza Mheshimiwa Swalle, wakati mwingine mtu ameingia aidha mmiliki wa pale, hakuchukua tahadhari yoyote, ama ya kuweka uzio au bango kwamba mtu haruhusiwi kuingia. Kwa hiyo, anaweza akajikuta yuko ndani ya eneo na akawa tayari ametenda kosa la jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunavyosema kwamba mtu ambaye ameingia bila ruhusa, tayari ni *trespass* na unasema siyo mtumishi wa shirika. Sasa ni kama hili neno "siyo mtumishi" wa shirika, halikuwa na ulazima wa kuwekwa pale. Ile tu ya kusema, mtu ambaye hana ruhusa, tayari ilikuwa inajitosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu unavyosema kwamba neno "au" ndiyo linaloleta utata, kwa hiyo, maana yake itakuwa "mtu ambaye bila ruhusa" ilikuwa tayari inajitosheleza. Maana yake kama ni mtumishi, tayari anayo ruhusa, itakuwa ni kujirudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naona ulikuwa unatuongoza sawasawa na ili kuepusha utata wa tafsiri inavyotokea, kwa sababu tayari kuna sheria nyingine ambazo zinasimamia na kulinda eneo la mtu, na tayari *trespass* ipo kwenye sheria nyingine ukiacha hii ya *TBC* na tayari ni jinai na lina utaratibu wake ambao unashughulikiwa wakati wote na siyo *TBC* tu wanayo maeneo, bali pia wapo watu wengine, kwa hiyo, hapa ili kuondoa utata nadhani ulikuwa unatuongoza kwa usahihi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Jamani mniwie radhi, nilikuwa nimemsahau Mheshimiwa Ramadhan, alikuwa amesimama pia. Mheshimiwa Mnzava, kisha Mheshimiwa Ramadhan. Mheshimiwa Timotheo Mnzava.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi yangu ulishamaliza. Nilikuwa na mawili; moja, tunatunga sheria. Kwanza, isitafsirike kwamba labda Bunge tuna nia ya kuruhusu maeneo ya

umma yaharibiwe au yatumiwe vinginevyo, siyo dhamira yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, niliona kama mjadala unahamishwa kidogo, na umelisema vizuri lile la shughuli, maana halipo kwenye maandishi ya sheria, lakini limesemwa na watu wakawa wanalichukua kana kwamba lipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu, hii hofu yote ya kusimamia maeneo yasiharibiwe au yasitumike vibaya au vinginevyo, pia iko *covered* kwenye sheria hii. Ukisoma kifungu cha 17, lakini kutoka hapo nenda soma kifungu cha 18, kisha angalia (c) na (d), bado hizi hofu ambazo Mheshimiwa Waziri anazisema kuna maeneo bado zinafanyiwa kazi. Nadhani ule mwongozo ambao ulikuwa umeutoa, ulikuwa umekaa vizuri zaidi. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ramadhan.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nimefuatilia mjadala na hoja zote kutoka Serikalini pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzangu walivyokuwa wanataka kusaidia ili tukwamuke kwenye jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoona kinatupa utata ni jinsi kifungu kilivyoandikwa. Ni lugha iliyotumika kukiandika. Nimeelewa vizuri *intention* ya Serikali na nimeelewa vizuri hoja yako unavyotaka kikae. Kwa maoni yangu, kama kingeandikwa namba 18 imeandikwa, "mtu ambaye" kama pasingekuwa na hii "(a) bila ruhusa au kama siyo mtumishi wa Serikali", pasingekuwa na hii sentensi kwa mfano, imeandikwa "mtu ambaye *(a) unlawful enter,"* ameingia *unlawfully*. Kwa hiyo, *unlawfully* inaweza kuwa bila ya kibali au sio mtumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu kosa lake, *count* yake ni ku-*enter* tu. Ukikutwa tu ume-*enter, offence* yako inafanyika hapo. Kuingia tu kwanza ni kosa. (a) tutakuandikia *count* ya kwanza, umeingia ndani hapa, tumekukuta; ya pili, *roman two* sasa, umekutwa ndani halafu

umeambiwa utoke hautaki. Kwa hiyo, hii ni *different offence*. *Very different*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, umeingia *lawfully* au kwa hiyo, kukiandika, tunaweza tukakiandika cha pili. Kwa hoja yako, huyu ame-*enter lawfully,* lakini ame-*refuse* kutoka. Kwa hiyo, hii ni *count* ya pili inayokuwa *separated* na *count* ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Mnzava alivyoinuka alisema hakuna uwiano wa adhabu kwenye makosa haya. Yote yamewekewa adhabu moja ya shilingi 10,000,000 na isiyozidi shilingi 20,000,000 wakati haya ni makosa mawili tofauti. Ku-*enter* tu ni kosa lake na kukutwa iwe haramu au halali, lakini umeambiwa utoke halafu hautaki, ni kosa lake. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, wakati unazungumzia ile hoja ya kusema kuna maeneo yako *fenced*, ulitumia neno gani? Sasa nafikiri hofu yetu inakuja pale kwenye bango kwa sababu mabango huwa hayawekwi kuzunguka uwanja. Huwa kuna bango, hata maeneo mengine ya jeshi na yenyewe kuna changamoto tu. Yaani kuna bango liko upande huu, mtu anaweza kuingilia upande mwingine.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani hoja zenu sasa hapa tukubaliane, hii *opening* ya (a) ile kubwa itaondoka. Tutengeneze hii *roman* ndogo ya kwanza ikae (a) halafu hii *roman* ya pili ikae (b) ili yawe ni makosa mawili tofauti, ili lile kosa la kwanza tuliweke kwa sura ambayo hofu ya Waheshimiwa Wabunge inaondoka, wakati huo huo kosa la pili pia liwepo ili mtu asione kama yeye hayumo kwenye lile kosa la kwanza. Si ndiyo!

Kwa hiyo, hapa mwanzoni pia yale maneno ya "bila ruhusa" yaani ile *opening statement* tuiondoe ili tuanze moja kwa moja. Kwanza, hili la jumla sasa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, una kifungu tayari?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo, nilikuwa nataka kupendekeza.

**MWENYEKITI:** Haya, pendekeza.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 18, nilikuwa napendekeza sasa kisomeke, "Mtu ambaye (a) bila ruhusa au kibali cha shirika anakutwa katika eneo lolote lililozuiliwa na linalomilikiwa na shirika"; tunaweka ile *semi colon*, koma (b) anakataa kuondoka katika eneo la shirika baada ya kutakiwa kufanya hivyo na shirika". *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, neno "maandishi", umeondoa kwenye lile la kwanza ulipotusomea. Hebu tusomee ili niwe na uhakika kinasomekaje? Ile (a), tusomee kwanza.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, "Mtu ambaye (a) bila ruhusa au kibali cha shirika anakutwa katika eneo lolote lililozuiliwa na linalomilikiwa na shirika" (b) anakataa kuondoka katika eneo la shirika baada ya kutakiwa kufanya hivyo na shirika".

**MWENYEKITI:** Hapo kwenye kibali cha shirika, sina hakika mtu atatafsiriwa kwamba ni shirika, au tuseme tu neno "kibali" badala ya kibali cha shirika?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza kuondoa shirika.

**MWENYEKITI:** Eeh, sasa nawaza, kwa mfano mtu anayeruhusiwa kuingia hapa Bungeni, anapewa kile kitambulisho, siyo! Ndiyo ameruhusiwa. Sasa kulikuwa na hoja iliyoletwa pale, kwa mfano, mimi naenda kumtembelea Ryoba, anahitaji kunipa mimi kibali cha kumtembelea au! Nimetoa tu mfano, yaani mimi kama rafiki yake wa mahali, nitakuwa na kibali cha aina gani? Si tumepigiana simu akaniambia, bwana sasa hivi nataka kwenda kula, njoo tunywe chai. Kile kitahesabika kuwa ni kibali, ama!

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kupita getini mpaka pawe na taarifa na amearifiwa.

**MWENYEKITI:** Tunarudi kule! Siyo ile, ofisi tu. Nimetoa mfano Mheshimiwa. Kule kwenye maeneo ya *TBC* sasa, si ndiyo tunayoyatengenezea kosa hapa. Tunayoyatengenezea kosa ni maeneo ya *TBC*. Kwa hiyo, siyo lazima kule kuwe na ofisi, lakini sasa pale inakuwa yaani mtu, sijui nieleze kwa sura gani?

Yaani kuingia, kwa mfano hata Bunge, si lina maeneo huko nje pia, lakini anayeenda kwenye hilo eneo hapewi kibali. Anapewa kibali anayeingia humu? Bali hili kosa tunaloanzisha, tunaanzisha kwenye eneo la *TBC*, kukutwa huko. Kwa hiyo, je, tuweke kibali cha shirika au tuweke tu neno kibali? Ndiyo hoja.

Tuongeze neno "kibali cha shirika" au tuweke tu "kibali"? Yaani kwamba, anaweza kuwa ni Mwajiriwa wa *TBC,* kaalika mtu, au! Semeni ninyi, kwa sababu tukishasema "kibali cha shirika", maana yake ndiyo, haina shida? Haya.

Waheshimiwa Wabunge, mmesikia namna vifungu hivi vilivyopendekezwa kusomwa? Nadhani yakianzishwa makosa mawili tofauti itakuwa imekaa sawa. Si ndiyo! Sawa.

Ile (b) itakuwa inakosa neno "kuingia," itakuwa iko sawa? Hebu tusomee ile (b) tuone inakaaje peke yake bila kuweka neno kukutwa ama na yenyewe iwe ni kukutwa na kukataa?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, (b) inasema, anakataa kuondoka katika eneo la shirika baada ya kutakiwa kufanya hivyo na shirika.

**MWENYEKITI:** Pale kuna haja ya kukutwa au tuache hivi hivi? Kwamba, huyu ni yule sasa ambaye ana kibali, lakini sasa anatakiwa kuondoka. Tuliache hivyo, si ndiyo! Sawa. Waheshimiwa Wabunge, nadhani hapo tumeelewana vizuri. Haya, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Sasa lingine ambalo twende pale kwenye (c) ya sasa ambayo nadhani itakuwa (d) sasa baada ya kubadilisha zile namba. Mheshimiwa Waziri, "anaharibu au bila ruhusa anaingilia". Hii "kuingilia" ilikuwa na kusudi ya lile neno *interference?*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUN, SANAA NA MICHEZO:** *Interference.*

**MWENYEKITI:** Hakuna Kiswahili kingine, ni kuingilia tu? Kwa sababu ukisoma kwa Kiswahili, "anaingilia mali yoyote ya shirika", yaani ni kama vile Kiswahili hakijakaa vizuri. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo imekuwa hofu yangu kubwa sana, tunafubaza Kiswahili kwa kulifanya kila neno la Kiswahili kuwa na maana ya kimuktadha baada ya maana sisi. Kwa hiyo, sisi tumelipa hili maana sisisi na siyo maana ya kimuktadha. Kwa hiyo, likibaki hivi kwa maana ya sisisi, halina ukakasi, lakini tukilipa tafsiri ya muktadha...

**MWENYEKITI:** Hapana. Maana yako hiyo hiyo, mtu akisema, anaharibu au bila ruhusa anaingilia mali yoyote, si unaona hata mimi kwenye tafsiri imebidi niseme kwa Kiingereza. Yaani, hii kweli kazi! Kuingilia mali ni kufanyaje yaani jamani? Ngoja, hebu tuone. Mheshimiwa Kisau.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kama ni Kiingereza, *interference* tayari ni kosa. Huwezi kuwa na *interference* ambayo ina ruhusa na ambayo haina ruhusa. Kwa hiyo, tuamue. Najua Kiswahili ni matatizo makubwa sana, lakini *interference* ni *illegal in all*.

**MWENYEKITI:** Hapana, anaweza akaharibu na akawa na ruhusa ya kuharibu au akawa ana ruhusa ya kuingilia. Huyu ameleta hoja nyingine, lakini nadhani pia ni ya msingi kuitazama. Bila ruhusa anaingilia. Kwa hiyo, mtu anaweza kuwa na ruhusa ya kuingilia? Nami nilikuwa nalitafuta lile neno "kuingilia", ila kama linaeleweka kwa the *rest,* haina shida.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tupe muda kidogo, unajua tutakuwa na kazi kubwa katika miaka 20 ijayo mpaka tupate istilahi zinazokidhi eneo hili la sheria. Waingereza walipohama kuacha kutumia Kifaransa na Kilatini, imewachukua miaka 300 kufika hapa. Kwa hiyo, tutakwenda na hilo, lakini lengo hapa lilikuwa ni hilo.

**MWENYEKITI:** Sawa. Mheshimiwa Waziri, hili neno "ruhusa" liendelee kuwepo? Nadhani kwa sababu hiki kifungu kinaanzisha kosa, nafikiri linakuwa kama lipo mahali ambapo sipo. Mheshimiwa Mnzava.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuingilia kwa maana ya *interference* ni kosa, hakuwezi kuwa kuna ruhusa ya kufanya kosa. Kwa hiyo, hakuna sababu ya kusema "bila ruhusa", ingeweza kusomeka tu "Anaharibu au anaingilia mali yoyote ya shirika," na isingepoteza maana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshangaa unataka kuondoka kwenye hoja yako ya kuingilia mali...

**MWENYEKITI:** Hiyo ya kuingilia nimeona kama, yaani nimejikuta akili yangu imeshindwa kufikiri jambo la tofauti, kwa hiyo,...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu pale kuna maneno mawili, kuna kuharibu mali, inaeleweka ukisema mtu anaharibu mali, lakini "kuingilia", nadhani ilikuwa kuingilia matangazo au mchakato wa matangazo, *something like that,* lakini huwezi kuingilia mali, yaani mali unaingiliaje? Ukishasema "kuharibu," imechukua na kuharibu mali. Lakini kama "kuingilia", nilikuwa nataka Mheshimiwa Waziri pengine atueleweshe vizuri, ni kuingilia matangazo au? Maana ukisema kuharibu mali, umemaliza kosa, tayari umesha-*establish*.

**MWENYEKITI:** Nadhani wanakusudia kusema *interference with the property of TBC* Mheshimiwa.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anaweza kuwa anaharibu au anaingilia mali yoyote ya shirika au shughuli zozote za shirika. Anayeingilia mali au shughuli za shirika, maana yake ana-*interfere* na matangazo, ana-*interfere* na shughuli hizo ili kulipa *this laboring, for me* ni nzuri sana kwa sababu inakomaza Kiswahili cha kisheria.

**MWENYEKITI:** Sawa, kwa hiyo, hapa itasomekaje?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inaharibu, anaharibu au anaingilia mali yoyote au shughuli za shirika. "Anaharibu mali yoyote ya Shirika au anaingilia shughuli za shirika."

**MWENYEKITI:** Uharibifu wa mali tumetaja hapa kwenye 17. Mheshimiwa Mnzava kwenye Kifungu cha 17 kinaongelea uharibifu wa mali za shirika.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kifungu hicho hicho cha 17 kinazungumzia uharibifu wa mali, lakini hicho cha 18 pia, nilitaka tu nikikumbushe Kiti chako kwamba, kwenye *marginal note* tunazungumzia kuingia kwenye eneo la shirika, kwenye *marginal note* ndiyo kifungu hiki kinazungumzia kuingia kwenye eneo la shirika, kwa hiyo, tutakaporekebisha huku, pia tukumbuke na hilo.

**MWENYEKITI:** Hii (c) inahitajika kuwepo hapo? *Marginal note* inasoma kuingia kwenye eneo la shirika, (a) tumeshakubaliana "anakutwa," (b) tumeshakubali "anakataa kuondoka," itakayokuwa mpya ya (c) akiwa kwenye maeneo ya shirika anapohitajika na mtumishi kutaja zile taarifa zake, anakataa; hii "anaharibu mali" ipo tayari kwenye 17, bado tunaihitaji kuwepo hapa Mheshimiwa?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukaiondoa kwa sababu ipo

kwenye ya kwenye 17, lakini hii ya (c) ni "kuingilia mifumo ya utangazaji na kuingilia miundombinu ya utangazaji." Kwa hiyo, hilo la "kuharibu" maadamu lipo kwenye 17, tunaweza tukaliondoa, lakini hicho (c) sasa kikabaki kikijihusisha zaidi na "kuingilia mifumo ya utangazaji na miundombinu ya utangazaji." *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mbona naona kama inakuwa shughuli, hiki kifungu "Kuingia kwenye eneo la shirika," "mtu yeyote ambaye..." Mwanzo tumesema kuhusu yule anayeingia; pili, yule anayeingia na (d) yule aliyeingia anamzuia huyu kufanya kazi na hii (c) yule aliyeingia anafanya jambo ambalo lipo kwenye 17, siyo Mheshimiwa! Kwa sababu hili la (d) kwa mfano, "Anamzuia mtumishi au wakala wa shirika kutekeleza majukumu yake," tunamzungumzia yule ambaye ameingia, si ndiyo? Sasa huku juu kifungu chetu, leo tutapata changamoto na ninadhani hii changamoto tutaenda nayo katika sheria yoyote tunayotunga kwa Kiswahili, kwa hiyo tuwiane radhi.

Kifungu cha 18 nia yake ni kuzungumzia mtu anayeingia kwenye eneo la shirika, tukasema hivi "Mtu ambaye," halafu unakuja (d) maana ile "mtu ambaye", unaweza kuruka nayo, inasema: "Mtu ambaye (d) anamzuia mtumishi au wakala wa shirika kutekeleza majukumu yake." Hili nalo ni kosa tofauti ambalo halina uhusiano na mtu kuingia. Anaweza kuwa hajaingia popote na anamzuia mtu kufanya hii shughuli, lakini *marginal note* yetu inataka yule ambaye ameingia kwenye eneo.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo zima hili lilikuwa ni *penalty and offences,* yaani haya yote ni kwamba tuna-*create offences* na ndiyo maana ile ya chini sasa ndiyo inatoa *penalty* ambayo sasa imebadilika kutoka hizo shilingi milioni 10, zimeshuka mpaka shilingi milioni mbili. Kwa hiyo, ukiangalia yale yote kuanzia (a), (b), (c), na (d) hayo yote ilikuwa ni kuyafanya haya kuwa makosa na baada ya kuyafanya haya kuwa makosa, adhabu yake ndiyo hiyo ipo kwenye kitako chake hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa yawezekana *marginal note* ikahitajika, kwa sababu hapa lengo ni kusema haya ya (a), (b), (c), na (d) ni makosa; na ukiyafanya makosa yake hayo, adhabu yake ndiyo hiyo ambayo ipo hapo chini ambayo sasa imebadilika na kuwa shilingi milioni mbili na isiyozidi milioni tano kama ambavyo wengi walisema ingawa mimi inanipa jakamoyo. Kipengele (c) ndiyo tulipendekeza sasa tuibadilishe tuondoe neno "wanaharibu" badala yake tuseme "anaingilia mifumo na miundombinu ya utangazaji", halafu hiyo ya kuharibu ingawa ilitakiwa ibaki hapo ili nayo "kuharibu" liwe kosa. Lengo lilikuwa ni kulifanya hili pia la "kuharibu" libaki hapa kwenye (c) ili na lenyewe liwe kosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukatenganisha tukawa na (c) ya kuharibu mali za shirika, halafu tukaongeza mpya ya kuingilia mifumo na miundombinu ya shirika, halafu tukaendelea, anamzuia mtumishi. Halafu *marginal note* tukaona jinsi ya kuiboresha, kwa sababu lengo hapa ni kuweka makosa na adhabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii *marginal note* ya kuingia ndiyo kidogo imetupeperusha huko tulipopeperukia, lakini tuibakize hiyo "kuharibu" kwa sababu hapa tunatengeneza makosa na adhabu. Hilo la kuingilia ninaafikiana nawe, huwezi kuingilia mali kwa maana tunayoitarajia iwe ni kuingilia mifumo na miundombinu ya utangazaji.

**MWENYEKITI:** Katika makosa, mtu atakavyopelekwa sasa mbele ya Mahakama. Tukichukua mfano wa hili kosa moja, nilikuwa nakiangalia hichi Kifungu cha 17 kinatoa adhabu tofauti na nzito zaidi kuliko hiki. Sasa mtu atakapokuwa anashitakiwa, akishitakiwa kwa Kifungu cha 18, adhabu yake ni hii ndogo ambayo Mheshimiwa Waziri inakuletea jakamoyo. Akishitakiwa kwa kosa hilo hilo kupitia Kifungu cha 18, adhabu yake itakuwa kubwa zaidi ambayo wewe itakupa amani.

Sasa kwa sababu haya ni makosa yanayofanana, tukiyaweka sehemu mbili tofauti, maana yake atapata adhabu mbili tofauti. Bora tuweke kwa sababu pia kwa maelezo uliyotoa, kwa kweli ni kosa kubwa, si anaharibu! Huyu ni mharibifu. Kwa nini awekewe hili kosa

ambalo tunamzungumzia yule ambaye ameingia kama kule mwanzo tulivyokuwa tunasema? Bora aadhibiwe na hii ya 17 ambayo ni kubwa zaidi, amefanya uharibifu na ameingilia hayo mambo mengine, hapa kwenye 17 nadhani inaleta adhabu kubwa zaidi.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo nimeafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Kwa hiyo, Waheshimiwa tunaondoa hii (c), tukishaiondoa, hii (d) itasomeka kama (c) kwa sababu bado ni kuingia kwenye eneo la shirika, lakini mtu ambaye ameingia sasa kwenye hilo eneo la shirika, halafu akamzuia mtu kufanya kazi zake; nimeelewa vizuri Mheshimiwa Waziri? *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunaomba tuje na (c) mpya, ile ya kuingilia mifumo na miundombinu ya utangazaji. Tuondoe hiyo ya kuharibu mali, lakini tuseme, ameingilia mifumo na miundombinu ya utangazaji kwenye hii 18.

**MWENYEKITI:** Hebu soma hii 17(1) Mheshimiwa Waziri tuone. 17(1)

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu hataingilia au kutumia kwa madhumuni yoyote au kushiriki katika kitendo kitakachosababisha au kinachoweza kusababisha mabadiliko, uharibifu au kusababisha kuondolewa kwa, au uharibifu wowote wa miundombinu ya utangazaji inayomilikiwa na Shirika.

**MWENYEKITI:** Sasa nikawa nawaza hili kosa ambalo tunataka kulianzisha hapa linaweza kusimama peke yake ili hii *marginal note,* sawa tutaibadilisha, lakini litaweza kusimama peke yake? Yaani litaweza kuingia kwenye hii adhabu? Yaani aina ya hilo kosa tuiweke kwenye hii adhabu ndogo au likae kwenye adhabu kubwa? Kwa sababu adhabu kubwa ni ile ya kwenye 17, tukishaweka hapa kwenye 18 wanasheria tutabishana Mahakamani mpaka basi, kwa nini tutumie Kifungu cha 17 na siyo cha 18 kwa huyu aliyefanya kosa?

Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuiona *angle* nyingine wakati mnazungumza. *Angle* niliyoiona ni kwamba ile 17 ni kama *physical* hivi, yaani mtu amefika na amefanya uharibifu, lakini hii (c) inatusaidia na pengine kama Mheshimiwa Waziri ataridhia itusaidie ku-*capture interference* kwa mfano ya kimtandao. Kwa mfano, wanasema walikuwa wanaingilia matangazo ya *TBC* kwenye taarifa ya habari wakiwa hawapo pale. Sasa nikasema, uharibifu hata kwa hawa *hackers* ni uharibifu, ame-*interfere,* lakini ame-*destroy* matangazo...

**MWENYEKITI:** Hii 17 siyo *physical* Mheshimiwa. Nimejaribu kuiangalia hapa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, 17 siyo *physical*?

**MWENYEKITI:** Aa, yaani hataingilia, hata-*interfere,* siyo *physical,* haina kuingilia. Hii ya 18 huku ndiyo inataka iwe *physical*.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ya 18 ndiyo inataka iwe *physical*?

**MWENYEKITI:** 18 ndiyo *physical,* hii nyingine yaani unapoingilia kokote, umetumia *artificial intelligence,* akili nini inaitwa?

**MBUNGE FULANI:** Mnemba.

**MWENYEKITI:** Mnemba imeshabadilishwa, watu mbona..., akili nini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, akili mnemba.

**MWENYEKITI:** Imeshaondoka kwenye mnemba, ni akili unde. Haya Mheshimiwa Waziri. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafikiana nawe kwamba tuiondoe ile (c) yote kwa sababu hata hilo tunalolizungumzia lipo kwenye 17(1).

**MWENYEKITI:** Ndiyo, shukrani. Sawa.

Waheshimiwa Wabunge, tunaweza kusonga mbele. Sasa nitawahoji kwenye kifungu hiki pamoja na haya...

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna dogo kwenye adhabu pale ambayo tunaibadilisha. Ile anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa *fine* isiyopungua shilingi milioni 10 na isiyozidi...

**MWENYEKITI:** Milioni mbili sasa inasomeka.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, "na isiyozidi shilingi milioni tano."

**MWENYEKITI:** Ndivyo ilivyoandikwa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nilikuwa nasema hilo neno tumelisahau, ingekuwa...

**MWENYEKITI:** Neno "shilingi"!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *yes.*

**MWENYEKITI:** Lipo. Kwenye ya kwangu mimi lipo, au ni wapi hamna? Ya kwangu inasomeka hivi: "Anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa *fine* isiyopungua shilingi milioni mbili na isiyozidi shilingi milioni tano." Kwangu ndivyo inavyosomeka.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi ya kwangu mimi ilikuwa haina.

**MWENYEKITI:** Ipo sahihi, sawa basi shukrani.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji, nadhani tumeweka sawa. Kifungu cha 18 pamoja na marekebisho ya Serikali na haya ambayo Bunge limefanya.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

Ibara ya 19
Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 25

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 26

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 27
*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 28
Ibara ya 29
Ibara ya 30

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 3

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kifungu cha tatu.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha Tatu, nilitaka nikisome, *AG* kisome.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapendekeza sasa kisomeke, Kifungu 3(1): "Kutaendelea kuwepo shirika linalojulikana kama Shirika la Utangazaji Tanzania au *TBC* lililoanzishwa kwa mujibu wa amri ya uanzishwaji wa Shirika la Utangazaji Tanzania kupitia Tangazo la Serikali Namba 136 la mwaka 2007."

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali unajua mimi sijaenda *legal drafting* hivi karibuni. Huo ni uandishi wa sheria wa kawaida au ni *convenience?* Kwa sababu tunatungia hapa ndani, kwa hiyo, inabidi tutafute namna. Ni utungaji wa kawaida! Yaani tunaweza kuchukua sheria mahali au kama hivi *order,* tukaiweka hapa kwa sura hiyo?

Mimi sijaenda *drafting* hivi karibuni, lazima nikiri kuwa mambo mengi yanabadilika, nimesoma kitambo sana *drafting*. Uandishi tu ule wa sheria wa kawaida tunaweza kufanya hivyo au tunapaswa kuweka kwenye *marginal note* au kuweka kile kifungu alichopendekeza Mheshimiwa Waziri mwishoni ili mtu awe anajua hapa tulikuwa kama vile tuna-*reestablish,* lakini ilishakuwa *established* na sheria ambayo tutaitaja sasa kule chini ambayo ndiyo hiyo *Order* ya *President*.

Wataalamu, ninyi si ndiyo mnapelekwa *training* kila siku? Hii ni *drafting,* mimi sijawahi kuona sheria imeandikwa hivyo, lakini inawezekana zipo kwa sababu sheria zipo *in thousands*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mapendekezo tuliyopewa na wataalamu wa uandishi wa sheria inawezekana kufanya hivi.

**MWENYEKITI:** Hapa ndiyo tuna dakika ngapi za Bunge? Hebu fanya ku-*search faster* hapo uniletee mfano wa sheria mojawapo ambayo tumewahi kuweka hivyo. Maana sheria zipo nyingi jamani. Tusije tukatoka hapa tukaanza kushikana mashati hapo nje. Hebu tafuteni *faster* hapo wataalamu.

Halafu naomba ile ilivyoandikwa, ile ya *AG* niletee hapa niione. Mimi mifano niliyonayo ni vifungu vya katiba tu. Hapa ninaona Katiba inaweka *marginal notes* huku na kule, tunaenda huku na nyingine ni hizo sasa za ku-*serve*.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** *I hope* maelezo yako ya sasa hivi hayanichanganyi kama kama yale ya mwanzo.

Mheshimiwa Ramadhan Ramadhan.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yale maelezo ya kwanza ndiyo yalitutoa kwa sababu nilipendekeza tuweke *two offences* na wewe ulikubaliana na yale mapendekezo tufute ile sentensi ya kwanza. Kwa hiyo, yale ndiyo yalitutoa yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi nilikuwa nataka arejee tu kwa sababu sikusikia alivyokuwa anakisoma, kitakavyoonekana. Nilikuwa nakuomba kama Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu atarejea kukisoma tena ili tukisikie vizuri.

**MWENYEKITI:** Haya. Wanasheria, nasubiria nisikie hivi vichwa viwili vimekutana pale. Hata hivyo, kuna hoja hapa na kwa kweli, wataalamu nao wako huku nyuma, kwa hiyo, nao wanatusaidia katika hili zoezi.

**MBUNGE FULANI:** *(Aliongea nje ya mic)*

**MWENYEKITI:** Naam, halijajibu. Kwa sababu, kwa maana ya Shirika la Utangazaji Tanzania, kwa historia ile uliyoitaja Mheshimiwa Waziri ni kwamba, hatukuwahi kuwa na sheria. Sasa hivi Bunge ndiyo linatunga sheria. Pia, ile sheria iliyoanzisha kwa utaratibu wa utungaji wa sheria, ile ni *subsidiary legislation.* Sasa hivi ndiyo Bunge linatunga sheria kwa ajili ya shirika hili.

Kuna madhara yoyote ambayo, kihistoria itaendelea kubaki vile ambavyo umeisema vizuri kwenye hotuba yako, ikiandikwa hapa kwamba, "kutakuwepo na shirika litakalo…" Kutakuwa na shida yoyote kwenye utendaji au kwenye chochote?

Kwa sababu pia, hata kile kitendo cha kusema kwamba, tutaweka kule mwishoni, haiwezekani kwa sababu, hii ndiyo Sheria Mama sasa na ndiyo inatungwa saa hizi. Wanasheria, *Legal Method* jamani, mwaka wa kwanza. Sheria Mama ndiyo inatungwa saa hizi, kwa hivyo…

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wa mwaka wa kwanza tuko hapa.

**MWENYEKITI:** Ninamaanisha kwamba, *Legal Method,* huwa tunasoma mwaka kwanza.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *yes*.

**MWENYEKITI:** Sasa, haya, mwaka wa kwanza, karibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBC* ilianzishwa kwa tamko la Rais. Leo Bunge Linatunga sheria rasmi ya kuanzishwa kwa Shirika la Utangazaji Tanzania. Je, sheria hii itamke waziwazi kwamba, inalifuta lile tamko la Rais au la! Je, ionekane hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana *AG* ameitamka hapa, pamoja na mambo mengine, ilikuwa ina-*cure* kutunza hiyo historia. Hata hivyo, ukiipeleka kule chini ukasema sasa, kwa kuwepo sheria hii, inafuta lile Tamko la Rais, naona inakuwa *a bit* kama; maana Uandishi wa Sheria na wenyewe una busara yake ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeshauri, hata kama inaleta *story*, lakini kama alivyoipendekeza *Attorney General,* ilikuwa inatutunzia, na mtu hawezi kusema kwamba hii sheria iliyotungwa ilitokeaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, anaipata pale pale kwamba, imetokana na lile tangazo la Rais, lakini pia, baada ya hapo tume-*establish* sheria hii na wala haileti fujo. Kwa sababu, kwenye sheria hakuna *clarity* mbaya. Kwenye *Legal Method* tumesoma hakuna *clarity* mbaya kwenye sheria.

**MWENYEKITI:** Haya, tuendelee na mabishano. Wewe si umemaliza hoja yako! Mwingine.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja nimalizie.

**MWENYEKITI:** Haya, malizia.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sheria hata ukisema nimekupa chungwa, lakini nimekupa na mbegu zake, nimekupa maji yake na nimekupa na ganda lake, ni sahihi tu. Wewe endelea kusema tu vyote ulivyovitoa. Kwa hiyo, hata tukisema na tukaongezea maneno, hakuna ubaya wowote kama alivyosema *AG*.

**MWENYEKITI:** Sawa, sasa ngoja. Kwa sababu, leo umejiita mwaka wa kwanza, utungaji wa sheria ni kwamba, huwezi ukafanya mabadiliko kwenye *order* ama *executive order* ama *whatever the name* ama pia *subsidiary legislation*. Kwa nini? Kwa sababu Bunge halitungi sheria hizo, na limekasimu madaraka kwa watu tofauti tofauti. Ndiyo maana hata Waziri tumemwekea za kwake kule, anakwenda huko, anakutananao na hapa tunaletewa tu taarifa. Sasa maana yake ni nini?

Hapa kwanza nimeletewa mfano. Mheshimiwa Waziri, *just in case*, hapa nimeletewa mfano, na huu mfano, nadhani unatuweka sehemu nzuri. Nilikuwa nimeomba mfano wa sheria ambayo yenyewe imeandikwa Kiingereza, lakini siyo mbaya kwa sababu siyo ndefu. "*There shall continue in existence the National Housing Corporation established by the rebuild National Housing Corporation Act*."

Kwa hiyo, hii hapa inazungumzia kuondoa sheria ambayo ilitungwa na Bunge, ila katika ule utaratibu wa kawaida wa utungaji wa sheria, *order,* kwa mfano, nchi ambazo zinaendeshwa kwa hizo *orders,* yaani *President* kaamua mambo fulani, Bunge likiwa halitaki jambo hilo la Rais, linatunga sheria kukataa. Yaani linatunga vifungu sasa na likishatunga, ile *order* inajikuta katika mazingira tatanishi. Kwa nini? Kwa sababu kazi ya Kutunga Sheria ni ya Bunge.

Sasa hoja ni pamoja na kwamba, umesema tunaweza kuweka maelezo, tunaweza kufanya nini? Hoja ya msingi ni kwamba, *Principals* za *Legislative Drafting,* tunaweza sisi tukaweka humu tukiwa tunazungumzia *subsidiary legislation*? Usilitazame kwa hoja nyingine, tunazungumzia tu hiyo *principal,* sisi hapa tunaweza hivyo? Kama hapana, turudi hapa.

Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, SANAA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa hapa ilikuwa ni kuyahifadhi yale yote ambayo yapo sasa na yanayofanywa na *TBC*. Kwa hiyo, tukienda na 3(1) ikawa, "kutakuwepo na shirika linalojulikana kama Shirika la Utangazaji Tanzani *(TBC),*" maana yake ni tutahitaji kuwa na kifungu kingine sasa cha kuyalinda na kuyaendeleza haya yote ambayo yamekuwepo toka *TBC* ilipoanzishwa na ile Amri ya Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, moja, tunaweza tukaiandika hiyo, *legislative drafting* ina *style* nyingi, siyo moja. Moja, tunaweza kuwa na kifungu kwamba, yale ambayo yamefanyika chini ya Amri ya Rais iliyoanzisha shirika hili yataendelea kuwa halali na yatakuwa na nguvu ya kisheria. Tukifanya hivyo, maana yake tutakuwa na *servings provision* bila kusema tunafuta.

**MWENYEKITI:** Hapana, hatufuti.

**WAZIRI WA HABARI, SANAA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutasema yale yote ambayo yalianzishwa na kuendelezwa na Amri ya Rais iliyoanzisha, yataendelea kuwa halali na yatakuwa na nguvu ya kisheria. Halafu hapa sasa tukawa na hiyo "kutakuwepo na shirika linalojulikana kama Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC).*" Halafu tutaongeza hicho kifungu kule kwamba, yale yote ambayo yalianzishwa na yanaendelea kuwepo, yataendelea kuwa halali kwa mujibu wa sheria bila kusema tumeifuta ile amri, lakini tumeyatambua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kwa sababu, pia, *elegance is of essence in legislative drafting,* ili tufanye kifungu hiki kiwe na huo umaridadi, ulimbwende au kupendeza na kueleweka, badala ya kuwa na hayo makochokocho mengi, halafu yanalifanya lisipendeze. Kwa hiyo, tunaweza tukasema kwamba, kutakuwepo na Shirika linalojulikana kama Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)*. Halafu sasa tuongeze kifungu kingine kwamba, "yale yote yaliyokuwa katika Shirika la Serikali *TBC* iliyoanzishwa na Amri ya Rais, Tangazo la Serikali Namba 137 yatabaki kuwa halali na yenye nguvu ya kisheria." Kama hilo litasaidia, nitashukuru.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani pendekezo hilo litatuweka katika mazingira mazuri zaidi. Kwa hiyo, kwa pendekezo hilo, badala ya kuweka hapa kwenye Kifungu cha Tatu, tuweke Kifungu kidogo cha 4, tuweke Kifungu cha 31. Mheshimiwa Waziri, sasa wakati tunaendelea, wewe tusaidie hapo kitasomekaje ili tulihoji Bunge kuhusu Kifungu hicho.

Haya, wakati wanaendelea huko jamani, niwahoji kuhusu Kifungu cha Tatu pamoja na marekebisho ya Serikali.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**MWENYEKITI:** Sawa, sasa wakati wanaendelea kujadili kwa yale maelezo niliyokuwa nimeyatoa mwanzo, ambayo nimepata na ushauri hapa kutoka kwa wataalamu, wakati hiki kifungu ambacho kinahifadhi *TBC* kama ilivyo sasa hivi na yale yote ambayo inayo na siyo kwamba inaanza upya, kile kifungu kwa sababu kinatambua *TBC* imekuwepo na yale yote ambayo inayo, ni muhimu kikawepo pamoja na kwamba ilianzishwa kwa kutumia Sheria Ndogo.

Kwa hiyo, pengine ni kuondoa huo mkanganyiko wa kwamba, Sheria Mama inakuwa inazungumzia Sheria Ndogo. Hata hivyo, hoja ni kwamba, tusipokiweka ni kama vile shirika linaanza leo wakati shirika lilikuwepo. Kwa hiyo, hiki kifungu kinatuweka kwenye hayo mazingira ya kwamba, shirika lilikuwepo, lina mali na kila kitu, ambazo ni mali

zake, zinaendelea kuwa mali zake na siyo kwamba, linaanza upya. Kwa hiyo, nimeona nitoe huo ufafanuzi ili tuwe tumekaa vizuri.

**WAZIRI WA HABARI, SANAA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupendekeza Kamati yako ione Kifungu hiki kipya cha 31 ambacho kitakuwa na *marginal note* ya masharti ya mwendelezo. Pia, mwendelezo uwe wa (*mw* na siyo *mu*), nalisema hilo kwa makusudi kabisa. Masharti ya mwendelezo wa *TS 186* (Tangazo la Serikali la 186 la Mwaka 2007); kifungu chenyewe kisomeke hivi, "Mambo yote yaliyofanyika kwa mujibu wa Amri ya uanzishwaji wa Shirika la Utangazaji Tanzania ya Mwaka 2007, yataendelea kuwa halali na yatatafsiriwa kuwa yalifanyika chini ya sheria hii."

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nadhani hilo linatuweka mahali pazuri. Sasa nitawahoji kwa hiki kifungu kipya cha…

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kuna haja ya ku-*rephrase* tena kidogo. Kama kwenye tangazo kuna mambo yamebadilishwa na sheria ni lazima *tu-reflect* kwenye hiyo *phrasing* kwamba, tutayaheshimu na yataendelea kuwa hivyo, *serve for* yale mambo ambayo yamebadilika. Ama *GN* inapingana na sheria, ili kuweka utaratibu mzuri.

**WAZIRI WA HABARI, SANAA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa turejee kwenye Sura ya Kwanza ya Sheria, *Cap one,* ama sivyo, sasa tutaanza kutunga sheria ambazo zinabeba kila kitu. Naomba tuongozwe na *Cap one*. Hayo yote uliyoyasema yanabebwa na *Cap one* ambayo nimependekeza liwe somo linalojitegemea kwa vyuo vyote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Olelekaita, maelezo haya nimeyaita kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Hii sehemu ya mwisho inasema,

"yataendelea kuwa halali na yatatafsiriwa kuwa yamefanyika chini ya Sheria hii."

Maana yake ni kwamba, kwa sababu, yatatafsiriwa yamefanyika chini ya sheria hii, maana yake ni kwamba, yanajikuta humo kwenye hii mpya. Kwa hiyo, hakutakuwa tena na yale ambayo…; jamani mbona Kiswahili kinaniruka leo!

Yaani hayatakuwepo ya sura mbili. Yote yatakuwa sasa yako chini ya sheria hii. Kwa hiyo, yale ambayo yamebadilishwa, yatajikuta yamebadilishwa na yataendana na sheria hii.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, Kifungu chetu cha 31, sasa nitawahoji kwa kadiri kilivyosomwa. Kwa hivyo, kitakuwa ni kifungu kipya.

Ibara Mpya ya 31

*(Ibara Mpya iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima)*

**NDG. HUSSEIN ATHUMAN – KATIBU MEZANI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake.

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA HABARI, SANAA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2023, napenda kutoa Taarifa

kwamba, Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania wa Mwaka 2024, ibara kwa ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania wa Mwaka 2024, kama ulivyopitishwa na Kamati ya Bunge Zima, sasa ukubaliwe. Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsanteni sana, sasa nitawahoji.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji wanaoafiki hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, kuhusu hoja ya Muswada wa Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania wa Mwaka 2024.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania wa Mwaka 2024 Ulipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Wote mmeafiki. Haya ahsante sana.

Katibu.

**NDG. HUSSEIN ATHUMAN – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria kwa Ajili ya Kuendeleza, Kusimamia na Kuendesha Shirika la Utangazaji Tanzania, Kubainisha Wajibu, Malengo na Majukumu na Mamlaka ya Shirika,**

## Kuweka Masharti Kuhusu Ulinzi na Usimamizi Thabiti wa Miundombinu ya Utangazaji na Kuainishwa Masuala Mengine Yanayohusiana na Hayo

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umeshasomwa mara ya tatu. Muswada ukishasomwa mara ya tatu, maana yake ni sisi, upande wa Bunge tumeshakamilisha kazi yetu ya kutunga sheria. Sasa tutaupeleka kwa Mheshimiwa Rais ili naye aweze kuufanyia kazi kwa sehemu yake kama matakwa ya Katiba yetu yanavyosema.

Hata hivyo, nitumie fursa hii kusema kwamba, Bunge limeshapitisha Muswada wa Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania wa Mwaka 2024. Kwa kusema hivyo, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na mtangulizi wake kwa maneno waliyotumia Kamati.

Ushirikiano ambao umeutoa Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri na Wataalamu wote kwa Kamati ulikuwa ni wa hali ya juu sana mpaka tumefika sehemu nzuri. Kwa hiyo, tunawashukuru sana, lakini pia kwa utayari wenu. Maoni mengi ambayo Kamati imeyatoa, mmeyaleta leo kwenye Jedwali la Marekebisho upande wa Serikali na Kamati haikuwa na sababu ya kuleta hayo kwenye upande wake. Hiyo inaonyesha namna ambavyo mnasikilizana vizuri kwenye ngazi ya Kamati, kwa hiyo, tunawashukuru sana.

Vilevile, tunaipongeza Kamati kwa kuutendea haki Muswada huu. Kwa kweli, mmeupitia vizuri, mmependekeza mambo mengi na mmefika sehemu nzuri. Tunawapongeza sana na pamoja na mambo mengine, mambo ambayo Wabunge wamekuwa wakiyajadili humu ndani tangu shirika hili lianze, mengi mmeyaingiza kwenye sheria.

Kwa hiyo, tunawapongeza kwa ufuatiliaji, kwamba, mambo ambayo yalikuwa yanachangiwa na Wabunge na mengine kama maazimio yamefika na sasa yamekuwa kama sheria na upande wa Serikali wamewasikiliza. Kwa hiyo, Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na

Wajumbe wote wa Kamati hii tunawapongeza sana na pia, tunawashukuru kwa kufanya kazi kwa niaba ya Bunge.

Pia, Wabunge wote ahsanteni sana katika kutunga sheria hii. Wakati mwingine mambo yanakuwa magumu kidogo, lakini tunafika sehemu nzuri. Kwa hiyo, ninawapongeza na kuwashukuru kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu, kuna wakati mwingine kunatokea changamoto na watu wanawaza, sasa leo hapa hii sheria tumeitungaje na mambo kama hayo, lakini Kanuni ya Tano inatoa fursa hiyo, na kwa sababu Utungaji wa Sheria kwa yale ambayo tunakuwa hatujayaona mapema, basi tunayaacha. *Then*, upande wa Serikali wakienda kuyaona mara moja wanayaleta na kutuambia kwamba tubadilishe hapa na tubadilishe hapa. Hata hivyo, yale tunayokuwa tumeyaona tunaleta majedwali kama Wabunge.

Vilevile, kama majedwali ya Wabunge hayakuja na mambo yamekuja hapa, basi Kanuni ya Tano inaweza kutumika ili sheria itungwe kwa ukamilifu, hasa kwa yale ambayo tunakuwa tumeyaona katika utendaji kazi wetu. Pia, kama binadamu huwa kuna kupitiwa hapa na pale, kwa hiyo, yale ambayo tunakuwa hatujapitiwa, basi tunayafanyia kazi kwa sura hii na yale ambayo tumepitiwa, basi Serikali inakwenda huko inaleta marekebisho na tumekuwa tukifanya hivyo. Maana wakati mwingine kuna mambo kama mtu haelewi, badala ya kuuliza, basi anatengeneza jambo na linakuwa na sura tofauti na ile ambayo ilikuwa imekusudiwa.

Kwa hiyo, Bunge linapotunga sheria linaruhusiwa kufanya hiki ambacho kimefanyika hapa ili sheria inapotoka, wananchi wasipate athari, na wakati huo huo Serikali isishindwe kutekeleza hiyo sheria kwa sababu kuna jambo fulani halijafanyika.

Kwa hiyo, nawatakia kila la heri upande wa Serikali. Mheshimiwa Rais atakaposaini Muswada huu, tunawatakia kila la heri kwenye Utekelezaji wa yale ambayo mmeyaeleza humu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ahsanteni sana.

Ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 7.26 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 31 Januari, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*